

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Tatu – Tarehe 15 APRILI, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkuu leo kiongozi wa Upinzani Bungeni hayupo kwa hiyo nitaenda na orodha za wachangiaji na nitakuwa ninakwenda kufuatana na itikadi ya chama, upande, *gender* na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, walioko hapa wasidhani watakwenda kama ilivyoorodheshwa. Kwa hiyo, nitaanza na msemaji wa kwanza Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa.

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi, Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa ni takribani mwaka mzima tangu nilipoanza kuhoji, mimi na Wabunge wenzangu, tulipoanza kuhoji kuhusu ubadhirifu na tuhuma mbalimbali zilizokuwa zinakabili matumizi ya fedha za umma zilizofanywa na makampuni kama Mwananchi *Gold Company*, *Tan Gold*, *Kagoda*, *Deep Green* na mengine mengi ambayo yalitajwa ndani ya ukumbi huu. Kwa nyakati tofauti maelezo mbalimbali yametolewa ndani ya Bunge. Mpaka leo hatujapata taarifa ya kinachoendelea. Bunge hili lenye jukumu la kuisimamia Serikali halijui au wananchi hawajui kama kuna kitu kinaendelea je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu ubadhirifu huo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kabisa Dr. Slaa, hutegemei kwamba kweli nitaweza kujibu maswali hayo uliyoyauliza kwamba mimi nina maelezo juu ya Kagoda, maelezo juu ya nani, *is not possible* nadhani si sahihi kabisa. (*Makofi*)

Mimi ninachowenza kusema ni kwamba jitihada za Serikali zipo zimekuwa zikionekana katika maeneo ambayo yameshaanza kufanyiwa kazi. Sasa kama kuna maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi jitihada za Serikali zitaendelea kwa kadri itakavyowezekana.

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamheshimu Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini Waziri Mkuu ndani ya Bunge hili ndiye aliyetoka kauli ya kwamba hatua mbalimbali zitachukuliwa. Kwa mujibu wa Katiba ibara ya 63(2)(3) Bunge ndilo lenye jukumu la kusimamia na kuihoji Serikali. Kama Waziri Mkuu anasema hawezi kutoa kauli sasa anataka kutuambia kwamba ni nani ndani ya Bunge hili mwenye jukumu la kuweza kutoa kauli kwa masuala mazito kama haya ambayo yeze mwenyewe ndiye aliyatolea kauli? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni kauli nimeitoa, yako mambo ambayo yaliibuka lakini katika mfumo wa hoja binafsi ambayo tumekuwa tunahangaika nayo. Yako masuala ambayo yalitaka mkondo wa sheria moja kwa moja masuala haya nayo yako mahakamani na nikasema kama yako mambo ambayo mengine unaona hayajafikia hatua hizo zote nimesema hapa Serikali itaendelea kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea maana swali la *general litajibiwa general*, si ndiyo. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa James Daudi Lembeli.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 1956 mtaalam wa Sayansi ya wanyama pori kutoka Ujerumani, Prof. Benard Jeemic na mwanaye Michale Jeemic walitengeneza na kutoa filamu ilijojulikana na inaendelea kujulikana kama *Serengeti shall never die*. Kwa tafsiri ya haraka haraka Serengeti itadumu milele. Mwaka 1961 Baba wa Taifa huko Arusha siku chache kabla ya Uhuru wa nchi hii alipokua akihitubia Kongamano la kimataifa kuhusu uhifadhi wa wanyamapori alitoa tamko kuelezea msimamo wa Serikali ya Tanganyika Huru kuhusu Uhifadhi wa wanyamapori na mazingira yao. Hata hivyo, katika siku za karibuni kumekuwa na minong'ono kwamba Serikali karibu itaanza ujenzi wa barabara ya lami, kukatisha katika eneo muhimu la uhifadhi wa Serengeti , minong'ono ambayo mimi binafsi sina uhakika nayo. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu minong'ono hii?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimshukuru sana ndugu yangu Lembeli kwa uelewa mpana juu umuhimu wa hifadhi zetu za wanyamapori na inaonekana amekuwa anafuatilia jambo hili kwa karibu sana. Lakini kuhusu swali lake nadhani tunachowenza kusema tu hapa ni kwamba ni vizuri ameanza kusema ni minong'ono maana ingekuwa kwamba ana uhakika pengine ningeweza nikalijibu vizuri zaidi. Lakini Serikali inatambua umuhimu wa hifadhi za wanyama, lakini wakati mwingine tunakabiliwa na tatizo tu la ukweli kwamba unahitaji barabara ile kwa sababu watu wa Mwanza, watu Mara wanaihitaji. (*Makofi*)

Barabara nayo ina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, suala linakuwa ni kama unabidi upitishe barabara katika hifadhi unaweka utaratibu gani utakaopunguza utaratibu au uwezekano wa wanyama kufa. (*Makofi*)

Kwa sababu nalo hilo tusije tukaliweka pemberi tukafikiri kazi yetu itakuwa ni wanyama tu, wanyama tu. Wanyama wako pale kwa sababu ya binadamu.

Kwa hiyo, la msingi hapa ni kutazama *migating factors* zinazoweza kutusaidia kupunguza athari. Lakini kwa upande wa Serengeti, Serikali inalijua ndijo maana tumesema barabara ile badala ya kupita Serengeti tunatazama *option* ya pili ya kuanzia Mto wa Mbu kwenda kuzunguka kutokea Mgugu na hatimaye tena kurudi katika maeneo ambayo tunaweza kuunganisha. Hiyo yote ni katika kuthamini hilo unalolisema. Lakini inawezekana kukawa na wakati katika maeneo fulani fulani lakini tukajikuta hatuna *option* nzuri kwa sababu mahitaji ya binadamu nayo ni lazima kuyazingatia. (*Makofi*)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu, miezi michache iliyopita kabla ya mvua kunyesha Tanzania ilikubwa na balaa la njaa katika mikoa mbalimbali na wananchi baadhi ya mikoa walilazimika kutumia matunda pori kujihami kama chakula chao na ilipelekeea baadhi wananchi hao kupata madhara ya afya na Serikali ilisema bayana hapa Bungeni na nje ya Bunge kwamba hakuna Mtanzania ambaye atakufa kwa njaa, ingawa mimi sina hakika juu ya hilo ni vyema uthibitishe.

Je, Serikali inajifunza nini juu ya tatizo hili linalotokea mara kwa mara hapa Tanzania na hasa tukijua kwamba tuna mito mingi isiyokauka mabonde yenyе rutuba na wataalam wengi wa kilimo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, unajua maswali mengine yakiulizwa yananipa tabu. Unajua ni kama tunawaambia watu duniani huko kwamba Tanzania haina uwezo wa kulisha watu wake, tunaacha Watanzania wanakula mizizi. Sasa wakati mwingine ni kujaribu kuona jitihada za Serikali katika eneo hili. Ni kweli tulikuwa na ukame na ni jambo ambalo wote tunalijua lakini ni vizuri kukiri jitihada ambazo Serikali imefanya. Tumejitalidi sana mpaka leo unaona hali ni shwari na imetulia, tumeondoa na kupeleka mazao katika maeneo mbalimbali zaidi ya tani laki moja katika jitihada za kuhakikisha Watanzania wanaendelea kuishi kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Sasa unaweza ukawa na kesi moja, mbili hapa na pale, lakini nadhani ni vizuri kutazama jitihada pana na namna ambavyo vimesaidia kunusuru tatizo hili. Tutaendelea sisi kwa nguvu sana na ndijo maana mtoto wa mkulima Waziri Mkuu huyu anakufa na kilimo zaidi kwa sababu hiyo. Kubwa hapa tunaloliona ni kwamba ni lazima Watanzania tujitalidi kutumia kila aina ya teknolojia bora ambayo inaweza ikatusaidia kuongeza uzalishaji. Kwa hiyo moja ni umwangiliaji ambalo tumelivalia njuga sana lakini lazima vilevile tupate zana bora za kilimo na tujitalidi kuongeza uwezo wetu wa ndani ya nchi kupata wataalam, wahandisi wa maji, wahandisi wa *irrigation* hawa pamoja na wataalam wengine katika fani nyingine za kilimo. Na Watanzania wenyewe kubadilika sasa na kuona kwamba ni lazima tufanye kazi kwa bidii sana hasa yale maeneo ambayo tuna uwezo wa kuzalisha zaidi nina hakika tutatoka hapa vizuri sana. (*Makofi*)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushurku pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, juu ya shughuli ya umwagiliaji maji.

Je, Seriali ina mkakati gani wa ziada juu ya kutoa elimu ya uvunaji wa maji katika kipindi hiki cha mvua ambazo katika baadhi ya mikoa ambayo inakumbwa sana na ukame?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri mimi natembea sana hapa nchini. Mheshimiwa Masoud nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge mwenzangu jitihada zilizopo ni kubwa sana na sasa hivi msukumo katika upande wa Serikali ni kutoa elimu zaidi ili watu waweze kutumia mvua hizi zinazomwagika kwa wingi kwa ajili ya kutenga mabwawa. Nilikuwa Tabora juzi nataka niwapongeze sana wananchi wa mkoa wa Tabora kwa kazi nzuri niliyoina. Kwa hiyo, unachokisema ni kweli lazima tuendeleze juhudhi hizi kwa kasi zaidi hasa mikoa ile ya Arusha kwa sababu ndilo eneo ambalo zaidi linakumbwa na ukame tutazame nafasi ambazo tunaweza kuzitumia upande wa Kilimanjaro lakini hata maeneo mengine kwa sababu kubwa ni kuzalisha zaidi ili tujitosheleze kiasi kwamba hata ukipata mahali penye tatizo tuweze kupata chakula cha kutoka ndani kwa wingi kupeleka kwenye maeneo yanayohusika. Nadhani dhamira ni kubwa na tutafikia hapo bila shaka. (*Makofi*)

MHE. ESTHERINA J. KILASI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa moja ya lengo la kuanzisha mpango wa stakabadhi ya mazao ghalani ilikuwa ni kuwasaidia wakulima waweze kukopesheka wakati wakisubiri bei ipande hasa ikiwemo zao la mpunga. Na kwa kuwa hivi karibu au kwa mwaka huu Serikali imezuia kuuza chakula nje ya nchi au nchi jirani. Sasa agizo hili la Serikali limeathiri sana wakulima wa Mpunga katika Wilaya ya Mbarali kwa kukosa soko la ndani na kwa kupata bei ya chini sana na ninavyozungumza sasa maghala mengi bado yana mrundikano wa mpunga ambaa umekosa soko.

Lakini mwezi huu tunategemea kuvuna mpunga mwingine ambaa utaongeza tena maghala kujaa na kufanya huu mpango usiweze kufanikiwa kama ilivyolengwa. Je, Waziri Mkuu utawasaidiaje wakulima hawa ili waweze kuondokana na umaskini kwa kupata soko la uhakika kama ni la ndani au la nje?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijaribu kumjibu dada yangu swalii lake nzuri sana kama ifuatavyo. Suala hili la mauzo ya mazao au baadhi ya mazao yetu nje ya nchi au hata ndani ya nchi ni jambo ambalo limekuwa likisemwa semwa hapa kwa namna tofauti na mara nyingine watu wanapata picha kana kwamba Serikali inakataa au inapata kigugumizi. Mara ya mwisho nilisema hapana, hapa wala si kwamba Serikali inakataa, na nikasema wala hatuogopi kusema tutauza mazao nje, isipokuwa jambo hili linataka tu mtazame uhalisia wa mambo yalivyo ndani ya nchi hii.

Kwa hiyo, kikubwa hapa ni kwamba lazima muwe na mazao ya kujitosheleza kwanza ninyi wenyewe ndani ya nchi. Kwa uhakika kinachotakiwa hapa ni ile ziada ndiyo mnasumbuka nayo kuona muitafutie soko la ndani hata nje pale litakapoonekana lipo. Lakini yako mazao ambayo inabidi tuwe waangalifu sana hasa zao pana la nafaka ya mahindi kwa sababu wengi wanatumia chakula hiki ndiyo maana tunalilinda sana na tutaweza tu kutoa vibali na kuruhusu pale itakapoonekana kwamba sasa tunayo

ziada ya kutosha hapa nchini. Lakini nimegundua vilevile kwa sababu mimi natoka Rukwa na najua vilevile tatizo tunalolipata upande wa Serikali.

Mara nyingi wakulima nao wanaingia ule ugonjwa wa kufikiria kila wakati kwamba bei bila shaka itapanda kesho na wakati mwingine hesabu zile zinawaponyoka hasa mvua zinapoanza kunyesha.

Kwa hiyo, mpunga ni kweli ulitoa matumaini nadhani wengi waliohodhi wakiamini kwamba bei zitaendelea kupanda. Sasa mazao yameanza kuonekana mashambani lakin wale walio wajanja waliuza sana mwezi Desemba kwa haraka sana.

Kwa hiyo, mimi ninachosema tu ni kwamba kama wako pale Mbarali, au Mbeya, watu wenye mpunga, mchele mwingi wanataka kuuza mimi nasema uzeni kama upo mpunga au mchele uuza peleka Malawi kama kuna soko zuri, peleka mahali popote kama kuna soko nzuri kikubwa tu tunataka Wizara ya Kilimo na Ushirika iarifiwe kwa maana ya kusema tuna tani 40,000. Sasa zinatoka kwenda mahali fulani na sisi tuweze kujua kwamba ni kitu gani tumefanya kwa mwaka unao husika. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kwa kipindi kirefu sasa toka yametokea matatizo ya njia ya reli mkoa wa Morogoro wananchi wa mikoa ya Tabora, Kigoma na Mpanda wamekuwa na matatizo makubwa sana ya usafiri wa reli na kumekuwa kuna juhudzi tunazofanya kwa ajili ya kuomba angalau usafiri wa reli ya abiria uanzie Dodoma na madhara makubwa tunayoyapata sasa hivi ni kwamba hata bei za vitu zimepanda sana, nauzi za njia ya mabasi zimepanda sana kwa sababu bado hatujaweza kuona barabara za kutosha upande wa Magharibi. Serikali inawaambia nini watu wa mikoa hii ya Magharibi kuhusiana na masuala ya usafiri wa reli?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kabwa swali lake muhimu sana kama ifuatavyo; kama nilivyosisitiza na mimi ni mdau mkubwa sana kwenye reli ya Kati na nataka niamini kabisa kwamba Ndugu Kabwe kama ningalikuwa na fursa ya kufanya hayo mambo nisingeacha kufanya hivyo kwa sababu na mimi yananimufaisha vilevile ukiona hata Waziri Mkuu naye kanuna kanyamaza ujue bila shaka kuna tatizo la msingi.

Sasa kilichotokea ni nini, wakati mafuriko yametokea kwa sababu ni vitu vimetokea bila kupangwa. Yako mabehewa na ziko *engine* ambazo zilikuwa upande wa pili ambao kumeharibiwa sana. Yako yaliyokuwa vipande vipande sehemu ya pili ambavyo ungeweza ukasema pengine yangeweza kutosheleza kuweza kufanya hiyo kazi kwa nguvu.

Lakini hayo unaona inahitaji vilevile kutafuta mbinu nyingine ya kuona tufanye nini ili ukitaka *ku-roll out* haya maana wakati ule tuliweza kwa sababu angalau tulikuwa na uwezo wa kupitisha mambo mpaka Dodoma kutoka pale ndiyo tunaunganisha sasa mabehewa kwenda maeneo mbali mbali.

Kwa hiyo, tumelitazama sana hili jambo kujaribu kuona tufanye kwa kile kidogo kilichopo na mipaka yake itakuwaje. Lakini bado tumeona uwezo ni mdogo sana tumbakiza reli ya Mpanda ndiyo inasuasua inakwenda pale inarudi. Lakini *impact* yake katika uchumi ni ndogo sana. Kwangu mimi ndiyo maana nasema *is very unfortunately* kwa namna liliyotokea.

Lakini matarajio yangu ni kwamba jitihada zinazoendelea zinaweza kutufanya tukafungua hiyo *portion* yote iliyoharibika ndani ya muda ili tuwezeshe juhudhi hizo nyingine kuanza kufanyika. Kwa hiyo, tunaendelea kulitazama hili tuone tutafanyaje, kama tubebe baadhi ya mabehewa kwenye magari sijui tufanyaje, ili kuongeza uwezo upande huu wa Dodoma tuone kama tunaweza tukafanya kazi. Mheshimiwa Kabwe na mimi ningependa ikafanywa kwa haraka sana.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Waziri Mkuu naridhika na maelezo ambayo umeyatoa kwa sababu yanatoa suluhisho kwa muda mfupi. Lakini tatizo la reli limekuwa ni la muda mrefu limekuwa na migogoro mingi na makampuni ambayo tulibinafsisha kwao.

Lakini sasa kumekuwa na *a goodwill* ya kutoka kwa baadhi ya nchi ambazo zimekuwa na ushirikiano na Tanzania kwa muda mrefu na moja ya nchi hizo ni Ujerumani na ambapo juzi Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani amekuja nchini na reli hii hasa hasa Reli ya Kati, kati ya Dar es Salaam na Kigoma imejengwa na Wajerumani na tayari Wajerumani wameanza juhudzi za kuirekebisha na kuitengeneza upyameli kongwe ya *Mv. Liemba* kwa ajili ya kutunza ile *heritage* kati ya Tanzania na Ujerumani.

Kuna juhudzi zozote ambazo Serikali imefanya kuongea na Deutsche Bahn ambalo ni Shirika la Reli la Ujerumani kuweza kuona kama wanaweza kushirikiana na Shirika letu ili kuweza kuihuisha reli na kuchochea uchumi wa nchi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi tu niseme juhudzi zipo si kwa maana hassa Ujerumani hapana mazungumzo ni mapana zaidi kuliko Ujerumani. Reli hii ni reli kongwe ni ya muda mrefu kusema kweli kwa viwango vyake imepitwa sana na wakati. Tunahitaji reli tofauti kabisa katika mazingira ya sasa, maana kuna sehemu nyingine inakwenda mpaka tani 45 kwa *yard* ambayo ni kiwango kidogo sana hata hiyo 60 ni ndogo sana. Ndiyo maana unaona mradi mpana uliopo sasa ni ule unaotokana na uchunguzu unaoendelea wa kuwezesha reli hii kuwa ni reli kubwa inayotuunganisha na upande wa pili wa nchi za jirani.

Kwa hiyo, *feasibility study* ile imeshakamilika kwa upande wa Isaka *all the way* mpakani lakini sasa hivi tumekamilisha *feasibility study* kutoka Isaka kuja mpaka Dar es Salaam kwa lengo ya kuona namna tunavyoweza sasa kuingiza reli pana yenyu uwezo ukubwa zaidi inayoweza kufanya kazi nzuri zaidi.

Tuna hilo wazo kubwa ambalo ndilo linahitaji mpango na fedha nyingi lakini hili wazo lako kwa maana ya kwamba *in the mean time* tuendelee kutafuta njia nyingine za kuboresha tu hii reli tuliyonayo kwa lengo la kutuwezesha tuweze kuendelea nayo hiyo. Tunaendelea nayo na ndiyo maana tumeanza sisi wenye ili watu wenye *goodwill* baadaye waweze kuja kutusaidia.

Mimi nitajaribu kuona uwezekano wa kuwazungumza na hiyo Serikali ya Ujerumanî kama watakuwa radhi katika jitihada tunazokwenda nazo pengine zikasaidia kuchangia kujaribu kuboresha hii miundombini ya sasa kwa kiwango angalau cha muda mfupi. (*Makofî*)

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kumejitokeza utata wa mpaka katika pori tengefu la Kijerishi Wilayani Magu. Utata huu umepelekea baadhi ya wanavijiji kukamatwa na askari wa wanyamapori. Lakini isitoshe wanapokamatwa wanapigwa sana na kufanyiwa vitendo ambavyo sio vizuri. Kwa msingi ya kwamba haiwatendei haki mbele ya sheria.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, utata huu unapelekea kuleta uvunjifu wa amani kati ya wanavijiji na askari wa wanyamapori kiasi cha kwamba hata malipo wanayolipa hawapewi stakabadhi kwa pesa wanazolipa.

Sasa unaonaje kama ungeunda kikosi kazi cha kubainisha juu ya mgogoro uliopo huu ambao kama hautatafutiwa ufumbuzi wa haraka unapelekea kuweka mgogoro mkubwa zaidi kati ya wanavijiji na askari wa wanyamapori. Lakini sambamba na kuunda kikosi kazi.....

NAIBU SPIKA: Liwe swali tafadhali.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kwamba ili kuepusha migogoro hii kuna haja ya wewe kutoa tamko ikiwa sambamba na kuunda kikosi kazi kubainisha juu ya tatizo lilipo na kupatiwa ufumbuzi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, natambua sana *concern* ya Mheshimiwa Dr. Chegeni na hasa mnapokuwa mpo katika dakika za mwisho hizi si vizuri sana kuchokoza Wapiga Kura kwa sababu nayo ina tatizo lake.

Kwa hiyo, Dr. Chegeni ninachowea kukuahidi tu ni kwamba ili tuweze kujibu kwa ufupi kabisa nitajitahidi tupate wataalam kidogo wanaohusiana na mipaka hii tutashirikiana na watu wa wanayamapori na Wizara husika watakuja Magu watajaribu kuona tatizo ni nini ili kuainisha mipaka vizuri zaidi lakini wakati huo huo na mimi niwasihî sana ndugu zangu wa Magu maana na mimi natoka Mpanda najua matatizo yanayotokana na maeneo haya ambayo yako karibu na Hifadhi. Nawasihi sana ndugu

zangu wa Magu nao wajitahidi kujiepusha kuvunja sheria pale itakapoonekana kwamba mipaka ni bayana. Pengine ndiyo wameingia katika maeneo ambayo si ya kwao. Kwa hiyo, ni sehemu zote mbili mimi nitafanya, lakini nataka niwasihi sana na wao basi wajitahidi kujiepusha na hiyo hali.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru kwa kauli hiyo lakini sambamba na hili ni vema suala la ardhi kupungua wakati wananchi wanaongezeka ni tatizo kubwa na nadhani maeneo ambayo kuna wafugaji na wakulima na wewe ukiwa kama mtoto wa mkulima.

Sijui Serikali inatoa tamko gani au inawasaidiaje, wana vijiji ili waweze kupata mahali pa kufanya kilimo kuendesha shughuli za ufugaji katika utata ambao kwamba ardhi haiongezeki lakini wananchi pamoja na mifugo inaongezeka?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, bado sijapata tatizo hili hasa linatokana na nini. Maana juzi nilikuwa Vetnum pale ka nchi kadogo kuna hekta kama milioni kumi hivi lakini wana idadi ya wakazi milioni 90 na hawana ugomvi juu ya ardhi hata kidogo sisi ni watu milioni 40 na hekta tulizo nazo hapa ni mamilioni sijui yanaingia mara ngapi katika nchi nyingine.

Kwa hiyo, katika hali ya kawaida usingetegemea kwamba jambo hili lingkuwa ni tatizo, lakini nadhani ni jambo tutakwenda polepole, maeneo ni mengi mapori yako wazi mengi tu wala si kidogo lakini nadhani tatizo ni *mind set* za wananchi pale alipo anataka akae hapo hapo. Hata kama wataongezeka wakafika mara tatu, nne, tano anataka hapo hapo ndiyo maana siku za nyuma tuliwahi kuwakaribisha Wachaga Mpanda. Kule tukasema nyie mnagombana gombana hapa Mpanda kuna mapori mengi tu njooni walioweza kuja wakaja, wamejikuta wanaishi maisha ya kawaida tu wala halina tatizo.

Kwa hiyo, kuna ile *attachment* ya maeneo nadhani ndiyo tatizo kubwa, lakini *bottom line*, ni kujitahidi kupitia Wizara ya Ardhi mpango ule wa kupima ardhi nchi nzima ukamilike ili kila mmoja aweze kujuwa eneo lake na ukitaka kuanzisha lingine lazima eneo lingine ambalo litazaa familia nyingine kwa malengo ya kuendelea na maisha.

Kwa hiyo, tutajitahidi ni jambo ambalo nadhani tutaenda nalo pole pole. (*Makofī*)

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mimi ni mdau wa sheria ya Manunuzi ya Umma, Serikali ikipanga Bajeti yake kwa mfano ikasema ni trillion 8 ambapo trillion 6 ni Bajeti ya kawaida na trillion 2 ni fedha za Maendeleo. Basi kwenye hiyo ya kawaida trillion 6 basi 80% inakwenda kwenye manunuzi na 20% inayobaki haiendi kwenye manunuzi. Hiyo ya maendeleo trillion 2, 100% inakwenda kwenye manunuzi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sheria yetu ya Manunuzi ya mwaka 2004 ina upungufu mwingi sana na mimi nimefurahishwa sana kwamba viongozi wa juu ikiwa ni pamoja na wewe mwenyewe na Mheshimiwa Rais mmeyaona hayo. Umewahi kusema mwaka jana ukasema viongozi waandamizi wa Serikali wanachochea sana kununua magari kuliko kununua matrekta. Sasa Serikali iko kwenye mchakato wa kuiboresha hii Sheria ya Manunuzi ili Serikali mtakayounda baada ya Uchaguzi Mkuu ianze na *clean slate*. Sasa ilikuwa ije mwaka jana mwezi wa Oktoba, lakini haikuja. Mwezi wa Februari, 2010 haikuja na sasa hivi haiji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa utalihakikishia Bunge hili kwamba hiyo Sheria ya Manunuzi itaboreshwu kabla ya Uchaguzi Mkuu ili Serikali mpya ianze na *clean slate*?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, analolisema Mheshimiwa Mwambalaswa ni kweli, ni jambo ambalo limekuwa likisemwa na Serikali ilishakubali kulifanyia kazina pengine tungekuwa tumeshaikalisha kwa sasa. Lakini tulifika katikati hapo tukaona zile jitihada ambazo zilikuwa zimefanywa ndani ya Serikali kwa *input* tulizokuwa tumezipata ikawa bado kama hazijatosheleza kututengenezea sheria nzuri.

Kwa hiyo, tuliona tushirikiane na wadau wengine ambao wangeweza kutuwezesha kuwa na uelewa mpana zaidi wa mfumo wa Sheria kama hizi kwa ajili ya ununuzi wa umma. Kwa hiyo, sasa hivi kazi ile inafanywa kati yetu kupitia vyombo vyetu pamoja na *Common Wealth Secretariat*, tuko pamoja na tunajaribu *ku-gain experience* na mifano mingi sana ambayo nchi mbalimbali zimetumia sheria kama hizi ili tuweze kuondoa kasoro zote zilizopo. (*Makofî*)

Kwamba tunaweza tukakamilisha zoezi hilo kabla ya uchaguzi maana nina Bunge moja tu sasa la *Budget* sina uhakika. Lakini sisi tutajitahidi kukamilisha jambo hili mwishoni mwa mwezi huu wa nne ndivyo tulivyokuwa tumekubaliana na wataalamu wote. Tutaona sasa kama pengine wakati wa Bajeti ile wiki ya kwanza tungeweza tukaslot in ule Muswada tutafanya kama nafasi itapatikana. Lakini wote kwa kweli tuna hamu kubwa ili tuweze kuondokana na hili balaa.

Lakini upande wa pili umegusia suala la magari, magari tunaendelea na jitihada hizi tumebanana banana sana Serikalini humu, lakini nitoe wito tu kwamba jambo hili ni letu sisi wote na kwa upande fulani ni suala la *mind set* lakini upande mwingine ni hali halisi tunayoishi nayo.

Lakini tulichokubaliana sasa nadhani nalo litakwisha wala halihitaji sheria, hili ni la kiutawala. Kwa hiyo, tulichofanya ni kwamba tumeamua kulizungumza kwenye Baraza la Mawaziri tuweke aina za magari ambayo ni lazima sasa yawe ni magari ya nchi hii kwa upande wa Viongozi, kundi hili aina gani na kundi hili aina gani maana sasa hivi kila mtu anataka VX hata Mkurugenzi wa Wilaya ya Nkansi anataka VX, ukimwambia

VX na Nkansi wala haviendani kwa hiyo mtu anasema VX kwa sababu anaona kidogo atapandisha mabega kwelikweli. Lakini kusema kweli *it is a very expensive deal.*

Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hilo lakini tunakwenda nalo vizuri nafikiri tutalikamilisha vizuri sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha, napenda kwa niaba yenu kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kujibu vizuri maswali yote mliyomwuliza, kwa sababu tunaendelea kujifunza naomba Wabunge muwe na maswali ambayo ni *précised* siyo yanakuwa marefu. Kwa hiyo matokeo yake tumejibu saba tu badala ya nane. Kwa hiyo, siku nyingine mjifunze hivyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo tunaendelea na shughuli nyingine. (*Makofi*)

MASWALI YA KAWAIDA

Na. 30

Uchafuzi na Uharibifu wa Mazingira Kutokana na Mifugo Wengi - Rufiji

MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Rufiji ilikadiriwa kupokea Ng'ombe 50,000 badala yake wameingia zaidi ya Ng'ombe 300,000 na hivyo kusababisha uchafuzi mkubwa wa ardhi ya kilimo.

- (a) Je, ni lini Serikali itapunguza Ng'ombe hao ili wabaki Ng'ombe 50,000 waliokadiriwa?
- (b) Je, ni lini Serikali itatekeleza wajibu wake wa kutenganisha maeneo ya wafugaji na ya wakulima ili kutenga maeneo yenye rutuba kwa ajili ya kilimo kuendana na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza?
- (c) Je, kuna malambo na majosho mangapi yaliyokwisha jengwa kwa kuwahudumia wafugaji katika Wilaya ya Rufiji?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ilikamilisha zoezi la kuhesabu mifugo katika vijiji 25 vyenye mifugo mingi na kubaini kuwa vina jumla ya Ng'ombe 124,058, Mbuzi 17,279, Kondoo 12,479 na Punda 329. Zoezi hili litafanyika pia katika vijiji 13 vyenye mifugo michache. Baada ya kukamilisha zoezi la kuhesabu mifugo na kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji itafanya tathmini ya kujua uwezo wa ardhi kimalisho (*carrying capacity*) kwa eneo lote lililotengwa kwa ufugaji ili kujua idadi ya mifugo itakayoondolewa wilayani au kuongezwa kulingana na uwezo huo.
- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali imepima vijiji 20 kati ya 98 vilivyopo Wilaya ya Rufiji, ambapo 15 kati ya hivi vimetenga jumla ya hekta 43,687.26 kwa ajili ya ufugaji. Zoezi la kupima vijiji vyote 98 litafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, zoezi hilo linabainisha matumizi ya ardhi kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo yenye rutuba kwa ajili ya kilimo na hivyo kuendana na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza.
- (c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kupitia Mpango wa Kuendeleza Kilimo wa Wilaya (DADPs) imejenga jumla ya majosho matano katika vijiji vya Malange, Muyuyu, Chumbi, Siasa na Nyamwage. Aidha, katika mwaka 2010/2011 Serikali itakamilisha ujenzi wa josho la Muholo na Lambo la Maji kwa mifugo katika kijiji cha Kiwanga ili kuongeza vyanzo vya maji. Vyanzo vya asili vinavyotumika ni mito ya Muholo na Luhoi na mabwawa ya Ilu (Kijiji cha Nyamwage), Rugongwe (Kijiji cha Utete), Weme (Kijiji cha Utunge), na Upa (Kijiji cha Mgomba).

MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu yasiyoridhisha, huwezi kuwa na vijiji 98 ukapima vijiji 20 tu.

Lakini maswali mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo. Kulikuwa na purukushani kubwa sana walivyoingia Ng'ombe hawa na watu zaidi ya watano waliuawawa. Je, Serikali itakuwa na huruma kuwalipa fidia jamaa ya hawa waliouawa katika purukushani hizi?

Kulingana na haki za binadamu na haki za watoto Rufiji ni nchi inayopata mvua ya kutosha, ukitembea katika gari unakuta watoto wa wachungaji wakichunga ya Ng'ombe. Ni lini Serikali itaingilia kati kuwapa haki watoto hawa na kuwajengea shule ili wapate elimu waungane na raia wengine?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Mtulia, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpa pole kwa watu hao waliouawa. Serikali yetu ni sikivu nafikiri italifuatilia hili jambo na kama itaonekana kama kuna umuhimu wa kuwalipa hao watu ambao ndugu zao waliuawa basi nafikiri Serikali baada ya kufanya utafiti inaweza kuamua kufanya hivyo. Lakini jambo hilo kwanza ni lazima tulichunguze.

Kuhusu mambo ya shule Serikali yetu inaamini kwamba kila mtoto anatakiwa aende shule. Kwa hiyo, kupitia mpango wa *DADPs* naamini kwamba kama shule hazipo wananchi waibue mpango huu na kuuweka katika mradi wa *DADPs* na vilevile wananchi kwa sababu ni wafugaji wanawenza kujitolea ili kila mtoto aweze kusoma hivyo ni muhimu kwamba kwa kweli shule zijengwe kwa hawa watu waliohamia huko.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, kuna ubishi mkubwa sana wa uharibifu wa mazingira kati ya wafugaji na wakulima. Je ni lini Serikali itafanya utafiti kuona kwamba huu uharibifu wa mazingira ni mifugo ndiyo inaharibu mazingira au kilimo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Laizer kama ifuatavyo:-

Uharibifu wa mazingira siyo kwamba kila siku unafanywa na wafugaji, ukichukua treni kama unakwenda Mpanda, mimi nilikuwa nasafiri pale utakuta eneo lipo lina miti mingi lakini baada ya kupita tu unakuta mkulima wa Tumbaku amelifyeka, amechoma moto na amepanda Tumbaku. Kwa hiyo, hapo moja kwa moja lawama zinakwenda kwa mkulima. Lakini vilevile kuna wakati nilipokuwa Tabora nikipita mahali unakuta muda mfupi wafugaji wamekuja wamefyeka mahali wamekata miti wamechona na wameleta Ng'ombe pale.

Kwa hiyo, inategemea kwani kuna wakati mkulima anaharibu mazingira na kuna wakati wafugaji wanaharibu mazingira. Lakini Serikali ko imara kuhakikisha kwamba mazingira yanapoharibiwa hatua za haraka zinachukuliwa na inapobidi kama itabidi tufanye utafiti kubaini mahali ambapo mazingira yanaharibiwa Serikali itafanya hivyo.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MHE. SALIM HEMED KHAMIS)
aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilipongezwa na Watanzania wengi pale ilipokamata meli ya uvuvi ikivua Samaki katika eneo la Tanzania kinyume cha Sheria:-

- (a) Je, kwa nini zoezi hilo halikuendeleza ili kulinda raslimali hiyo muhimu kwa uchumi wa Tanzania?
- (b) Je, Serikali imejifunza nini kutokana na zoezi hilo ili kasoro zilizojitokeza zisirudiwe tena?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, napenda kujibu swali la Na. 5455 la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye vipengele a na b kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, zoezi la kupambana na uvuvi haramu hususan katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*EEZ*) linaendelea na halikukoma baada ya kukamata meli iliyokuwa inavua katika eneo hili mwezi Machi, 2008. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Kusimamia Uvuvu katika Bahari Kuu Na. 3 ya mwaka 1998 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2007 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2009, Serikali imeanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvu katika Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority (DSFA)*) yenye Makao Makuu Zanzibar. Mamlaka imekwishaanza kazi na ndicho chombo kitakachosimamia masuala yote ya uvuvi ikiwa ni pamojana kuhifadhi raslimali zote za uvuvi katika ukanda huo.
- (b) Mheshimiwa Spika, katika kukamata meli ya uvuvi ikivua Samaki bila kibali katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari eneo la Tanzania na uendeshaji wa kesi inayoendelea Mahakamani, hakuna kasoro zilizojitokeza kwa kuwa Sheria zote za Kitaifa na Kimataifa zilifuatwa na kesi bado iko Mahakamani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shoka nadhani hutaingia kwenye kesi iliyoko Mahakamani.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa, pamoja na kukamata meli hii na wafanyakazi wake kupelekwa Mahakamani na pamoja na kuunda Mamlaka ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja, lakini bado kunaonekana kuna meli za kigeni zinaendelea kuvuna raslimali hizi

za Watanzania bila ya kuwa na kibali. Je, Serikali ni lini itakomesha suala hili ili raslimali za Watanzania zisiendelee kuvunwa na watu wa nje?

Swali la pili, kwa kuwa Waziri wa Wizara hii ni hodari wa takwimu anaweza akalieleza Bunge hili ni faida gani na hasara kiasi gani zimepatikana kutokana na meli hii iliyokamatwa?

NAIBU SPIKA: Meli iliyokamatwa Mheshimiwa Waziri usijibu kwa sababu kesi iko Mahakamani, unajibu lile la kwanza.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Nilikuwa nimesimama kumweleza kwamba sitajibu lile swalii kwa sababu bado liko Mahakamani, kwa hiyo tungkuwa tunaingilia uhuru wa Mahakama na ile kesi imeanza tangu meli ile ilipokamatwa mwezi Machi, 2008.

Kuhusu swalii la pili kwamba ni hatua zifi zinachukuliwa na Serikali, baada ya kupitishwa Sheria ya *Deep Sea Fishing Authority* ya mwaka 2007 hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa na hivi karibu zaidi ya Dola mia sita elfu zimeingia kwenye akaunti baada ya kupata kibali cha meli kutoka Spain kuanza kuvua. Lakini pia tumesaini makubaliano na meli kutoka Japan zaidi ya 30 ambazo nazo zitaanza kuvua.

Kwa hiyo, Sheria hii kadri itakavyokuwa inatekelezwa tunaamini kwamba uvuvi haramu utakuwa umekomeshwa katika *Exclusive Economic Zone. (Makofi)*

Na. 32

Kushuka kwa Kiwango cha Ufaulu Kidato cha Nne – 2009

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM aliuliza:-

Kwa kuwa, kiwango cha ufaulu cha matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne kwa mwaka 2009 kilishuka sana ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2008 na kusababisha hisia tofauti katika jamii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha dosari hiyo kwa mwaka huu 2010?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA)alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa kiwango cha ufaulu katika matokeo ya mtihani ya Kidato cha Nne mwaka 2009 unaonyesha kushuka kutoka 83.69% (2008) hadi 72.51% (2009).

Kutokana na mwelekeo huo Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti kukabili ana changamoto zilizochangia hali hiyo. Hatua hizo ni pamoja na kuzipatia shule za Sekondari za Serikali:-

- (i) Vitabu na vifaa vya kutosheleza kufundishia na kujifunzia;
- (ii) Maabara zenyne vifaa na kemikali za kutosheleza;
- (iii) Kutoa mafunzo endelevu kazini kwa Walimu;
- (iv) Kuboresha ufuutiliaji wa tathmini ya ufundishaji na uelewa wa wanafunzi katika masomo;
- (v) Walimu wa kutosheleza pamoja na kuboresha mazingira yao ya kazi; na
- (vi) Wakuu wa shule walipata mafunzo ya uongozi ili kuimarisha usimaizi na uendeshaji wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mikakati hii tulishaanza kutekeleza na ufuutiliaji zaidi utafanyika katika utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari yaani MEM2.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali dogo moja la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kutoboresha mishahara ya Walimu, kutolipa madeni yao kwa wakati ni moja ya chanzo kikubwa kilichopelekea wanafunzi hao kufeli kwani Walimu wamekuwa wakihangaika kujitafutia riziki kwa njia nyingine.

Je, uko tayari kuboresha mishahara na kulipa madeni yote ya Walimu kama inavyostahili kwa wakati wake?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kushuka kwa ufaulu na maslahi ya Walimu na mazingira yao ni factor moja tu. Kushuka kwa ufaulu kitaalam kunawenza kukawa na sababu nyingine zinazohusu pande tatu kwa maana ya upande wa watekelezaji, upande wa wanafunzi na upande wa wazazi.

Serikali kwa nafasi yake imeshafanya vya kutosha kwani madai ya Walimu yamelipwa kwa kiasi kikubwa, Bunge lililopita la kumi na nane tulitoa kauli kama kuna yeoyote ambaye bado hajaridhika milango iko wazi na kama wewe Mheshimiwa Mbunge unao unaowafahamu basi walete kwangu. Suala la kusema Wizara ya Elimu itoe tamko itaboresha mishahara hili nilizungumza kwa lugha tofauti, Walimu ni sehemu ya watumishi wa Umma, mchakato wa kuboresha maslahi ya watumishi utakapokuwa unatekelezeka basi na wao ni sehemu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa kauli thabiti kwenye Bunge hili. Suala la kushuka ufaulu lisielekezwe kwa Serikali peke yake, wazungu wana methali inayosema *it take too to tango*. Lazima wazazi na wao waelekezwe juhudzi za kufuatilia maendeleo ya watoto wao na wanafunzi wenyewe lazima watambue wajibu wao wanapokuwa shulenii na Serikali kwa pamoja tunatambua dhamana yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

Na. 33

Wanafunzi Kukoseshwa Masomo kwa Sababu ya Michango

MHE. DR. IBRAHIM SAID MSABAHA aliuliza:-

Licha ya Serikali kupiga hatua kubwa ya kuanzisha Shule za Sekondari za Kata na kupunguza karo kufikia Shilingi 20,000/=. Lakini mafanikio nayo makubwa yanadhoofishwa na michango mingi wanayotakiwa wazazi walipe ambayo wengi wana kipato duni.

- (a) Je, Serikali inafahamu kuwa licha ya wanafunzi wengi wanaochaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza, wengi wao hurudishwa nyumbani kwa sababu ya kukosa michango?
- (b) Je, ni lini Serikali itachukua hatua dhidi ya wahusika ili wanafunzi waweze kuendelea na masomo yao?
- (c) Je, Serikali ipo tayari kufanya uchunguzi mahususi kwenye baadhi ya shule za sekondari hasa Kibaha Vijijini ambako tatizo hili limekithiri?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZOYA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini, lenye sehemu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali licha ya kutoa waraka unaofuta michango yote mwaka 2001, ilichunguza na kubaini kuwa bado kuna michango mingi inayochangishwa

katika shule za Sekondari. Aidha, imebainika baadhi ya shule zilikuwa zikichangisha michango zaidi ya shilingi laki moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo Serikali ilitoa mwongozo kuhusu aina ya michango inayokubalika kuchangishwa kwa shule zote za Sekondari nchini nayo ni:-

- Ada shilingi 20,000/= kwa shule za kutwa na shilingi 70,000/= kwa shule za bweni;
- Mchango wa dawati shilingi 15,000/=;
- Mchango wa ulinzi shilingi 5,000/=; na
- Mchango wa taaluma shilingi 15,000/=.

Lakini michango hii pia inategemea na Board kuna wengine wana taalum shilingi 10,000/= halafu kuna rim ya karatasi shilingi 5,000/= kwa hiyo inatofautiana kwa kibali maalum.

Jumla ya michango yote kwa shule za kutwa ni shilingi 60,000/= na kwa shule za bweni shilingi 110,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kubainisha michango halali kwa wanafunzi wa Serikali Wakuu wa Shule hawapaswi kuwarudisha wanafunzi nyumbani kwa kukosa michango. Naomba kurudia tafadhali. Pamoja na taarifa ya kubainisha hali halisi ya michango inayopaswa kuchangwa, wakuu wa shule hawapaswi kuwarudisha wanafunzi nyumbani kwa kukosa michango. Aidha, inapobainika kuwa wapo wanafunzi wanaorudishwa nyumbani kwa kukosa michango ya shule Serikali huchukua hatua stahili mara moja.

Mheshimiwa Spika, Serikali natoa agizo kwa Afisa Elimu wa Wilaya ya Kibaha Vijijini kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Wilaya kufanya uchunguzi ili kuwabaini Wakuu wa Shule wanaowarudisha wanafunzi nyumbani kwa kushindwa kutoa michango. Aidha kuwafutilia wale wanaokusanya michango zaidi ya kiwango kilichowekwa na Serikali na kuwachukulia hatua madhubuti.

MHE. DR. IBRAHIM SAID MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanzza kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha na mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa inasemekana kwamba sababu kubwa ya michango mbalimbali inayotozwa katika shule hizi inatokana na ufinyu wa Bajeti za hizi shule na mahitaji mbalimbali ambayo yapo katika hizi shule.

Je, Serikali ina mpango gani kwa ujumla wa kuhakikisha kwamba inaboresha Bajeti ya hizi shule kila wakati ili taratibu tuweze kuondokana na michango hiyo hata hizo Shilingi 20,000/= na Shilingi 70,000/= ambazo zinazungumzwa kwa ajili ya wanafunzi wa kutwa na wa bweni?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZOYA UFUNDI(MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalil Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaboresha Bajeti kwa shule za Serikali pale tu ambapo na yenyewe itakuwa imepata fedha za kutosha.

Naomba tu nitoe taarifa kwamba tunapeleka fedha kwa ajili ya fidia ya ada, tunapeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na matumizi mengine. (*Makofi*)

Lakini nikiri hapa kwamba bado kiasi hicho cha fedha hakitoshi, Bodi za Shule zimepewa mamlaka kukutana na wazazi ili kuweza kujadili maendeleo ya shule zao. Tumekuwa tukitoa maelekezo endapo wanaona wanahitaji kuchangia zaidi ya agizo la Serikali kibali kinatolewa na Kamishna wa Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kusema kwamba Bodi zisifanye hivyo kwa sababu ruzuku inayotolewa na Serikali inachelewa, ni ndogo na kama tukifuta michango yote hali ya shule hizi hasa hizi za Kata itakuwa mbaya sana. Kwa hiyo, naomba tu hekima itumike na Bodi za Shule ziwe makini ili kuhakikisha azma inatekelezeka.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa, shule nyingi zimekuwa zinawarudisha watoto kutokana na michango ikiwemo na ada hasa wakati wanapokaribia kufanya mitihani na kuwafanya hawa watoto kuweza kufeli kwenye mitihani yao na wakati mwininge watoto hawa wako mpaka hata wanaoishi kwenye mazingira magumu inabidi warudi.

Je, Wizara inatoa tamko gani la kufanya Walimu wasiwarudishe hawa watoto wakati wanakaribia kufanya mitihani?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZOYA UFUNDI(MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu nimetoa tamko kwamba Wakuu wa Shule kwa sababu yoyote ile hawapaswi kuwarudisha wanafunzi ili wasipoteze muda wao wa masomo na kwamba nijalize kwa kusema waalimu na wakuu wa shule wawasiliane na Kamati zao au Bodi za Shule ili wazazi wale ambao kwa sababu moja au nyine hawataki kulipa basi wakutanishwe na Bodi na adhabu hiyo wasipewe wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, uchunguzi unaonyesha kwamba baadhi ya wanafunzi hata pale wanapopewa zile fedha hawazifikishi, tunazo hizo kesi na Mheshimiwa Mbunge akitaka ushahidi anitafute nitamwelekeza. Kwa hiyo, niseme kwamba wanafunzi nao waonyeshe uadilifu wakipewa zile fedha wazifikishe kwa Walimu wao.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa kuwa kuna familia zenye kipato cha chini na wengi wao wanalea watoto yatima, watoto hawa wanapofukuzwa masomoni au wanapofukuzwa shule hawaoni kwamba hao Walimu wanaofanya kitendo hicho wanakiuka ile sera nzuri ya Serikali ya ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwamba kila mtoto apate elimu sawa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZOYA UFUNDI(MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia wanafunzi yatima Serikali Kuu ina utaratibu wake wa kuwatambua kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Halmashauri, Mkoa hadi Taifa. Wanafunzi wale ambao tayari wameshabainishwa orodha yao ikiwasilishwa Serikalini wanasomeshwaa na Serikali na hawapaswi kubughudhiwa.

Hata hivyo, bado kama wapo ambao hawajabainika na kwa kuwa hivi sasa Shule za Sekondari ziko chini ya TAMISEMI tunaomba Wakurugenzi wa Halmashauri waagize

zoezi hilo kufanyika. Pamoja na hayo bado tamko liko pale pale kwamba mwanafunzi asirudishwe nyumbani kwa kukosa michango ya shule. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofī*)

Na. 34

Wilaya ya Liwale Kupatiwa Umeme

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA (K.n.y. MHE. HASSAN C. KIGWALILO) aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Liwale umekuwa haupati umeme wa uhakika kutokana na uchakavu wa majenereta na kwa kutopatikana kwa vipuli husika kwa wakati muafaka:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kurekebisha hali hiyo kwa manufaa ya Wananchi wa Liwale?
- (b) Je, kwa nini hadi sasa hakuna kinacholeweka juu ya Wilaya ya Liwale kupatiwa umeme wa gesi kutoka Mnazi Bay au Songosongo?
- (c) Je, Serikali haioni kwamba ni vyema kuipatia Wilaya ya Liwale jenereta mpya?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Chande Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia kwa karibu suala hili na kwa muda mrefu sana. Awali, taarifa zilizokuwepo ni kwamba, tatizo la upatikanaji wa huduma ya umeme Liwale lilikuwa ni la upatikanaji wa vipuri. Mitambo iliyopo Liwale ni majenereta matatu ya aina ya *Rolls Royce*, yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa jumla ya kW 600, kwa maana kW 200 kila moja. Mwaka 2008 jenereta moja iliharibika na ili iweze kufanya kazi tena, inahitaji ifanyiwe matengenezo makubwa (*major overhaul*). Kwa hiyo, kwa kipindi hiki mashine mbili zinafanya kazi na zinakidhi mahitaji ya Liwale kwa asilimia 80. Jana tarehe 14 Aprili, 2010, mashine moja ilisimama na hivyo kwa leo hii Liwale inapata umeme wa kW 200 tu, sawa na asilimia 40 ya mahitaji. Mashine hii imeanza kufanyiwa matengenezo leo na inatarajiwa kukamilika tarehe 17 Aprili, 2010. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala la umeme wa Liwale, Wizara yangu imelipa kipaumbele na tunalifuatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye maelezo ya utangulizi, pamoja na uchakavu wa majenereta ya kuzalisha umeme Mjini Liwale, Serikali kuptitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), imekuwa ikiifanya matengenezo mitambo hiyo na hivyo kuendelea kuupatia Mji wa Liwale huduma hii muhimu ya umeme. Aidha, Serikali itahamisha mitambo miwili ya kuzalisha umeme kutoka Ikwiriri mara tu Mji wa Ikwiriri utakapopata umeme kutoka mitambo ya gesi ya Somanga na hivyo kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mji wa Liwale.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya tathmini pana ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili na njia rahisi na ya gharama nafuu kuupatia umeme Mji wa Liwale ni kuhamisha mitambo miwili yenyewe uwezo wa jumla ya 848 kW kutoka Ikwiriri ambayo inatosheleza mahitaji ya Mji wa Liwale. Hii inatokana na gharama kubwa ya ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 66 kutoka Masasi hadi Liwale ili kutumia umeme unaotokana na gesi ya Mnazi Bay unaozalishwa na Kampuni ya ARTUMAS.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuipatia Wilaya ya Liwale jenereta mpya maana jenereta zitakazotoka Ikwiriri zitatoshya kukidhi mahitaji ya umeme wa uhakika kwa Mji wa Liwale na Vitongoji vyake. Hii inatokana na matengenezo makubwa ya majenereta hayo ya Ikwiriri yaliyofanyika mwaka 2009. Hivyo, bado mitambo hiyo ina uwezo mkubwa wa kuzalisha umeme pasipo ukarabati mkubwa kwa muda mrefu.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali mara kadhaa ilikuwa inaahidi kupeleka spea kwa wakati muafaka ili kuleta umeme bila ya kuwa na matatizo; na kwa kuwa mara kadhaa Serikali hiyo hiyo ilikuwa ikichelewa sana kupeleka hizo spea hivyo kupelekea Wananchi wa Liwale kupata shida; je, Serikali haioni kwamba sasa hivi ni wakati muafaka kupeleka spea hizo kama ilivyoahidi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yangu ya msingi, nimetaja mpaka mashine inayotumika pale kuwa ni *Rolls Royce*; kwa bahati mbaya katika mashine nyingi zilizokuwepo TANESCO *Rolls Royce* ni mashine ya kipekee. Kwa hiyo, hata ile mashine ilipopata matatizo mwaka 2008 spea zake ziliorodheshwa, lakini kwa sasa hivi imebainika kwamba, kuliko kuingia kwenye gharama ya kuifufua hiyo mashine ambayo itahusisha *major overhaul* na tatizo likitokea bado tunakwama kwa sababu ni mashine adimu; tumeamua kuchukua hizi mashine mbili za Ikwiriri ambazo zimeshafanyiwa matengenezo zinafanya kazi vizuri nazo zitapata umeme wa gesi kutoka Somanga Fungu ndani ya miezi sita au saba hivi.

Kwa hiyo, tukishachuka zile mashine mbili tukizifunga pale tunaongeza kW 800 juu ya kW 600, mahitaji ya Liwale ni kama kW 900 hivi, tunaamini kabisa kwamba huu utakuwa ni ufumbuzi mkubwa kwa sababu siyo tu kwamba utakuwa na umeme wa ziada, lakini pia kutakuwepo na umeme wa akiba.

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo ya Liwale hayana tofauti na matatizo ya Kilwa; na kwa kuwa Wananchi wa Kilwa wamekuwa na matumaini ya kupata umeme wa Songas bila ya mafanikio kwa muda mrefu; na kwa kuwa tatizo hili pia linapotokea la umeme Kilwa huletw majenereta ambayo siyo mapya; je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini kuhusu Wilaya ya Kilwa ambayo inacho chanzo cha umeme ambacho ni Songas hakipati umeme na majenereta haya tunayoletewa ni makuukuu; Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna umuhimu wa kuleta jenereta mpya kwa sababu tumeshakata tamaa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Kilwa inapata umeme wa jenereta. Ni kweli kanda nzima ile kuanzia Mafia, Kilwa, Lindi, Liwale na Nachingwea, majenereta yaliyokuwepo pale hadi yaliyokuwepo Masasi yamekuwa hayafanyi kazi vizuri na ndiyo maana katika kipindi hiki tumejaribu maeneo yote haya, pale ambapo inapatikana rasilimali ya gesi asilia kutoa umeme huu wa jenereta na kuleta umeme wa gesi asilia ambao una uhakika zaidi na umeme nafuu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Kilwa itapata umeme kutokana na Mradi wa Umeme wa Somanga Fungu, gesi inayotoka kwenye Visiwa vya Songsongo inakuja pale Somanga Fungu halafu nusu ya gesi inarudishwa Wilaya ya Kilwa na nusu nyingine inakuja Wilaya ya Rufiji kuanzia Utete, Ikwiriri mpaka Bungu. Mradi huo ulikuwa umechelewa kwa sababu kulikuwa na migogoro ya wakandarasi, lakini migogoro hiyo imemalizika na tunataraji kwamba, Juni 2010, awamu ya kwanza ya Mradi huo utakamilika ambao utapeleka umeme Wilaya yote ya Kilwa kuanzia Kilwa Mjini na kwenda mpaka Utete kwa Mheshimiwa Prof. Mtulia. Awamu ya pili ya Mradi huo utakamilika Desemba, 2010 baada ya kukamilika taratibu za kuvusha nyaya za umeme kwenye Daraja la Mkapa na hivyo kupata umeme Ikwiriri, Kibiti mpaka Bungu.

Na. 35

Kupeleka Umeme Katika Maeneo ya Jimbo la Magu

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (K.n.y. MHE. RICHARD M. NDASSA) aliuliza:-

Kwa kuwa umeme ni chachu ya maendeleo na kwa sasa umeshafika katika maeneo ya Tallo Sekondari na Bukimbwa Station:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika maeneo ya Ibindo, Kadashi, Nyashana, Iseni Sekondari, Maligisu na katika Mji wa Kabilia katika Jimbo la Magu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Magu na Jimbo la Sumve ni Majimbo ambayo tayari yamefikiwa na umeme wa Gridi ya Taifa, ambapo katika Jimbo la Magu umeishia katika Kijiji cha Nyashimo na Busega na katika Jimbo la Sumve umeishia katika Mji Mdogo wa Sumve (*Sumve Centre*). Aidha, hivi karibuni mradi wa kupeleka umeme Malya umefikisha huduma ya umeme mjini hapo na sasa kazi za usambazaji zinakamilishwa. Umeme huu wa gridi katika Majimbo haya amba ni wa msongo wa kilovoti 33, unachukuliwa kutoka Mwanza katika Kituo cha Umeme cha Nyakato. Mkao wa Mwanza ni mionganoni mwa mikoa ambayo Wilaya zake zote zimefikiwa na umeme wa Gridi ya Taifa. Licha ya kwamba, Wilaya zote za Mwanza zinafikiwa na umeme wa gridi, kama ilivyo kwa maeneo mengi ya nchi yetu, hivi sasa Mkao umekumbwa na matatizo ya upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo hayo yamechangiwa na umbali wa maeneo ya Wilaya za Mkao na mtandao mpana wa usambazaji kutokea Nyakato na uchakavu wa njia kuu za usambazaji zinazochangia upotevu wa umeme. Kwa kuzingatia hayo na umuhimu na mchango wa kiuchumi wa Mkao huu kwa Taifa letu, Serikali imefanya maamuzi ya makusudi ya kuwekeza kwenye mradi wa uzalishaji wa umeme wa MW 60 ili kuboresha uhakika wa upatikanaji wa umeme katika Mkao huo na hatua za zabuni za mradi zinakamilishwa hivi sasa. Mradi huu ukikamilika, Mkao wa Mwanza na Wilaya zake zote, utapata umeme wa uhakika na mtandao wa Taifa utapata uimara zaidi (*Grid Stability*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, pamoja na maelezo hayo ya utangulizi, maeneo ya vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, tathmini ya kuvipatia umeme vijiji hivyo vya Ibindo, Kadashi, Nyashana, Iseni Sekondari, Maligisu na Mji wa Kabilia katika Jimbo la Magu imekamilika mwezi Machi, 2010. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 kilometra 36 na msongo wa kilovoti 0.4 kilometra 24.5 pamoja na ufungaji wa transfoma tisa. Maombi ya kufadhili mradi huu unaokisiwa kugharimu jumla ya shilingi 3,646,500,000.00 yanaandalialiwa ili yaweze kuwasilishwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) mwezi huu wa Aprili, 2010 kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua ya sasa gharama hizi ni kubwa na ni vyema nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, kipaumbele ni kuboresha upatikanaji wa umeme Mkao wa Mwanza, sambamba na kuongeza mtandao wa upatikanaji wa umeme kwenye maeneo ya mkoa huu na maeneo mengine ya Kanda ya Ziwa, kama alivyoomba. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kufanya kazi kwa pamoja ili tupate ufumbuzi wa masuala hayo kwa ufanisi na kwa manufaa na maslahi endelevu ya Wananchi wa Mkao wa Mwanza.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza sana TANESCO na Serikali kwa ujumla, kwa kukamilisha tathmini ya kuvipatia umeme Vijiji vya Ibindo, Nyashana, Maligisu na Mji Mdogo wa Kabilia amba ni upo Jimbo la Magu na Tarafa ya Ndagalu.

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Ndagalu ambayo ina uzalishaji mkubwa sana wa mazao ya kilimo, mifugo na kadhalika, haijapata umeme kabisa Tarafa nzima. Sasa pamoja na Waziri kusema kwamba wameshapeleka maombi hayo REA mwezi huu; je, Mheshimiwa Waziri anawaambia nini Wananchi wa Ndagalu; wasubiri mpaka lini ili nguzo zianze kutandazwa na hatimaye umeme uanze kupatikana?

(ii) Umeme uliopelekwa Sumve unatokea Kisesa Jimbo la Magu lakini unapitia katika Vijiji vya Kanyerere na Kolomije na pale Kolomije tayari wameshaweka mitandao ya kufunga umeme; Mheshimiwa Waziri anawaambia Wananchi wa Kolomije kwamba watawashiwa lini umeme pale? (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Yaani vijiji vyote hivyo lazima uvijue, basi itabidi ujibu kwa kifupi tu hapo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la Tarafa ya Ndagalu tumesema kwamba, miradi ile ilipofanyiwa tathmini jumla ya gharama zote ni shilingi 3.645 bilioni. Labda nimpe tu picha kwa kifupi kwamba, kwa mwaka huu REA ilikuwa ianze na shilingi bilioni 20 na mpaka sasa hivi wamepokea shilingi bilioni nane au tisa hivi. Kwa hiyo, kuna miradi mingi sana ambayo tayari ilikuwa inasubiri utekelezaji, tunatarajia kwamba kadiri pesa zinavyozidi kupatikana, tutaanza utekelezaji wa namna fulani.

Kwa hiyo hii miradi iliyokuwepo hapa, huu mradi peke yake shilingi bilioni 3.6 ni mradi mkubwa. Sasa umeniomba nitoe kauli kwa ajili ya Wananchi wa Ndagalu; mimi nasema kwamba, kwa kuwa mradi huu unaweza kufanywa kwa awamu, basi naomba unipe ruhusa kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, niwasiliane na TANESCO wafanye tathmini ya awamu ili tujuje utekelezaji wa mradi huu unaweza kufanywa vipi ili usizidi kuchelewa na Wananchi wa Ndagalu ambao wana harakati kubwa za kiuchumi hasa wavuvi umesahau kuwataja, waendelee kupata huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Kijiji cha Kolomiji, nadhani swalii hili pia nimelipokea kutoka kwa Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili. Kwa kuwa sasa hivi umeme unapita pale juu ukienda Wilaya ya Magu na TANESCO wameshasema kwamba zipo nguzo za kupeleka pale, mimi nadhani kwa kuwa nguzo zipo na umeme unapita juu, tuwaulize TANESCO gharama za kuushusha umeme kwa maana ya kuupatia transfoma na kadhalika na ni jambo ambalo sitarajii kuwa na gharama kubwa. Ninaomba nimhakikishie kwamba, nalo tutaliangalia lakini bado nasisitiza tatizo kubwa ni ubora na kiwango cha upatikanaji wa umeme Mkoa wa Mwanza, jambo ambalo linaloshughulikiwa na Serikali hivi sasa.

MHE. DR. JOHN S. MALECELÀ: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka nitoe shukrani zangu kwa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Swalii langu la nyongeza ni kwamba; Bwawa la Mtera liko katika Wilaya ya Chamwino na Jimbo la Mtera, lakini mpaka sasa kandokando ya Mtera kuna vijiji vingi sana kutoka Mtera kuelekea Sumve na kadhalika wanauliza juu ya umeme wa kwenda vijijini unaotoka Mtera; je, Waziri haoni umuhimu na anawaambia nini Wananchi wa Mtera juu

ya upatikanaji wa umeme ambao uko kwenye Wilaya yao na vijiji vyao mpaka sasa havijafaidi umeme huo? (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa juhudhi ambazo zinafanywa na Serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme nchini. La pili, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo la Mtera kwamba, mipango tunayo, maeneo ambayo mmeyasemea hapa tunayajadili na bahati nzuri hata leo asubuhi kabla ya kipindi hiki kuanza, tulikuwa na mazungumzo na Mheshimiwa Malecela ya namna ya kufanikisha miradi hiyo. Naomba nitumie nafasi hii, kuwaahidi Wananchi wa Mtera, kwa maeneo ambayo hayako kwenye Mradi wa MCC, tutaendelea kuyafanya kazi kupitia mpango wetu wa Wakala wa Nishati Vijijini.

NAIBU SPIKA: Naona Mheshimiwa Waziri itabidi utoe kauli ya mwenendo wa umeme kwa sababu wote hawa wamesimama na mimi sitaki kuwaangalia nisije nikawaonea huruma bure. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 36

Wauguzi Wenye Lugha za Udhilishaji Katika Hospitali za Serikali

MHE. LUCY T. MAYENGA aliuliza:-

Kwa kuwa kauli ni moja ya mambo yanayoweza kumfariji au kumkatisha tamaa mgonjwa awapo katika mazingira yoyote hasa hospitalini:-

- (a) Je, Serikali inafahamu kuwepo kwa Wauguzi wenye lugha za udhalilishaji katika wodi za akina mama wanaojifungua katika Hospitali za Serikali?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kauli chafu za aina hiyo zinazotolewa na Wauguzi katika wodi za wazazi zinakomeshwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa baadhi ya watumishi wachache wa Sekta ya Afya, wakiwemo Wauguzi, wasiozingatia maadili wanapotoa huduma. Kesi nyingi zinazowahusu Wauguzi ambazo zimewasilishwa na kushughulikiwa na Baraza la Wauguzi ni zile zinazohusiana na kutokutoa huduma stahiki

kwa muda muafaka. Aidha, Serikali inatambua jitihada za watoa huduma wengi wa Sekta ya Afya hapa nchini wanaotekeleza majukumu yao kwa uadilifu na upendo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikisisitiza watumishi wote wakiwemo Wauguzi kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya kazi na kupiga vita ukiukwaji wa maadili katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini, ikiwa ni pamoja na lugha chafu za udhalilishaji wa akina mama wanaojifungua katika Hospitali za Serikali. Katika kushughulikia tatizo la mmomonyoko wa maadili katika fani ya uuguzi, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

- Somo la maadili limepewa uzito wa ziada katika mitaala ya Wauguzi na Wakunga na limewekwa kama somo la kufanyiwa mtihani wa kuhitimu katika vyuo vyote vya uuguzi ikiwa pamoja na kuwajengea uwezo Wakufunzi wa Vyuo vya Uuguzi wa kufundisha somo la maadili;

- Vjarida na vipererushi vinavyotoa ujumbe kwa umma kuhusu haki na wajibu wa mteja na muuguzi na hatua za kuchukua pale mteja atakapotendewa kinyume na inavyotakiwa vimetengenezwa na kusambazwa nchini kote;

- Mafunzo yametolewa kwa Wauguzi Wafawidhi wa Hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa ya kuwajengea uwezo wa usimamiaji, uzingatiaji wa maadili na utawala bora ili kuboresha huduma ya uuguzi nchini kote;

- Baraza la Wauguzi na Wakunga hushughulikia mapema malalamiko yaliyopokelewa kutoka kwa wateja dhidi ya Wauguzi na adhabu mbalimbali za kinidhamu zimetolewa kwa Wauguzi waliopatikana na hatia ikiwa ni pamoja na kuwafutia usajili wahusika inapobidi; na

- Vile vile ufuutiliaji wa karibu juu ya malalamiko yanayotolewa na wananchi hufanyika kupitia Idara na Mamlaka husika kwa lengo la kuweza kutatua matatizo yanayojoitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kuwa, mshikamano wa umma katika kupiga vita vitendo vya ukiukwaji wa maadili kwa watumishi wa umma ni muhimu. Hivyo basi, natoa rai kwa umma kuwa wanapoona mtaalamu wa afya anafanya kazi kinyume na maadili, taarifa itolewe sehemu husika mapema iwezekanavyo ili hatua sahihi zichukuliwe kwa wahusika.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa kumekuwa na hatua nyingi ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali ikiwemo somo la maadili kwa Wauguzi wetu, vile vile Baraza la Uuguzi kuweza kuchukua hatua mbalimbali lakini vitendo hivi vya lugha chafu na udhalilishaji kwa akinamama wanaokwenda kujifungua katika Hospitali za Serikali bado viro na vinaendelea; je, Serikali iko tayari sasa kuwa inatoa maamuzi katika Wizara hii na hasa katika sekta hii muhimu lakini vile vile kujivekea kipindi cha kufanya tathmini kujua

kama yale ambayo yanawakwaza wananchi na hasa akinamama wetu yanashughulikiwa na utekelezaji wake umefikia katika hatua gani?

(ii) Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba wapo Wauguzi ambao wamechukuliwa hatua; je, yupo tayari sasa wakati wa Bunge la Bajeti atuletee takwimu kuweza kujua hawa Wauguzi idadi yao ni wangapi na wamechukuliwa hatua gani ili walau iweze kuwa fundisho kwa wale Wauguzi ambao siyo waaminifu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, pamoja na maadili yanayofundishwa katika vyuo, bado kuna baadhi ya watoa huduma hasa Wauguzi wanaoendelea kutoa lugha chafu hasa kwa akinamama. Nakubaliana na yeche kabisu kwamba, ipo haja ya kufanya tathmini ya utekelezaji lakini nataka kusema tu mpaka sasa hivi tumeweza kufuatilia na tunayo orodha au idadi ya watu mbalimbali ambao wamefukuzwa kazi. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa kwamba ni vizuri tukatoa tathmini ili tuone ufuatilaji unakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wauguzi waliochukuliwa hatua kwamba idadi yao ni ngapi na hatua gani walizochukuliwa; mpaka sasa hivi ninayo idadi ambapo siyo lazima ningoje wakati wa Bunge, lakini kuna tuhuma ambazo utekelezaji wake zimefanyika ambazo ninaweza nikasema tu kwa ufupi na nyingine ninaweza nikampa Mheshimiwa Mbunge au na Wabunge wengine ili waweze kujua.

Hadi hivi sasa ninavyozungumza, Mkoa wa Manyara katika mwezi wa Machi tunaye mfanyakazi mmoja ambaye alichukuliwa hatua na alifutwa katika Daftari la Uguzi kwa sababu ametenda kosa.

Vile vile Dar es Salaam hadi sasa tunao watu saba ambao wametoka Manispaa ya Temeke mwezi Aprili, 2010 ambao wamepewa adhabu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kusimamishwa kazi kwa muda na wengine wamepewa maonyo makali. Pia katika Hospitali ya MOI, mwezi Februari, 2008 kuna wafanyakazi wanenambao walizembea katika kuhudumia wagonjwa nao wamepewa adhabu za makaripio makali, pamoja na maonyo makali.

Hospitali ya Morogoro, Oktoba, 2007 kuna mfanyakazi mmoja ambaye alionekana hana tuhuma akafanyiwa uchunguzi na akaonekana hana hatia.

Wapo pia wafanyakazi ambao kama mnafahamu wa Hospitali ya Mwananyamala, ambao walikuwa na tuhuma mbalimbali ambao masuala yao yameshughulikiwa na wengi wao wamechukuliwa hatua, ikiwa ni pamoja na kupewa maonyo makali na wengine wamefanyiwa uhamisho mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, sisi kama Serikali na Baraza la Wauguzi, linafanya kazi kubwa sana ya kufuatilia hili ili kuhakikisha kwamba, watu wanafanya kazi kwa maadili kama ambavyo inahitajika wafanye.

Na. 37

Uhaba wa Madaktari wa Fani Mbalimbali

MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE (K.n.y. MHE. MCH. DR. GERTRUDE P. RWAKATARE) aliuliza:-

Kwa kuwa uhaba wa Madaktari na Wauguzi ni kero kubwa na kwamba kuna fani nyingine hazina Madaktari kabisa; na kwa kuwa hata Madaktari wachache waliopo wanakaribia kustaafu na hakuna matumaini ya kupata wengine kama vile *Neuro-Surgery*, Mama Cheza, Madaktari wa Macho au wa Ganzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Madaktari wa fani hizo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla sijajibu swalii la Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kwanza, naomba kufanya marekebisho madogo kwenye swalii la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: Jina rasmi la wataalam ambao wametajwa kama Mama Cheza sasa hivi tunaomba tuwaite Wazoeza Viungo.

Baada ya marekebisho hayo sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, upo uhaba mkubwa wa wataalam katika Sekta ya Afya katika fani zote na ngazi zote za kutolea huduma nchini. Wastani wa upungufu wa wataalam wa afya nchini kwa ujumla ni takriban asilimia 62. Zipo fani ambazo uhaba huu wa wataalam ni mkubwa zaidi ikilinganishwa na fani nyingine kama vile Madaktari Bingwa wa Mifupa na Wazoeza Viungo. Aidha, zipo sababu mbalimbali zinazosababisha uhaba huu, mojawapo ya sababu kubwa ni kuwa na idadi ndogo ya wahitimu katika fani mbalimbali kutoka vyuo vya afya ndani na nje ya nchi. Aidha, baadhi ya fani hazivutii wahitimu kwenda kuchukua kozi za uzamili, pia zipo fani ambazo mafunzo yake yanapatikana nje ya nchi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka ya hivi karibuni, Wizara kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu vya hapa nchini, imekuwa na mkakati wa kuanzisha mafunzo ya fani hizi adimu hapa nchini, kama vile upasuaji wa mishipa ya fahamu (*neurosurgery*), upasuaji wa mifupo, utaalalm wa magonjwa ya figo (*nephrology*), magonjwa ya moyo, wazoeza viungo (*physiotherapist*), huduma kwa wagonjwa mahututi (*critical care*) na nyinginez.

Kipaumbele kimewekwa katika kusomesha wataalam katika fani hizi adimu nje ya nchi ili hatimaye kujenga uwezo wa kutoa huduma na kufundisha wataalam hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa mafunzo katika fani hizi adimu, kunakwenda sanjari na ongezeko la wataalam wa afya wanaojiunga na mafunzo ya uzamili katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2008, kumekuwapo na ongezeko la wataalam wa afya waliogharimiwa na Wizara kujiunga na mafunzo ya uzamili kutoka wastani wa wanafunzi 60 kwa mwaka katika miaka ya nyuma kufikia 168. Mwaka huu wa masomo 2009/2010, Wizara inawagharimia wanafunzi 254 waliojiunga na mafunzo ya uzamili ndani na nje ya anchi. Idadi hii inategemewa kuongezeka mwaka hadi mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Utaratibu huu utatuwezesha kuwa na idadi kubwa zaidi ya Madaktari Bingwa katika fani zote kwa uwiano katika Hospitali za Kitaifa na za Mikoa, ambazo kwa utaratibu uliopo zinakuwa Hospitali za Rufaa.

Na. 38

Kugawa Mashamba ya Mkonge Kwa Wananchi wa Korogwe

MHE. ENG. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa muda mrefu iliahidi kumega ardhi katika mashamba ya Mkonge na kuwapatia wananchi wanaozunguka mashamba hayo Jimbo la Korogwe Vijijini kwa ajili ya shughuli zao za kimaendeleo:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa ili kuepuka migogoro ya mara kwa mara kati ya wamiliki wa mashamba hayo na wananchi?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kutekeleza ahadi ya kumega Ardhi kutoka katika mashamba ya Mkonge Wilayani Korogwe kwa kutoa ardhi yenyewe ukubwa wa hekta 7,305 na kuwagawia wananchi wanaozunguka mashamba, ambapo ugawaji wa ardhi hiyo ulifanywa kati ya mwaka 2000 na 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kugawa ardhi iliyokuwa chini ya Mashamba ya Mkonge ultokana na maombi ya wananchi kuititia Halmashauri ya Wilaya yao, ambayo ilijadiliana na wamiliki wa mashamba hayo na wakakubaliana kwamba, sehemu ya mashamba hayo yamegwe na kuwagawia wananchi wasio na ardhi. Baada ya makubaliano yaliyofikiwa, Serikali ya Mikoa Tanga na ya Wilaya ya Korogwe, waliwasilisha Wizarani kwangu makubaliano hayo ya kumega ardhi hiyo ili kuwagawia wananchi.

Mashamba yaliyopendekezwa na kukubaliwa kumegwa ni Magunga, Gomba/Mwenga, Toronto, Hale/Mruazi, Mwelya, Mkumbara na Usambara, yote kwa pamoja yakiwa na ukubwa wa hekta 33,913. Kati ya ardhi hiyo, eneo la ardhi yenye ukubwa wa hekta 7,305 lilimegwa na kugawiwa wananchi katika vijiji 26 vinavyozunguka mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la watu katika maeneo hayo, inawezekana ardhi hiyo iliyogawiwa hajatosheleza mahitaji na pia inawezekana kuna mashamba ambayo wamiliki wake hawayalimi yote. Kama hivyo ndivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe Vijijini inashauriwa ichukue hatua kama zile za awali na Wizara yangu inaahidi kutoa ushirikiano.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na pamoja na kutambua mchango mkubwa unaotolewa na Katani Ltd kwa kugawa baadhi ya sehemu zake kwa ajili ya huduma za jamii, naomba kuuliza swali moja la ziada.

Kwa kuwa wananchi wengi wanaoishi pembezoni mwa mashamba hayo kwa muda mrefu walikuwa wanayatumia kwa ajili ya kilimo cha chakula lakini inapotekea kwamba wenyе mashamba hayo hawayahitaji hujitokeza watu kutoka nje na kupewa mashamba hayo na kuachwa hawa wenyeji waliokuwa wanayatumia; je, ni juhudи gani ambazo zinaweza zikakomesha biashara hii badala ya kupewa wageni wapewe wenyeji ambaо walikuwa wanayatumia kwa takriban miaka 10 hadi 30?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe Vijijini iingilie kati kwa sababu haiwezekani mahali ambapo kuna uhaba wa ardhi ile ardhi ya ziada ambayo wenyе mashamba wanayo wanawapa watu kutoka nje ya Korogwe halafu inawaacha wale watu wa Korogwe wenyе shida; siyo sawa sawa.

Kwa hiyo, nashauri Halmashauri ya Korogwe iingilie kati ihakikishe kwamba, yale mashamba ambayo kuna ardhi ya ziada, wenyе mashamba yale kwanza watoe kipaumbele kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo badala ya kutoa kipaumbele kwa watu wanaotoka nje. Pili, kama kuna mashamba ambayo yametelekezwa kwa wamiliki wa awali hawayalimi na hata kodi ya ardhi hawalipi.

Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe iorodheshe ili yaingie katika utaratibu wa wale kufutiwa hati zao ili hatimaye mashamba yale wagawiwe wananchi ambaо wana matatizo ya ardhi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha sasa ni matangazo. Kwa bahati nzuri sana leo tumefikiwa na Mabalozi wa Jumuiya ya Ulaya ambaо wamekuja kututembelea hapa Bungeni. Mabalozi wanaongozwa na Balozi Kiongozi wa EU, ambaye ni Mheshimiwa Balozi Tim Clarke. Tunaye Mheshimiwa Balozi Bjarne Sorensen kutoka Denmark; Mheshimiwa Balozi Dr. Ad Koekkoek kutoka

Netherlands; Mheshimiwa Balozi Staffan Herrstrom kutoka Sweden; na Balozi wa Ireland, Mheshimiwa Anne Barrington.

Tunao Maafisa waliofuatana nao, yupo Bwana Rene Benesi, Ndugu Pia Weranda, Ndugu Tumsifu Mmari na Bi. Agnes Hant.

I am sure I didn't pronounce some of your names correctly but you need some exercise to pronounce some of these names. You are most welcome to our Parliament, it is not your first time but you are welcome to Dodoma in particular to our House. (Makofit)

Wageni wengine ni wa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, hao ni wanafunzi wa darasa la nne, St. Mary's International School; wanaitwa Baraka Alex na dada yake Salvina Charles.

Tuna wageni 18 wa Mheshimiwa Mussa Zungu, hawa ni Kikundi cha Kiwakai toka Jimbo la Ilala, wakiongozwa na Mwenyekiti wao anaitwa Situ Mwasa. Wote walipo wasimame. Kumbe kikundi chenyewe ni cha akinamama.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mbunge wa Ulanga Magharibi, Mrs Francisca Matanda, anatoka Itete. Tuna mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Katibu wa CCM Wilaya, ambaye ni Mberito Magova.

Tuna Mameneja wa NMB Dodoma, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge ambao ni Meneja wa Kanda ya Kati, Mrs Lilian Mwinula; na tuna Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kule kwetu nadhani, Mrs Makirie.

Tumefurahi sana Mameneja kuwepo hapa na ninyi, tunapata nguvu sana maana wakiwezesha wanaweza. Tuna wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Biashara Dodoma, hawa ni majirani zetu hapa karibuni sana na msome vizuri.

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Lucas Selelii, *actually*, ni familia yake yote ikiongozwa na mke wake, Rose Selelii na watoto na wajukuu wote. Ahsante sana. Hapa kuna watoto na wajukuu, kwa hiyo, tumefurahi sana mmekuja. (*Makofit*)

Tuna matangazo ya kazi; kwanza kabisa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Zitto Kabwe, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo tarehe 15 saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati kwenye Ukumbi Namba 231, Jengo la Utawala. Leo hii pia kuna semina ya MKUKUTA kwenye Ukumbi wa Msekwa, sasa semina ya MKUKUTA ni muhimu kujua tulifanya nini kipindi kilichokwisha na sasa tunaingia awamu ya pili, kwa hiyo, mtaamua wenyewe.

Jana nilitangaza kwamba, Kamati ya Uongozi ya Bunge kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu, saa tano hii watakuwa na Kikao kwenye Ukumbi wa Spika. Halafu Wabunge wote kutakuwa na Semina hii ya MKUKUTA saa saba, katika Ukumbi wa Msekwa. Kamati ya Uongozi ya CCM itakutana saa mbili usiku baada ya kuahirisha kikao hiki. Tunaendelea na kazi za leo Katibu.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010 (*The Mining Bill, 2010*).

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2010*).

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni
Mara ya Kwanza)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Miswada mnakumbuka imeletwa kwetu kwa *Certificate of Urgency*, kwa hiyo, nakala zake ziko kwenye *pigeon halls*. Kamati zinazohusika zitaelekezwa wapi pa kufanya.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010
(*The Livestock Identification, Registration
and Traceability Bill, 2010*)**

**Muswada wa Sheria ya Malisho na Vyakula vya Mifugo wa Mwaka 2010 (*The
Grazing Land and Animal Feed
Resources Bill, 2010*)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, jana niliwataja wafuatao kwamba wangechangia; yupo Mheshimiwa Christopher Ole-Sendecka, Mheshimiwa Tom Ntimizi, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Nsanzugwanko, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Zaynab Vulu na wengine tutawataja kadiri tunavyoendelea.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii ya mwanzo, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Hoja ya Miswada yote miwili muhimu katika mustakabali mzima wa wafugaji wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu, baada ya kuhitimishwa kwa kesi iliyonichukua mwaka mmoja na miezi miwili, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kushinda kesi hiyo na sasa nipo huru baada ya uamuvi wa Mahakama wa Hakimu Mkazi Mjini Arusha. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Simanjiro, kwanza, kwa kuelewa chanzo, dhamira ya kesi yenye na zaidi dhamira ya wadau waliowazi na waliokuwa nyuma ya pazia katika kesi hiyo na kunipa ushirikiano kuanzia siku ya kwanza mpaka siku ya mwisho. Nataka pia kuwashukuru Wananchi wa Monduli, ambapo tangu siku ya kwanza nilipopatwa na mkasa huo uliotengenezwa walikuwa wa kwanza kunidhamini na walijaa pale Kituo cha Polisi na hatimaye kunidhamini na nikapata fursa ya kurudi kwa watoto wangu na wapiga kura wangu na kuanza mchakato wa kesi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru Mawakili wangu wote watano; Mheshimiwa Wakili Neema, Wakili Kamara, Wakili Ngaro, Wakili Mwaluko na Wakili Akida, wote wakiwa wasomi ambao wamenitetea katika kesi hiyo. Nawashukuru pia Wabunge wenzangu Wanasheria ambao wamenipa ushauri tangu wakati wa misukosuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nirudi kwenye Muswada ulioko mbele yetu. Muswada tunaoujadili au Miswada yote miwili tunayojadili nina hakika ikirekebishwa na ikisahihishwa vizuri, inaweza kuwa na dhamira njema na ikasaidia wafugaji huko tuendako. Kutokana na upungufu ulioko katika Miswada yote miwili, unaalika busara ya hali ya juu ya Bunge lako Tukufu; busara ya mshikamano na busara ya kusikiliza ufahamu wa wale wenye uzoefu katika Sekta ya Mifugo ili kwa pamoja tutakapopitisha Miswada hii miwili, iweze kuwa na maslahi kwa wafugaji wa Tanzania.

Upungufu huu unaalika busara ya hali juu ya Waziri anayewasilisha hoja hii na Serikali kwa ujumla, kuona kwamba kurejeshwa kwa Muswada katika Kamati ili iweze kusahihishwa na kufanyiwa marekebisho, haitakuwa kitendo cha kujidhalilisha wala kujifedhehesha, bali kitakuwa ni kitendo chema kabisa cha kwenda kuitendea haki Miswada hii ili baadae Bunge lako litakapopitisha, liwe limeshafanya masahihisho muhimu kwa maslahi ya wafugaji wa nchi yetu.

Nina hakika Waziri na Naibu Waziri ambao ni watoto wa wafugaji ni Makada wa Chama cha Mapinduzi, watakubaliana nami kwa mujibu wa Ibara ya Tano, kifungu cha 58 cha Mwongozo wa CCM wa Mwaka 1981 inayosema kujikosoa na kukosoana ni silaha ya mapinduzi; kwa kufanya hivyo na kusema huko mbele inakosema kukiri upungufu si dalili ya kushindwa bali ni ishara ya kujiimarisha. Wao ni waumini wazuri sana wa chama chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninawashawishi kwamba, pale hitaji litakapokuwepo la kurejeshwa kwa hoja hii kufanyiwa masahihisho zaidi, waone ni kwa nia njema na si kwa nia ya kutaka kuifedhehesha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niseme Miswada tunayojadili sasa lazima tuijulize inakusudia kuwalenga akina nani? Bila shaka wote tunakubaliana inawalenga wafugaji na hasa ambao ninyi mnawaita wachungaji ambao kwa hakika hawana malisho, hawana maji ya uhakika, hawana majosho kwa ajili ya mifugo yao, ardhi yao ya kulishia imevamiwa kwa ajili ya matumizi mengine halali ya ardhi ambayo ni wanyamapor, migodi katika maeneo mengine na maeneo mengine pia yamechukuliwa na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wa nchi yetu wamekuwa ni wakimbizi katika nchi yao kutokana na maeneo yao kuchukuliwa na shughuli hizo nyingine nilizozitaja. Nenda Hanang leo kwenye mashamba ya Basuto, nenda Simanjiro katika eneo lililochukuliwa na Tarangire National Park, nenda Serengeti iliyokuwa ni malisho ya wafugaji, nenda Ngorongoro ambayo eneo lote ni hifadhi lakini eneo lote la Polpet, eneo tengefu la Loliondo lote nalo linashughulikiwa zaidi na masuala ya wanyamapor ambao wanapewa kipaumbele zaidi kuliko wafugaji wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda Magharibi mwa Wilaya ya Simanjiro ambako kumeanzishwa Mkungonero Game Reserve, ambayo bado masahihisho hayajafanyika ya mipaka ya Mkungunero Game Reserve na Wilaya ya Kiteto na Mkungunero Game Reserve na Wilaya ya Simanjiro, ambayo Serikali iliahidi kuyafanya kwenye mipaka hiyo ili kuacha eneo lililokuwa limevamiwa na eneo hilo la Mkungunero kubaki katika vijiji vinavyohusika vya Wilaya ya Simanjiro na Wilaya ya Kiteto. Haya ni maeneo ya malisho ya mifugo ambayo yalikuwa yamevamiwa. Lazima tuijulize hivi tunapokwenda kuisajili mifugo hii kwa mujibu wa Sheria ambayo Muswada wake umeletwa mbele yetu, tunakwenda kusajili kwa faida ya nani maana tumeweka Sheria iliyopitishwa miaka nenda rudi ya kusajili vizazi na vifo ambapo tulitakiwa kusajili watoto wanaozaliwa na pia kutoa taarifa ya wale wanaofariki.

Ninataka kujiuliza na Bunge lako lijiulize; hivi hadi leo Watanzania wangapi wamesajiliwa na wana vyeti vya kuzaliwa? Huko Simanjiro pengine hawafiki hata asilimia tano au kumi na nina hakika maeneo mengine ni mabaya zaidi na mengine pengine ni ahueni kidogo. Bado tunajiuliza tunapokwenda kusajili mifugo tunasajili mifugo itambuliwe na nani maana mimi mwenyewe ninajua alama za mifugo yangu na za ukoo wangu na Wamasai wote wanajua alama walizoziweka na utambuzi wa kumtambua mnyama yule hata usipompiga chapa ninajua ndama huyu amezaliwa na ng'ombe yupi na ninajua ukoo mzima wa ng'ombe huyo? Sasa unapokwenda kusema tutafute usajili maana yake lazima utafute *tags* ambazo zitakuwa na namba, bila shaka hapa kuna mtu mmoja nyuma anatakiwa kupewa *tender* ya *tags* hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ng'ombe milioni 19 kwa takwimu za Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvubi, ng'ombe hawa ukiwachaji kila *tag* shilingi 500 au 1000, unazungumzia shilingi bilioni 19. Ukitsema tusajili ng'ombe hawa kwa siku saba, unatengeneza mradi wa mtu kupata shilingi bilioni 19, ambapo msingi wake wala

hatuuoni. Nataka nimsadie sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana; mifugo yetu si kwamba haijapata soko kwa sababu haina *tags* au haijasajiliwa, hapana; ni kwa sababu *ranches* za taifa ambazo zinazalisha madume bora ya mbegu kila siku mnawapeleka madume hao buchani, hamjawachukua wale madume bora wa mbegu kwa ajili ya nyama na kugawanya hata kwa wagogo waliozunguka Kongwa Ranch ili wapate ng'ombe wazuri wenye manufaa.

Hamjachukua hawa madume wa nyama na kuwagawia wafugaji wanaozunguka ili kuambukiza huo ufugaji bora. Hamjachukua ng'ombe bora wa maziwa na kuwasaidia wafugaji hao wapate maziwa zaidi. Leo mnakimbilia kwenye Sheria na kuchukua mifano ya Botswana ambao watu waliwekeza kwa kiasi kikubwa? Nataka niwahakikishieni leo lete ng'ombe wa Boran au wa Saiwal pale Simanjiro; huna maji, ng'ombe wale wa kienyeji wa Kimasai wanakaa siku tatu, nne, hawajanywa maji ndiyo wanawenza kuhimili kwa kiangazi. Nenda leo Kajado Kenya kaangalie wale Boranasai wamebaki wangapi kwa msimu huu; hawana. Wanarusi ng'ombe wetu hawa wa kienyeji wanaowenza kuhimili ukame ule ndiyo wanaanza.

Nenda Longido kwa Mheshimiwa Lekule Laizer kama ng'ombe wake wasingekuja katika Jimbo la Simanjiro *along* Tarangire National Park, leo Longido usingekuta alama ya ng'ombe hata mmoja. Leo mnaweka Sheria inayowaweka wafugaji hawa wasihame kutoka katika sehemu moja kwenda sehemu nyingine, maana yake si kwamba Sheria hii inakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayomruhusu Mtanzania kwenda mahali anapotaka bali mmeamua kuweka mazingira ambayo yataabweka wafugaji hawa katika mazingira ambayo mifugo itakufa na wao watakufa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishieni, tumewaona Viongozi Wakubwa wa Serikali wakipanga bajeti ya dharura ya kuweza kuwasaidia wafugaji kupata mifugo ambayo kwa hakika hali yao ni mbaya. Nenda Longido, unakuta mtu alikuwa ana ng'ombe 1,000 leo hana hata mmoja, njoo baadhi ya maeneo ya Simanjiro utakuta hali ni hiyo hiyo. Nenda Monduli utakuta hali ni hiyo hiyo. Nataka niiambie Serikali kwamba, kwa kuwa hali hiyo imeonekana baada ya Serikali kushindwa kutoa fidia ya kuwasaidia hawa kama ilivyokuwa ikifanya juzi katika baadhi ya maeneo ya wakulima wa pamba kuhakikisha kwamba, athari za mabadiliko ya uchumi duniani isiwaathiri kwa kiasi kikubwa. Bado rai yangu kwa Serikali, itenye fedha kwa ajili ya wafugaji ambao wameishiwa mifugo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika vifungu ambavyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri aviondoe na bahati nzuri hata Mwanasheria Mkuu mwenyewe ni mchunga ng'ombe, anajua mazingira hayo. Suala la usajili kwenye sehemu ile ya sita naomba lifutwe kwa asilimia mia moja. Suala lingine ambalo naomba libadilishwe ni sehemu ya 20, ambayo inagusa mamlaka ya mkaguzi na upunguzaji mifugo. Nimesema na mwenzangu Mheshimiwa Simbachawene jana ameeleza; huu ni utaifishaji katika karne hii nyingine ambako tuna *Bill of Rights* katika Katiba ya Nchi yetu. Ondoa na kiumbe hicho kinachoitwa Mkaguzi asiwepo kabisa hapo aende akafanye

kazi nyingine; akakague nyama, aache kutupunguzia mifugo yetu, tutapunguza wenyewe kwa kadiri mahitaji yatakavyokuwa.

Suala la utambuzi wa kimila; nataka niwahakikishieni mtawafunga wafugaji wote, kwa sababu hatuko radhi kuacha mifugo yetu kuweka alama ya ukoo inayotambulisha ukoo huu na ukoo mwingine, inayotofautisha kati ya Familia ya Sendeka na Familia ya Lekule Laizer; ni lazima alama hizi ziwepo, mnachoweza kusema ni kuangalia athari katika ngozi, lakini ngozi yenyewe mnaipeleka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya ngozi vyote mliviuba leo ni magodown; nenda Morogoro, nenda Mwanza, nenda Moshi, viwanda vile viko wapi mbona Mheshimiwa hasemi? Viwanda vile vimekuwa magodown na waliochukua magodown haya ni wakubwa na wakubwa wenyewe wamo humu humu ndani ya Bunge hamuwezi kuwanyoshea kidole halafu mnatuambia ngozi; ngozi ya kumpelekeaa nani; kupeleka Kenya? Hebu mfike mahali muelezane ukweli huko mliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utambuzi mnaozungumza na chapa, mnataka kutengeneza *tender* na hao hao tena mlete *tags* za kuweka kwenye masikio ili mpate hiyo shilingi bilioni 19 ya ng'ombe kabla ya mbuzi na kuku. Mtatafuta hata *tags* ya kuku sasa baada ya hapo sijui mtamfunga wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze wazi, shida ya wafugaji ni maji, majosho na malisho yao yalindwe. Sheria inayokusudia kulinda hayo tupo pamoja nayo. Bado naomba sana Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria Mkuu wakubali hoja hii irudi kwenye Kamati tukasahihishe, tukileta hapa tunaipigia makofi imepita. Kwa hali hiyo, siwezi kuunga mkono hoja hizi mbili, kama kungelikuwa na namna nyingine ya kueleza dhamira yangu ya kuchukia Miswada hii miwili, ningeweza kuonesha zaidi. Kwa kuwa kitendo cha kutembea kwenda nje ya Bunge hili si cha kistaarabu, Mheshimiwa Waziri aone kuirudisha hoja hii kwenye Kamati siyo kitendo cha kujifedhehesha, tuirudishe huko tusije tukalazimisha masahihisho ya hapa na pale halafu keshokutwa tukarudi kwenye kusahihisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja hizi mpaka hapo zitakaporudi kufanyiwa masahihisho ya kutosha. (*Makofi*)

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Miswada hii miwili. Nami natoka katika kundi la wafugaji, ingawa si wakubwa kiasi hicho kama Wasukuma na Wamasai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja hii na mimi pia nirudi Jimboni kwangu, niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Igalula, kwa jinsi walivyokuwa pamoja nami baada ya matatizo niliyokuwa nimeyapata ya kufanyiwa operesheni ya mguu; wamenifariji sana na wameendelea kunifariji na mpaka sasa tunafanya kazi bega kwa bega na kazi ambayo inaendelea; *aluta continua* na wako pamoja na mimi kwa hali na mali. Wala sina wasiwasi kipindi hiki kinachokuja wako na mimi. Unajua kitanda ulaliacho unakijua kunguni wake, kwa hiyo, sina wasiwasi na naomba waendelee kuniunga mkono ili tufikie azma ya kazi ambayo tunaifanya sote kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja zote mbili lakini mambo kadhaa naomba yazingatiwe. Wafugaji wana mifugo mingi, imekuwa ni jadi ningeomba tu wenzangu tusikubali kuendelea na jadi, tujaribu mabadiliko kwa manufaa ya mifugo yetu na pia kwa manufaa ya Taifa. Tuna mila nyingi sana za kikabila ambazo tumekuwa nazo lakini kila siku tunajaribu kuzibadilisha. Kwa mfano, ukeketaji ilikuwa ni mila ya kawaida lakini Serikali imeona hapana hebu tujaribu kuelimisha na tuiondoe mila hii. Kwa hiyo, tukisema tung'ang'anie mila zilezile za kuweka alama kwenye mifugo yetu ni kweli imesaidia sana, lakini hebu tubadilike tutafute mbadala kusudi hii mifugo iwe na afya njema na iweze kutambulika vizuri kwa manufaa yetu wenyewe wafugaji na manufaa ya Taifa. Kwa hiyo, ndugu zangu nawasihi sana tukubali marekebisho. Wizara na Viongozi nina hakika ni wasikivu, waone mabadiliko gani ni muhimu ili hawa ng'ombe wapate manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu kuna mfugaji mmoja anaitwa Maguta, ana ng'ombe 4,000 wakati wa kutoka anasimamia na wachungaji; ndama si chini ya 400 anawafahamu kwa sauti; akipiga mluzi aina fulani ndama wanatoka, akipiga mluzi fulani majike yanatoka; lakini anapata kazi kwa muda wa saa mbili hadi tatu kusimamia ili waende kwenye machunga. Ukimwambia hebu jaribu kupunguza ili maisha yawe bora na ujenge nyumba bora, anakwambia kwamba, nina wasichana wengi wanaolewa na kila anayolewa ninapata si chini ya mifugo 20 hadi 30, kwa hiyo inazidi kuongezeka na siwezi kuacha kuzaa kwa sababu ni mila na destui zetu kuwaozesha wasichana kwa ng'ombe.

Amejaribu kushawishiwa kwamba, nyumba zake ziwe nzuri lakini amekuwa ni mgumu; elimu inahitajika. Tuwasaidie badala ya kuwapelekea *inspectors* wa kuhesabu, tuanze kuwaelemisha wao kwanza; elimu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa Naibu Waziri wa Afya, mambo ya ukeketaji, nilikuwa naenda katika mahospitali, katika mikusanyiko, jamani kuna suala hili linakuja na ukeketaji siyo mzuri. Kidogo wakaanza kuwa na uelekeo hata wa kukubali kwamba tusitishe kukeketa. Lakini, tukienda tu moja kwa moja na hii sheria kwamba imepitishwa, sasa asiyekubali kuhesabiwa mifugo yake atapelekwa mahakamani, kuna Inspekte atafanya hivi; kwa kweli tutapata *hostility* kubwa sana kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hawakushirikishwa vya kutosha. Walishirikishwa wafugaji wale wa mijini wanaofuga mifugo ndani ya majumba. Lakini, wafugaji hasa ambao wanachunga eneo kwa eneo, nafikiri uwakilishi wao ulikuwa mdogo kabisa katika kujadili hoja hii. Ningeomba pia, kama siyo kurudisha huu Muswada, lakini jaribu pia kabla ya Kanuni kutengenezwa twende katika maeneo ambayo wafugaji wako wengi wafanyiwe semina, wapewe maelekezo, waelekezwe mambo mazuri ambayo yataleta faida. Kama tunavyojumuisha kuhusu mambo ya maji, tunawaambia kwamba changia ili upate maji, aidha malambo, mabwawa au visima. Wananchi wakielimishwa, wakilifahamu, kwa kweli hawana matatizo. Tatizo letu tunavamia. Naomba suala hili la wafugaji tusilivamie. Twendeni kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu wafugaji wengi wametoka maeneo ya ndugu zangu. Karibu 70% ya wakazi wa Jimbo la Igalula ni wafugaji wazuri sana na wana mifugo mingi. Lakini huwezi kumwambia tu Msukuma punguza mifugo ili ujenge nyumba nzuri. Kwanza, atakwambia kwamba nitazame kama nyumba nzuri itakuwa na faida katika familia. Kwa hiyo, ukijenga nyumba nzuri kuna wachawi, nyumba nzuri mifugo haitapona. Kwa hiyo, kuna maadili ambayo wanayo kichwani, si rahisi tu leo kumwambia ghafla kwamba punguza mifugo kwa manufaa yako, elimu inahitajika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha kiangazi kinakuja, tutoe watalaan waende katika maeneo haya. Watutumie sisi Wabunge ambao bado tupo, tuendelee kuzungumza na wao, jamani faida zake ni hizi na hizi. Ukimwambia mara ya kwanza, mara ya pili, mara ya tatu, ataanza kuingiza neno hilo akilini na kulifanya kazi. Lakini, kutumia ma-Inspeksa kwenda kuhesabu, sijui kutumia Mjumbe wa Nyumba Kumi, halafu Mjumbe wa Nyumba Kumi mwenyewe anaweza kuwa si mfugaji, kwa hiyo ule uchungu wa ufugaji hana, yeye atatimiza sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, tufanye elimu ni kitu cha msingi kabisa katika kuhakikisha sheria hii inafanya kazi. La sivyo, kama walivyosema wenzangu, tutapeleka sheria ambazo hazifanyi kazi. Kwa hiyo, inakuwa kwamba, tunakula posho ya kufanya maneno badala ya kutafsiri hayo maneno tunayozungumza hapa ndani ya Bunge yakawa na faida kwa wananchi wetu ambao tunawawakilisha. Naomba sana hili lifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna mifugo kutoka nchi jirani. Kama mnakumbuka miezi miwili iliyopita watu wa Bukoba au Kigoma, wamelalamika kwamba mifugo inayotoka jirani inapitishwa na viongozi wetu wa Serikali. Kama siyo Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji au Mwenyekiti wa Kijiji, wanafanya mazungumzo, anapewa pengine shilingi 10,000/=, anawapitisha katika njia za panya. Kwa hiyo na kule nako kutafutwe udhibiti mzuri. Serikali iende kule, mkiwaachia tu hawa uongozi peke yao, kwanza viongozi wengine wana hekima lakini elimu ya kutafsiri mambo inakuwa ni haba kwao, lakini wanakuwa na hekima nzuri, ni watu wazima wenye busara zao, lakini njaa pia ipo, akipewa Dola 100 anaona kwamba atajijua kule atakakofikia na mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba sana, tuanze kwanza usalama wa mipaka yetu, tuone jinsi gani hawa ng'ombe wanaotoka nchi za nje wanatembea kutoka kule mpaka kufika kilomita 1000, wamepita pitaje katika njia hizi? Kuna nini hapo? Lazima kuna ushirikiano, siyo wafugaji tu walaumiwe kwamba wanakubali mifugo inakuja. Lakini kuna suala la mifugo ya Burundi yenye mapembe marefu, wengi wanawachukua ili wawazalishe, wapate ile mbegu. Mifugo hii ya kutoka Burundi imeenea hasa katika maeneo yetu. Mfugaji anasema kwamba afadhali na mimi niwe na *style* nyingine ya mifugo. Sasa yote haya yanataka elimu. Naomba sana kwa kweli, tufanye kazi ya elimu zaidi kwa wananchi na viongozi wetu ambao wamo katika maeneo hayo ya wafugaji waelewe sheria hii kabla ya utekelezaji. La sivyo, mtapata *hostility* kubwa sana na migongano ambayo italeta mauaji kama ambayo yapo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za mifugo zipo, lakini wachache wanaotumia. Imeonekana wakati fulani miaka miwili imepita, walikuwa wanachanja ng'ombe, baada ya muda wanakufa wengi kuliko walivyotegemea. Kumbe kulikuwa na tatizo, muda mrefu wamewficha bila kuwachanja. Sasa wanapowachanja kwa mara ya kwanza, *reaction* yake wanakufa, wengi wakawa wanaficha mifugo yao. Ana mifugo 1000, anakwambia ana mifugo 400, wengine anawaficha kwa sababu aliona *effect* ya kuchanja wamekufa ghafla kwa mpigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata kuhesabu kutakuwa na matatizo pia kuhakikisha kwamba kweli ng'ombe wote wamehesabiwa. Kwa sababu kwanza anaanza kufanya *conspiracy* na huyo kiongozi wa pale, wengine wamekwenda machungani, wengine wamekwenda Lubaga (Lubaga nafikiri wafugaji wanafahamu). Wakati wa kiangazi wanatolewa pale. Kwa vyovoyote vile huna namna, hata ukisema hapa wasitoke, pamekuwa pakame kabisa. Waliondokaje watu wa Shinyanga kuja katika maeneo yetu? Ni kwa sababu ardhi ilikuwa imekwishakomaa, imedumaa, haina tena mazao ya kuweza kutoka wakati wa masika ili mifugo iweze kupata chakula. Kwa hiyo, wanahama, hata katika maeneo ambayo wafugaji sasa hivi wapo, wakati wa kiangazi inakuwa ni kukavu kweli kweli inabidi awahamishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huwezi kusema kwamba basi wafe kwa sababu na Serikali inategemea mifugo ili tupate *revenue* kutoka kwao, halafu na lishe pia. Kutwa sisi viongozi wa kula nyama, asubuhi, jioni, usiku, je, hiyo nyama inatoka wapi? Siyo kama hawa wafugaji ambao wanapata tabu katika kulisha, wanapata tabu katika kuwatunza. Kwa hiyo, naomba sana pia kuwe na dawa za uhakika, wanasema siku hizi Serikali haiuzi, wakienda kununua dawa katika maduka ya kawaida inakuwa ghali sana. Mfugaji hakai na pesa nyingi, pesa zake ni mifugo. Sasa tukiangalia kwamba tuwasogezee dawa hizi kwa bei nafuu na tuone tutakavyo-*regulate*, wanaweza kuishi vizuri na mkapata mahesabu. Lakini bado nina wasiwasi hesabu za mifugo hii, anaozesha leo binti, anapata mifugo 26, baada ya miezi miwili, kaozesha binti mwengine, kapata pengine mifugo 30. Sasa kumwambia kwamba kila siku aweke *data* kwamba leo ana mifugo 20, kesho 1000, kesho wangapi na kufa vile vile kutokana na chanjo ambayo nimeizungumza hapa itakuwa vigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hebu naomba tuangalie mazingira yote kwa pamoja, maeneo wanayokaa wafugaji, kuna sehemu zingine kweli kuna majani ambayo karibu mwaka mzima au robo tatu ya mwaka. Lakini kuna sehemu zingine miezi mitatu au minne katika kipindi cha mwaka yamekauka. Huyu mfugaji hawesi kusema kwamba abaki mifugo yake ife kwa sababu haendi. Lakini kwa sababu tunasema kwamba Mtanzania anaweza kwenda mahali popote mradi asivunje sheria, basi anakwenda anaingia kwenye maeneo ya *reserve*, kule wanapigwa risasi. Tunawatendea mambo ambayo kwa kweli hawaridhiki. Ikiwa wananchi wenyewe hawaandikishwi wote, sheria ya kuandikisha binadam tofauti na mifugo, tuikubali hii tujaribu, angalau tuone matokeo yake. Pia tusisitize kwamba tufuatilie, baada ya sheria kurekebishwa au kuletwa, basi tufuatilie. Wafugaji kwa kweli hawatapata faida ya sheria hii kama elimu hawana, halafu

pia hawapewi heshima yao kwa kuzungumza nao vizuri badala ya kuwakemea, wewe kwa nini una mifugo 1000? Wewe kwa nini umekaa hapa? Namna hiyo, haifai....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda
wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, naona umesema sana.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naendelea kuunga mkono hoja, lakini marekebiso yawepo. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ROSEMARY R. KIRIGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwa mchangiaji kwenye Miswada hii miwili muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema na kuweza kuhudhuria Bunge letu Tukufu. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wangu wa Mara na wananchi kwa ujumla kwa namna wanavyoniusa mkono na kunisaidia katika utendaji wangu wa kazi wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumshukuru Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii na Kamati zilizohusika katika kujadili Miswada hii miwili kwa namna walivyojitali kwa kweli kujadili kwa kina. Upo upungufu ambao tunauona, lakini si mwingi sana, kwa kweli wamejitali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikushukuru wewe binafsi kwa kitendo chako cha jana. Ililetwa hapa hoja kwamba tusitishe kujadili Miswada hii. Kwa kweli nakushukuru sana ultumia sana busara, kwa sababu bila sisi Wabunge kujadili, yale makosa yaliyopo kwenye hii Miswada hayataweza kuonekana. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa busara ulioitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba, sekta hii ya mifugo ni sekta ambayo imekuwa ikishindwa kukua siku hadi siku, lakini sababu tunazona kwamba wafugaji wengi wamekuwa wakifuga kijadi na hawataki kutoka kule kwenye kufuga kijadi na kwenda katika kufuga kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawezaje kufuga kisasa? Kufuga kisasa ndio kama inavyosema Miswada hii yote miwili kwamba lazima kuwe na *Identification, Registration na Specialization* ya mifugo yetu. Bila kufanya *identification* kutakuwa hakuna ule ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyoangalia Miswada hii nimeona itatupeleka kwenye ufugaji wa kisasa hasa kwa kupata takwimu. Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa tunashindwa kupata takwimu, bado sekta hii ya mifugo inatumia takwimu ambazo ni za zamani sana, sensa iliyoangalia mwaka 1984 ndiyo takwimu inayotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba sekta hii inachangia pato la Taifa kwa asilimia 4.6 ambayo tunaona ni kidogo sana. Lakini tuna-*base* kwenye takwimu zipi? Kwenye takwimu zile zile za mwaka 1984. Kwa hiyo, kwa kutumia vigezo hivi vyā *identification* na *specialization*, tunaweza tukajua na tukapata takwimu ambazo ni *up to date* na tukaweza kuzitumia kujua sekta hii ya mifugo inachangia kiasi gani cha Pato la Taifa. Lakini vile vile, kukuza na kuendeleza na kuboresha soko la mifugo. Tunaboresha viyi, tunaboresha soko la mifugo kama wenzangu walivyosema kwenye masuala haya ya kuondoa kutia *mark* kwenye ngozi za mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunaona kwenye ukurasa wa 4, kwenye hizi *provisions* kuna hili neno ningependa lifanyiwe marekebisho kwa kuleta ufanisi. Tunasema kwamba “*complimentary identification system means the use other livestock identification system other than the National Livestock Identification and the Registration System for specific purposes*”. Sasa, kutakuwa na zile *National Identification System* ambazo zimebekwa, labda kutakuwa na *mark* fulani kwa ajili labda ya *National Identification*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa wale wenzetu ambao wanapenda kufuga kijadi, tumesikia hapa kwa mfano wenzetu Wamasai wanatambua mifugo yao kwa kuweka alama za kijadi. Kwa hiyo, bado Muswada huu wala wasiwe na wasi wasi, bado Muswada huu unawagusa kwenye hii *page number* 4, kwamba mbali na kwamba watakuwa na *National Livestock Identification and Registration System*, bado watakuwa na *other identification system*, wataweza kuweka *mark* zao zozote zile. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi wenzetu wa jamii ya Kimasai, hizo *mark* zao za kijadi zinaingia ndani ya Muswada. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa tufanye marekebisho kidogo hapa kwenye huu ukurasa wa 8, kifungu cha 6(4) “*registration of premises for traceability*”. Jamani ninavyoona, hii *registration* bado lazima iongezwe. Hapa tumesema *within seven days* mtu anatakiwa awe amekwisha-*register* mifugo yake. Sasa nikiangalia hapa makampuni ya simu wamesema tufanye *registration* kwa simu zetu, wengine mpaka leo hatuja-*register*, na ni simu tunazitumia kila siku. Sasa fikiria yule mfugaji wa kawaida na piga picha kwa wale wafugaji kwa mfano Mkoa wa Mara mtu ana ng'ombe kuanzia 6000, 10,000, 12,000, huyo ni mtu mmoja. Sasa ina maana yule mtu ataacha shughuli zake zote kila siku aende ku-*register* mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na ng'ombe kuanzia 6,000 ina maana wanazaliwa ndama kila siku, kwa hiyo wewe hata kama ni mwalimu, basi utaacha kazi yako ya ualimu, utafanya kila siku kazi ya kwenda ku-*register* hiyo mifugo. Lakini najiuliza katika kifungu hiki, ni nani anayelazimika ku-*register*? Ni Halmashauri itakuwa inawafuata wafugaji kule waliko na ku-*register* mifugo? Je, pia itawatoza tozo fulani? Maana yake tusije sasa tukawa tunaongeza *unnecessary cost*, kwamba wafugaji sasa inabidi walipie ile *registration fee*, kitu ambacho tunawaongeza wafugaji mzigo. Au vile

vile tunaiongezea Serikali bajeti kwamba sasa inabidi Halmashauri ziongezewe pesa kwa ajili ya kufanya kazi hii ya ku-*register* mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hapa, nia ni nzuri kwamba lazima twende kwenye ufugaji wa kisasa, lakini sasa huu ufugaji wa kisasa tunaufanyaje? *Seven days*, Mheshimiwa Waziri hazitosh, ningekuomba na ningeshauri angalau uweze kuweka miezi sita watu waweze ku-*register* mifugo yao. Kama ilivyo simu, waliweka miezi sita ikashindikana na sasa mwaka na sijui itakuwaje. Kwa hiyo na kwa upande huu tuangalie hilo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 11, ningependa pia kutoa maoni kwenye hiki kifungu cha 12(1). Hapa tunasema: “*A Local Government Authority shall within its organizational structure designate one of its officers*”. Jamani, “*one of its officers*” Hii ni *livestock section*, hapa zinatakiwa *specialization* za watu zitambulike, huwezi tu ukachukua mtu yejote ukamweka kwenye kifungu hiki. Kwa hiyo, naomba hapa isiwe “*one of its officers*”, badala yake liongezwe neno “*any veterinary professional*” na ikiwezekana aweze kutajwa ana *level* gani ya hiyo *qualification* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vige kwenye kifungu hicho cha 12(2), ningeomba hapa kwenye sehemu (g) waweze kuongeza kazi ya “*registrar and maintain a register or computerized database of premises and identified livestock and livestock products for the purpose of monitoring livestock movement....*”, lakini pia tuweze ku-*monitor epidemiological status*”. Kwa hiyo, ningeomba haya maneno yaongezwe ili kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 12(4) wamerudia tena hawakutaja huyu mtu. Wamesema “*a Local Government Authority shall within its area of jurisdiction, appoint from among its employees*”. Haifai, lazima hapa u-*identify*, lazima awe *veterinary professional* na awe na *level* gani ya hiyo *professional* yake, kama ni *graduate*, kama ni nini, lakini lazima wa-*identify*, ukiacha tu wazi namna hii, wanawenza kuchukua mtu yejote ambaye hana utalaam wa mambo ya mifugo, sasa sijui atawenza kufanyaje hiyo *specialization identification* ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vige vige napenda pia kujielekeza kwenye ukurasa wa 13. Tunapokuwa tunafanya hizi *retention of livestock records*, kwenye hiki kifungu cha 14(3) “*...records refer to under sub-section 2 shall be taken when the animal...*” Hapo wame-mention mambo mengi sana na bahati nzuri wametaja kitu “*inseminated*”. Lakini napenda pia baada ya “*inseminated*” waongeze neno “*castrated*”. Wanyama wanaopelekwa kule “*castrated*” lazima tuwe na *document* na sababu ni kwa nini wanyama hawa wanakuwa *castrated* kwa ajili ya mambo ambayo ni ya *future*. Kwa hiyo, hapo waongeze hilo neno *castrated*. Lakini, vige vige waongeze *slaughtered* hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukua huu Muswada mwingine huu wa *grazing land*, Muswada pia ni mzuri sana, lakini una upungufu mdogo sana ambao pia ningependa Waziri na watalam wake wajaribu kujielekeza huko. Kwenye hiki kifungu cha 4, ningependa kwenye hii sehemu (c), kifungu cha 4(2)(c). Kwanza, hatuna *National Pastoral and Agro-Pastoral Organization*. Hizi hazipo kwenye nchi yetu, kwa hiyo badala yake ningependa waweke “one representative from pastoralists or agropastoral association ambazo tunazo hata kwenye village level. Kwa hiyo, wajaribu kuingiza hili badala ya kuweka hiyo *National Organization* ambazo hatuna kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kwenye (k) naomba iongezwe (l) iwe tena “one representative from reputable NGOs” ambaye ana-deal na *animal keeping or livestock keeping*, kwa hiyo wangeweza kuongeza na waongeze tena (m) “one representative from farmers association” ambaye ana-miss kwenye hawa *representatives* wote, hakuna mtu yejote kutoka kwenye *farmers association*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 11, kifungu cha 7(2), huyu mtu akiwa *Bachelor Degree in Animal Science* anafaa, *Veterinary Medicine* anafaa, *Animal Feeds Technology* anafaa. Lakini, hata *Food Science* angeweza pia kutufaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kwa kweli sikukipenda na naungana na wenzangu wote kwenye huu Muswada wa pili ni ukurasa wa 15 hasa hiki kifungu cha 20. Hii sheria ni sheria ya mkoloni, yaani hapa mtu anaingia anaanza kupunguza mifugo. Hivi kama ni mfugaji, Mkurya wa kule Tarime nina ng’ombe 20,000, unaniambia sasa unatakiwa uanze kufuga ng’ombe 100 tu! Nadhani haya ni mambo ya kiukoloni kabisa. Kwa hiyo, ningewomba Mheshimiwa Waziri atumie busara yake, *delete* hivi vifungu vyote hapa kwenye huu ukurasa wa 15, hiki kifungu cha 20 kuanzia (1), (2) mpaka (3), ondoa, kwa sababu kwa kuviweka hivi kwa kweli utakuwa unawanyima haki wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Wizara kwa kuleta Miswada hii, hasa hili jambo la *tracing*. Sisi kule Tarime, Serengeti, Musoma Vijijini tuna shida sana ya wizi wa mifugo. Wenzetu wanaweza wakawa wanachangia, hawaoni faida ya Miswada hii. Lakini kwa Mkao wa Mara nakwambia Muswada huu utakuwa kama ni mkombozi. Tunashindwa leo hii ku-*trace* mifugo yetu. Tunaibiwa na nchi jirani – Kenya, lakini tun-*trace* vipi? Hatuwezi kui-*trace*. Lakini, ningewaomba wajielekeze kuweka zile *identification mark*, labda mfugo wa Tarime, uandikwe kabisa huu mfugo wa Tarime, Tanzania. Hata kama utakapokuwa unavuka kwenda upande wa pili wa Kenya, basi tuweze ku-*trace* kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ukiandika mfugo wa Tarime, ngozi yote imekwishaharibika. (*Kicheko*)

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabla sijasema ninayotaka kusema, naomba

kwa namna ya pekee kwanza niishukuru Serikali na Wizara kuleta sheria hii. Hii ni sheria muhimu sana, sana, sana. Huwezi kuwa na ng'ombe wanazurura tu, hawajulikani, wanaharibu mazingira, halafu mtu anajaribu kuchachamaa hapa. Haiwezekani, lazima kuwe na *control*. Huo ni utamaduni duniani kote tu, lazima ifanyike hivyo. Huwezi kuwa na ng'ombe wanazurura tu, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijasema ninayotaka kuyasema, naomba kwa namna ya pekee kwanza niwape pole sana watu wa Kasulu Mashariki na hasa Kijiji cha Mlufita ambacho majuzi walivamiwa na majambazi ambao wanahisiwa wametoka nchi jirani na kusababisha vifo katika kijiji kile. Naomba wajue kwamba na mimi Mbunge wao niko pamoja nao katika maombolezo hayo. Pia niwaombe watulie, Jeshi la Polisi linazidi kuwatafuta maharamia hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa namna ya pekee naomba niwapoze Kikundi kikubwa cha Waendesha Pikipiki katika Mji wa Kasulu ambao walimshika muuaji, lakini tumesikia muuaji na wenzake wametoroka katika Kituo cha Polisi cha Kasulu. Lakini nimewasiliana na *OCD* na *RPC* kwamba wanafanya kila jitihada kuwapata hao walitoroka lakini pia kuwashughulikia wale waliowatorosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa kwetu hili ni jambo kubwa kwa sababu ya jiografia yetu na tuko mpakani na nchi karibu tatu, tuna Kongo, Burundi na Rwanda, kwa hiyo masuala ya kiusalama kwetu ni muhimu kuliko jambo lolote. Kwa hiyo, niwaombe wananchi wa Kasulu na hasa Kasulu Mashariki watulie, vyombo vyetu vyaa usalama vinafanya kazi hiyo kwa juhudu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niongeze kwa kusema mimi natoka katika Mkoa wa Kilimo, natoka katika ile Mikoa sita iliyotengwa kwa ajili ya kuwa Ghala la Taifa. Umuzi ule wa kututenga kuwa Mikoa ya Kilimo, tafsiri yake ilikuwa ni kwamba lazima tuwe na maeneo ambayo hayapokee mifugo ya ziada ili tuzalishe chakula na maeneo mengine yapokee mifugo. Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka kuna maeneo ambayo yalikuwa *earmarked* kupokea mifugo ili kuondoa hii *conflict* ambayo inajitokeza katika maeneo mbalimbali kama ilivyokuwa inatokea katika Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme kwamba sisi katika Mikoa ya Kilimo na hasa nizungumzie upande wa Mkoa wa Kigoma, tumekuwa *victims* wa mifugo iliyozidi kutoka katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, toka Mwanza, toka Shinyanga, toka Tabora. Wale wafugaji wanapokuja katika maeneo yetu, kwa kweli ukiangalia kimsingi wanafuata majani kwa sababu sisi tuna hali ya hewa nzuri zaidi. Lakini hawa watu wanavyokuja kwa sababu wanakuja kiholela, wanakuja kutuharibia mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikueleze tu au niliambie Bunge hili kwamba uholela huu ukiendelea bila hii sheria ambayo i naiona kama ni mkombozi, hakutakuwa na Ziwa Tanganyika, ndiyo, kwa sababu *echo system* ya Ziwa Tanganyika sasa imevamiwa na ng'ombe malaki kwa malaki ya ng'ombe kutoka katika Mikoa ambayo ina shida ya malisho. Kwa hiyo, Waziri Magufuli, sheria hii ya kuwa-*trace* ng'ombe hawa, ya kuwa-

identify ng'ombe hawa wanatoka wapi na hata maeneo ya malisho kulindwa kisheria ni hoja ya msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko nchi nyingi sana zinafanya mambo haya. Mimi niliishi Australia, Australia ni nchi ya kilimo, ni nchi ya mifugo pia. Wana maeneo maalum *earmarked* kwa ajili ya kilimo na maeneo *earmarked* kwa ajili ya mifugo. Sasa wenzangu walikuwa wanazungumzia habari ya huduma kwa wafugaji. Hilo ni jambo la kiutawala ambalo Mheshimiwa Waziri bila shaka aliangalie kwa sababu ni jambo la msingi vile vile. Lakini msingi wa sheria yenyewe ni kwamba lazima sasa mifugo yetu iwe *controlled* kwa maana ya kujulikana, iko wapi na inaswagwa kutoka eneo gani kwenda eneo gani. Kwa hiyo hii sheria naiona ni sheria ya msingi sana, sana kabisa na pengine imechelewa hata kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa ni nchi ya ajabu kabisa kwamba mifugo wanatembea tu kwa sababu kuna uhuru wa kutembea, hakuna kitu kama hicho. Lazima kuwe na *intelligent control* ya vitu hivi. Leo hii ng'ombe wanazurura mpaka wako kwenye *banks* za Lake Tanganyika sasa maeneo ambayo ni Hifadhi ya Urithi wa Dunia. Chepechepe yote ya Malagarasi, imevamiwa na imekuwa ikitusumbua sana kwa sababu ile sheria ya hifadhi ya mazingira kidogo imekuwa *weak* haitusaidii sana. Lakini nina hakika sheria hii ambayo itakuwa inajielekeza katika kujua mifugo hii iko wapi, ni mifugo ya nani, inatoka wapi na hata lile eneo la malisho ambalo Mheshimiwa Kirigini anasema lifutwe, nafikiri hapana, lirekebishwe tu. *Grazing land* lazima iwe *controlled*, huwezi kuwa na ng'ombe malaki wana-graze kwenye eneo dogo, wataharibu mazingira tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbaya zaidi hawa ng'ombe wanaozurura, tena wengine wanakuja kule kwangu wanatajwa kwamba ni ng'ombe wa baadhi ya Wabunge katika maeneo haya. Hawa ng'ombe, pamoja na kwamba hatuna ugomvi na wafugaji moja kwa moja, lakini lazima kuwe na *echo balance* kati ya maeneo ya *grazing* na hifadhi ya mifugo. *In fact* nafikiri tungefanya kama nchi za wengine wanavyofanya, hii sheria pia imlazimishe huyu mtu kama ngombe wakiwa wengi, awauze kwa nguvu. Asidhulumiwe tu, lakini wauzwe, fedha achukue yeye, lakini wapungue. Huwezi kuwa na ng'ombe wamezagaa tuu, mfugaji mwenyewe kachoka, ng'ombe wamechoka na watoto hawasomi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magufuli kule kwangu tuna tatizo jipya linalojitokeza kwa *Community* ya Kisukuma nitakuomba uje kule kwangu maana sasa hata watoto hawasomi. Wanakaa kwenye mapori makubwa, tunapata tatizo jipya linalojitokeza, kuna rafiki yangu mmoja anaitwa Masanja kule kwangu ana ng'ombe 700, ana wake 6, ana watoto 15, lakini watoto hawasomi. Sasa mimi kama Mbunge haiwezekani kuwa katika eneo ambalo watu hawasomi, haiwezekani hata kidogo, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aje Kasulu aone Wasukuma wenzake ambao wamekuja kwa nia ya kufuga lakini wanatuharibia mazingira vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekeze mchango wangu mahsusni katika ukurasa wa 11 wa Muswada huu wa *Identification, Registration and Traceability*, kile kipengele

naona hata Mheshimiwa aliyetangulia amekizungumza. Ushauri wangu ni kwamba, nafikiri kile kipengele mngekiboresha, kile ambacho kinazungumzia habari ya *Livestock Identification and Traceability Agent* ukurasa wa 11(12) ambacho kinazungumzia habari ya *Local Authority shall within its Organizational Structure designate one of the officers to be a Livestock Identification, Registration and Traceability Officer.* Nafikiri mngekiboresha, rather than having an Agent kuwe a special Committee kwenye Halmashauri ambayo inaweza ikaongozwa na a Veterinary Scientist. Kwa hiyo, hainisumbui lakini tuondoe Mamlaka hayo kwa mtu mmoja ambaye atajiita yeye ndiye *Traceability Officer.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza itapunguza vishawishi vya rushwa kwa sababu *by nature* wafugaji ni matajiri wanatembea na benki, wanatembea na utajiri ule. Kwa hiyo, ni rahisi kum-corrupt mtu yoyote, kwa hiyo, nashauri very strongly kwamba kwa sababu maeneo haya yako chini ya *Local Authority rather than saying* kuwe na *Agent* mmoja nashauri kuwe na *a specialized committee* ya *Registration* na *Traceability* katika *Local Authorities* zetu, sasa inaweza ikawa *chaired au manned* na *Veterinary Scientist* ambaye atakuwa anaongoza hiyo *rather than having an individual* ambaye utam- *designate* kama *Agent* ambaye ataajiita *Traceability Officer*, hapana kuwe na *specialized committee* ambayo pia inaweza ikawashirikisha hata *experts* wa Mazingira katika baadhi ya maeneo fulani fulani lakini inakuwa katika *powers za Council.*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nzungumzie juu ya elimu ya wafugaji. Hili limezungumzwa na wachangiaji wengi na nakubaliana nao. Nadhani kama kuna vitu ambavyo tunapungukiwa ni elimu kwa wafugaji. Nilikwenda Ethiopia wakati huo nikiwa Serikalini nikaona jinsi sekta ya mifugo inavyotoa ajira kwa vijana na viwanda vya sekta ya mifugo kusema kweli hili ni jambo ambalo lazima tulitazame kwa makini sana, wafugaji hawa hawana elimu ya kutosha mifugo badala ya kusema iwe ni *a moving bank*, iwe ni faida, mifugo inakuwa inaongeza umaskini tu kwa watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sisi kwetu tumeanzisha minada hii kwenye mipaka kwa maana ya kushawishi soko la mifugo lipanuke na hawa wafugaji wauze mifugo yao ili kuweza kuboresha maisha yao na familia zao. Suala la elimu ni suala muhimu sana na pengine katika bajeti inayokuja Mheshimiwa Waziri aje na *package* maalum kwa ajili ya elimu kwa wafugaji, ambayo itakwenda sambamba na kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Wafugaji ili waweze kujua kuwa mifugo ile ina faida kwa na pia ina faida kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Sheria hii kwa sisi watu wa Kasulu hasa Mkoa wa Kigoma ambao tumepokea mifugo mingi sana kutoka maeneo ambayo walifukuzwa wafugaji hawa kutoka Ihefu wanakuja Kigoma, kutoka Shinyanga wanakuja Kigoma, kutoka Tabora wanakuja Kigoma na hasa wanakuja Kasulu Mashariki maana ndiyo eneo lenye rutuba. Nafikiri sasa wanavijiji wenzangu katika vijiji vya Kata ya Kongwe mpya

ambako kuna mifugo mingi kupita kiasi, kule Titye, kule Helushingo, kule Mvugwe Makale, Kitanga nadhani Sheria hii itatusaidia na imekuja kwa wakati wake na niombe tu Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa anaanda Kanuni zake yapo mambo ya kiutawala bila shaka ambayo ni muhimu kuboresha huduma za wafugaji, elimu kwa wafugaji vitakuwa ni vitu ambavyo vitatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namwaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo kuhusu hili suala la minada ya mifugo kwenye mipaka walipe kipaumbele cha aina yake. Nchi za wenzetu wanaweza sana sisi kama nchi biashara ya mifugo inaweza kuwa ni biashara kubwa sana kama minada yetu itaimarishwa katika *level* za *Local Authority* kuititia fedha zetu za *DADPS*. Nafikiri Mheshimiwa Waziri na Wataalam wenzake, mabingwa wa mifugo waliopo wanaweza kutembelea baadhi ya maeneo hasa katika Mkoa wa Kigoma ambako tuna minada mingi na wakatusaidia namna ya kuboresha na pia siyo vibaya hata kwenye bajeti yetu inayokuja pia akapanga fedha kidogo hiyo hiyo anayoipata maana najua anapata fedha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa fedha hiyo hiyo anayoipata basi apange fedha mahsus kwa ajili ya ku- *strengthen* hata kama maana yake ni kitaaluma. Ku-*strengthen* minada hii katika mipaka hasa katika mpaka wa Kigoma na nchi za Burundi, mpaka wa Kigoma na DRC iweze kuwa na manufaa zaidi kwa wafugaji hawa. Hii Sheria yetu naona imejiegemeza sana kwa wenzetu wa *Local Authority* kwa maana ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula nao wajiandae.

MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri wa Mifugo, Naibu Waziri wa Mifugo, Katibu Mkuu pamoja na Wizara kwa ujumla kwa namna ambavyo wameweza kujitahidi angalau kuboresha kwa kiasi kikubwa kuwaboreshea wafugaji kwa maana ya kuwapa unafuu wa huduma katika ufugaji mzima wa mifugo. Nakumbuka katika miaka michache ya nyuma tulikuwa na tatizo kubwa la majosho na mifugo mingi ilikuwa inashindwa kuoga kwa sababu gharama ya *dip* ilikuwa ya juu sana, lakini tunaishukuru Wizara angalau kwa kiasi fulani imeweza kuleta *dip* za ruzuku, kwa hiyo mifugo mingi inajiepusha na magonjwa ambayo mifugo wengi wangeweza kufa na kusema kweli magonjwa kwa 50% kama ng'ombe au mifugo inapata dawa basi zaidi ya 50% ya magonjwa yangeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishukuru Wizara lakini tunaiomba iendelee kufanya juhudhi hii ambayo ni pamoja na utoaji zaidi wa chanjo kwa ajili ya mifugo hii ya wafugaji. Katika hizi Sheria mbili mimi binafsi naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kuunga mkono hoja ni kwamba, kwanza tutakapokuwa tumeweza kutambua mifugo tuliyonayo, itatupa unafuu zaidi wa kuwa sensa ya idadi ya mifugo tuliyonayo na kwa kutambua hilo itawezesha hata bajeti ya

Serikali katika kuhudumia mifugo hii tuliyonayo kwa maana ya madawa kiasi gani yanatakiwa, wapate huduma kiasi gani, itatusaidia sana. Halikadhalika katika wimbi hili kubwa tulilonalo la wizi ni imani yangu kwamba huu usajili na utambuzi utatusaidia kwa namna ya ku-control wimbi kubwa la wizi hasa kule kwetu Mkoa wa Mara, ukiangalia zaidi Tarime kwa sababu ya kutokuwa na utambuzi huu wa mifugo, wizi ni mkubwa lakini kila wanapoiba na watu wanaauawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwamba tutakopofika kwenye huo utaratibu wa kuwawekea namba kwa kweli hasa kule kwetu mara kule basi ni vizuri zile *tag* zikaonyeshwa kwamba hii ni *tag* ya Mkoa wa Mara. Hiyo itatusaidia hata ng'ombe wanapovuka nje ya Mkoa pale basi iwe rahisi sana kufuatilia na inawezekana kwa kiasi kikubwa itasaidia watu wetu wengi wasiweze kufa kama ilivyo sasa, pamoja na hii mipango mizuri ambayo imeweza kuletwa na Wizara nadhani kikubwa ambacho kinapaswa kifanyike ni suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu kwa kweli halipingiki na hata hawa watu wetu au Waheshimiwa Wabunge kwa namna walivyochangia kwa kutokubaliana na Muswada huu ni kwa sababu tu wanajaribu kulinganisha elimu waliyonayo wale wafugaji wetu na namna ambavyo Sheria inakuja, kwa hiyo, inaonekana kama ni jambo ambalo haliwezekaniki. Ndiyo maana tunaomba kwamba elimu ni suala la msingi sana maana ukiangalia umuhimu wa mifugo katika nchi yetu ni mkubwa kwa maana kwamba katika *data* tulizonazo katika Afrika Tanzania ni nchi ya tatu kuwa na mifugo mingi lakini kusema kweli hii mifugo haijatusaidia, haijasaidia wafugaji wetu kwa sababu kati ya watu ambao wanaonekana ni maskini ni pamoja na wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani mojawapo ya elimu kubwa inayotakiwa kufanyika ni kuwaelimisha wakulima au wafugaji hawa wajue kuwa wanapaswa kufuga ng'ombe wa aina gani. Sijui hili lina ugumu gani katika Wizara yetu katika kulismamia maana wafugaji wetu wengi kwanza wanafuga hawa ng'ombe wa kienyeji kama kule Mara tunafuga ng'ombe wanaoitwa ZEBU, ili umfuge ZEBU aje awe na uzito wa kuweza kuuzwa akakupa shilingi laki nne lazima umfuge kati ya miaka saba na miaka tisa. Sasa miaka saba na miaka tisa huyu mfugaji lazima atakuwa maskini, lakini ninachojua Wizara ikipenda na ikiamua leo ni rahisi zaidi kuwahamisha wafugaji wetu hawa badala ya kufuga kienyeji waweze kufuga kisasa na hawa ng'ombe au mifugo wanaowafuga waweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli elimu inayopaswa kutolewa hapo ni kwamba lazima tufuge ng'ombe wa aina mbili. Ng'ombe wa kwanza, aidha, tufuge ng'ombe anayeweza kutoa maziwa ya kutosha kama ni ng'ombe wa maziwa au ni ng'ombe wa nyama basi tuweze kufuga ng'ombe wanaoweza kukua kwa muda mfupi na wanaoweza kuwa wakubwa na wakatoa nyama za kutosha kwa mfano, ukizungumzia habari ya ng'ombe wa maziwa lazima ujielekeze kule *Frisian* na ukizungumzia ng'ombe wa nyama lazima ujielekeze kule kwenye *borani* na wale wengine kama Umasaini wako ng'ombe wanaitwa *Sahiwa*, kwa hiyo kama hivyo ndivyo sasa nadhani, Wizara ina hilo jukumu la kuendelea kuelimisha wafugaji lakini si kuwaelimisha tu katika hizi *Ranch*

zetu tulizonazo zote basi hebu wazalishe *mitamba* mingi ya hao ng'ombe wa maziwa lakini na madume wengi kama *borani* kwa ajili ya nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani maana leo ukizungumza habari ya ng'ombe kama *borani*, ukimfuga kwa muda wa mwaka mmoja na nusu mpaka miwili, ukimuza utapata si chini ya shilingi laki nne. Lakini huyo huyo ng'ombe ambaye unamfuga miaka miwili hawa wa kwetu ZEBU, lazima umfuge miaka tisa ndipo uweze kuuza shilingi laki nne. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo sasa tutakuwa tumemsaidia zaidi mfugaji na hata ni rahisi na wao wakafuga kisasa kwa sababu wana uhakika kwamba ndani ya muda mfupi watapata fedha na ninachoweza kukisema hapa maana kwa nafasi nyingine naye ni mfugaji, kwa hiyo, ukizungumza wafugaji na mimi ni mmoja wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ufugaji tunaofuga sasa maana tumesikia wapo watu wanafuga mpaka ng'ombe 2,000 - 1,000 lakini bado ukimkuta huyo mfugaji anayefuga ng'ombe 2,000 ndiyo kati ya wafugaji wenyewe tabu kubwa. Maana hata watoto hawaendi shule na yeye kazi yake ni kuoa wanawake wengi ili wamsaidie kuangalia mifugo, lakini ninachoweza kusema nikitoa tu mfano mdogo ni kwamba, leo huyu mfugaji ambaye anaamua kufuga aidha, ng'ombe wa maziwa au ng'ombe wa nyama na nitoe mfano mdogo tu kwenye nyama na akafuga aina ya *borani* peke yake, akifuga ng'ombe 200 ana uwezo wa kuzalisha kila mwaka ng'ombe wasiopungua 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, akizalisha ng'ombe 150 mwaka wa kwanza akienda mwaka wa pili ni kwamba, atakuwa na uhakika wa kupata kati ya milioni 45 na milioni 60. Akipata milioni 60 maana yake kwa wastani kwa mwezi ni shilingi milioni tano. Sasa hakuna wale wafugaji wa kawaida, hao wanye ng'ombe 2,000 mpaka wenyewe ng'ombe 3,000 hawapati shilingi milioni tano kwa mwezi lakini kumbe akifuga hawa ng'ombe wachache wa nyama anaweza kupata fedha hizo na gharama za kuendesha hao ng'ombe 200 hata ungezipandishaje hazitavuka shilingi milioni moja. Kwa hiyo, bado atakuwa ana shilingi milioni nne, milioni tatu za kumwezesha kuishi katika maisha ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema kwamba, tunadhani pamoja na elimu kubwa inayopaswa itolewe na ni imani yangu kwamba Wizara ina kazi kubwa ya kuweza kusambaza *mitamba* kwa ajili ya hawa ng'ombe wa maziwa pamoja na madume kwa ajili ya *borani*. Baada ya hilo, sasa na hata katika huu Muswada wa Malisho Pamoja na Vyakula, nao ni Muswada mzuri kwa sababu utasaidia yale malumbano kati ya wafugaji na wakulima maana kila leo mara wamepigana, mara wamefanya nini kwa sababu mfugaji anachunga mahali popote, lakini vilevile utasaidia kupunguza suala la uharibifu wa mazingira kwa sababu wanapokuwa wengi wanatembea umbali mrefu kwa ajili ya utafutaji wa maji lakini pamoja na kuhama na hali hiyo wanaelekeza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hiyo, ni imani yangu kuwa, Muswada huu utasaidia katika upunguzaji wa tatizo hilo. Lakini ili hilo liwezekane sasa lazima wale wafugaji wapate huduma muhimu ya maji katika yale maeneo wanayochunga au wanayolisha na vile vile wapate huduma za majosho na hilo ni jukumu la Wizara ambapo Wizara inatakiwa iangalie ni kwa kiasi gani itajitahidi zaidi kuhakikisha kwamba huduma

hizo zinapatikana. Pamoja na mapungufu mengi yaliyoko katika Muswada huu nashukuru kwamba, Waziri ameweza kufanya *amendment* katika ule Muswada wa kwanza wa Utambuzi kwa maana ya kuondoa kile Kifungu cha 6 (4) badala ya siku saba angalau wameongeza imekuwa siku 30. Siku 30 ku-*register* mifugo angalau inaleta mantiki kidogo kuliko ilivyokuwa siku 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini basi tumwombe na kile kifungu cha 20 kwenye eneo la malisho na chenyewe nacho aweze kukifanyia marekebisho. Kwa sababu *Inspector* akiamua tu kwamba leo fulani mifugo punguza maana yake ni aidha, umpe rushwa ili uendelee kubaki na mifugo au ile mifugo yako itauzwa kwa gharama ambayo si gharama halisi. Lakini eneo lingine kubwa ambalo Wizara nadhani inahitaji kuliangalia kwa kweli katika maeneo mengi Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba mazao hayauzwi kwa ule ujazo wa lumbesa, lakini bado yule mfugaji akipeleka mfugo wake mnadani hauna bei, ukifika kule ni mnunuzi ndiye anaweza kuamua anunue kwa shilingi laki moja hata kwa ng'ombe ambaye angeweza kumpa shilingi laki tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kuna haja kubwa ya Wizara nayo kuangalia uwezekano wa kutoa bei za kuanzia za mifugo kama inavyotoa bei za pamba, kahawa na mazao mengine kwamba bei ya ng'ombe ni shilingi kadhaa kwa kilo. Pia ihakikishe kuwa inakuwa na mizani ya kutosha katika maeneo ya masoko au kule minadani ili yule mfugaji sasa anavyopeleka mfugo wake mnadani anajua bei ya *live weight* ni shilingi 1,000 au ni shilingi 1,500 anajua hapo ndipo mahala pa kuanzia, kuliko anavyokwenda maana wakati mwagine yule mfugaji anapeleka mfugo mnadani kwa sababu ana tatizo na akifika kule sasa bei ni ile na kwa bahati mbaya akikuta siku hiyo mto ulijaa, wanunuzi hawakuja, sasa atauza kwa gharama yoyote ile hata kama ni gharama ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunadhani kwa kufanya hivyo nayo Wizara itakuwa imewasaidia sana hawa ndugu zetu wafugaji na kusema kweli kutohaka na matatizo kama hayo yanayojitokeza sasa ambayo siku zote mfugaji anafuga lakini haoni faida anayoipata kwa sababu hata akienda kuuza inategemea na siku hiyo kama amebahatisha bei ni nzuri au bei siyo nzuri. Kwa hiyo, ni imani kwamba Mheshimiwa Waziri kama ataboresha kwenye hayo maeneo ambayo tumeweza kuyachangia na elimu zaidi ikaendelea kutolewa kwa ajili ya wafugaji, basi hali hiyo itaweza kuboreka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Pwani na hasa wanawake kwa kunipa ushirikiano mzuri ambao unaniwezesha kutimiza majukumu yangu vizuri na naomba ushirikiano wao uendelee na mimi nitakuwa nao bega kwa bega. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kabla sijachangia Muswada huu kwa kusema kwamba Muswada huu umekuja wakati muafaka kwa sababu sisi sote tunafahamu jinsi gani nchi yetu

ilivyokuwa inathamini wafugaji na wakulima, lakini ni lazima kuzilinda na kuzitetea haki za watu wote wawili. Kwa mujibu wa takwimu tulizopewa na Mheshimiwa Waziri za idadi ya mifugo na ukilinganisha idadi ya binadamu waliopo unaweza ukakuta uwiano hauendani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukija kwenye suala la uharibifu wa mazingira ng'ombe mmoja eneo analokula ni kubwa sana ukilinganisha na matumizi ya mkulima kwa hiyo, utakuta mifugo ikiwa mingi lazima kutakuwa na uharibifu wa ardhi na hili sote tumelishuhudia katika maeneo yetu na ukilinganisha sisi watu wa Mkoa wa Pwani kuna maeneo wanakaa wafugaji. Pia kuna maeneo ambayo hawakai wafugaji kwa yale maeneo ambayo walikuja watu kutoka maeneo mbalimbali wakahamishiwa kwenye maeneo ambayo hawakai wafugaji, kwa kweli tulipata tabu sana na tunaendelea kupata taabu kwa sababu mifugo imekuwa ikiharibu mazingira na ukizingatia Mkoa wa Pwani una mito ambayo inanywesha maji wananchi wanaoishi Mkoa wa Dar es salaam. Sasa ni vizuri hili suala hii Sheria ikapita na kuweka hizo takwimu, itatusaidia sana wakati wafugaji hawa walipoingia Mkoa wa Pwani tuliambiwa wamekwenda kwenye maeneo watakuja wataalam watachimba malambo kwa ajili yao na watatengeneza majosho, kuna maeneo zoezi limefanyika na kuna maeneo zoezi halijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule ambako halijafanyika mgogoro umekuwa ukitokea mara kwa mara, ni vizuri Serikali ikalizingatia suala hili na kuisisitiza hii Sheria ikapita kwa sababu lazima tuangalie maisha ya mfugaji na ile mifugo yenewe. Unakuta watu wanahama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine, wanaswaga mifugo, wanafika mahali hakuna miundombinu ya kuwasaidia wao, matokeo yake wafugaji wale wanaishi maisha yanayofanana na mifugo yao, hakuna nyumba bora, hawana maeneo ya kupata chakula, watoto wao hawawezi wakapata elimu kwa sababu wanakwenda kuvamia mapori, mapori yale hayana Miundo ya kutosheleza wao pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna haja ya kuhakikisha kama tunataka Sheria hii pia iende vizuri basi tuhimize pia suala la uundaji wa vikundi kwa maana ya Asasi. Vikundi vya Ushirika, *NGOs*, *CBOs* ambazo hizi zitasaidia kuwaelimisha hawa wafugaji nini umuhimu wa kwenda mahali pamoja, nini umuhimu wa kuwa na Ushirika, wale wafugaji wakatafutiwa soko ambalo litawasaidia wao wenyewe katika kujipatia kipato chao na hata kuangalia mifugo bora, kwa mfano unakuta kuna mfugaji nimesikia ana mifugo 20,000 na wake 20, hili nalo ni tatizo, uzuri nilichofurahi suala la idadi ya wanawake kulingana na mifugo limezungumzwa na wanaume wafugaji, hili limenifurahisha sana kwa sababu Muswada huu ukiuangalia sioni mahali popote panapolinda maslahi ya watu wawili, hawa watoto na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake imekuwa kama ni vitendea kazi kwa wafugaji hao je, katika Sheria hii ni kipengele gani kinamlinda mwanamke huyu anayeolewa kwa sababu ya kwenda kukaa na mifugo. Naomba uangaliwe utaratibu wa kuwekwa kipengele angalau kitakachowezza kuwasaidia na kuwalinda wanawake hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika Muswada huu ambalo nimeliona kwangu ni pungufu, hakuna kipengele chochote kinachomlinda mtoto, mtoto kwa

makabila mengine ya wafugaji anayechunga mifugo mpaka anafikia miaka 14 anapopelekwa jandoni ndiyo anaacha kufuga, sasa hiki kipindi chote hapa anachofuga Sheria iko wapi inayomlinda.

NAIBU SPIKA: Siyo kufuga, kuchunga.

MHE. ZAYNAB M.VULU: Aah! Kuchunga niwie radhi Mama, Sheria iko wapi inayomlinda huyu mtoto anayechunga mifugo. Mtoto yuko na mifugo zaidi ya 20,000, 2,000 au 300 hata achunge ng'ombe watano bado anahitaji Sheria ya kumlinda, tunapozungumza haki sawa kwa wote, tunapozungumza haki ya motto, basi lazima tuangalie huyu mtoto analindwa vipi na hii Sheria na tunataka mtoto huyu aendelee kusoma au aendelee kuchunga tu mifugo, shule tunawajengea wao, wao badala ya kuwapeleka watoto shuleni, watoto wale wanaendelea kuchunga. Naomba suala la maslahi na haki ya mtoto liangaliwe na liingizwe kwenye Sheria hii ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo suala litatusaidia kwa sababu sisi tunategemea tuwe na vizazi endelevu, vizazi vilivyokwenda shule na watoto ambao watakuja kuwa viongozi wa kesho. Watani zangu Wasukuma hakikisheni mnapeleka watoto shule. Kama tunataka kuchunga ng'ombe basi tuhakikishe na watoto wetu tunawapa malezi bora, huu mpango wa kuhamahama unapelekea mahali wafugaji hawa na mifugo kunakuwa hakuna tofauti kwa sababu hawawezi kwenda mahali wakapata nyumba bora akaishi, anakwenda mahala na ye ye analala kwenye mazizi. Sasa ni matumaini yangu Sheria hii itatusaidia na itatuelekeza mahali panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ninachoomba kusisitiza ni kuhusu suala la *Inspector*, mionganoni mwa kazi atakazofanya huyu *Inspector* ahakikishe wafugaji wanapeleka watoto wao shule. *Inspector* akgundua mtoto anachunga ng'ombe, achukue hao ng'ombe iwe maslahi na faida ya Halmashauri na mtoto apelekwe shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE.EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Muswada huu ambao umeletwa mbele na Serikali lakini nimpongeze pia..

NAIBU SPIKA: Hebu badilisha hiyo *microphone* kwa sababu inaleta kelele sana.

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ushauri wako, niipongeze Serikali kwa Muswada ambao wameuleta, najua Muswada huu kama utatumia vizuri, utasaidia wafugaji kwa sababu wafugaji wengi wana matatizo makubwa sana ya maeneo yao na hasa namna ya kulisha mifugo yao na shughuli zingine. Kwa hiyo, nimeamua nitumie nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, niwape pole wananchi wa Wilaya Bukombe waliopata mafuriko kwa siku zilizopita, tulikuwa wote kule, miundombinu imeharibika sana na vitu vingine, shilingi bilioni 1.3 zinahitajika kuirudisha Bukombe katika hali yake. Lakini niipongeze Serikali kwa sababu imewahi kupeleka huduma mbalimbali, naomba waendelee kukamilisha huduma zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwape pole wananchi wa Wilaya ya Bukombe, Wachimbaji wadogo wadogo hususani katika Kata ya Uyovu ambao wamekuwa wakipata shida sana kutokana na operesheni zinazoendeshwa kule. Wananchi wale wanapata shida, dhana zao za kufanyia kazi zinakamatwa. Jambo hili nimekuwa nikilieleza mara kadhaa, naomba Serikali ilisikie kwa sababu wanantumia meseji wanasema wanaishi kama wakimbizi ndani ya nchi yao. Naamini Serikali itasikia, Mawaziri wapo hapa wamesikia, *IGP* amesikia, hali iliyopo kule siyo nzuri, naomba wafuatilie. Lakini niombe pia Vyombo vya Habari, kwa sababu kule tupo porini, mtembelee maeneo yale, mpate nafasi ya kuzungumza na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nitumie fursa hiyo...

NAIBU SPIKA: Sema mpo pembezoni siyo porini.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Msukuma lakini nashukuru kwa kunisahihisha, tupo pembezoni, wengi hawafiki maeneo yale, inawezekana wakati mwininge watendaji wabovu katika Serikali ya Chama cha Mapinduzi wanaweza wakatumia fursa hiyo kwa sababu wanajua habari zao hazitaripotiwa. Kwa hiyo, ninaamini Serikali itafuatilia na nimeshawaeleza, wananchi wanateseka kule, wakaangalie shida iliyopo kati ya wachimbaji wadogo wadogo na mgodi wa Tulawaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niende kwenye Muswada wa Malisho, kipengele cha 16 na 17. Waziri amesema kwamba vijiji vitatenga mipaka ya maeneo ya malisho. Nimeshawahi kuuliza swali hapa Bungeni, tunalo tatizo kubwa sana la maeneo ya malisho kwa wafugaji wetu, uwezo wa vijiji kutenga maeneo haupo, ninachoomba, kwa sababu watu wanaongezeka, mifugo inaongezeka, eneo ni hilo hilo, wakati Muswada huu unapitishwa kuwa Sheria, tuhakikishe Wilaya zitenge maeneo kwa sababu Serikali za Vijiji hazina maeneo ya kutosha, tuangalie uwezekano wa Wilaya kutenga maeneo ambayo wafugaji wataenda kuyatumia, huo ndiyo ushauri wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, asubuhi wakati anajibu swali la papo kwa papo kutoka kwa Mheshimiwa James Lembeli, yapo maeneo ambayo kila wakati tunapanua maeneo kwa ajili ya Hifadhi zetu za Taifa, ninashauri kwa mfano katika Kanda yetu tunayo hifadhi ya msitu wa Burigi, tunao msitu wa Kigosi Meyosi, tutafute eneo mojawapo tulitenge kuwa eneo la wafugaji, tuwagawie maeneo yale ili tuone maana ya mifugo yetu hii maana wafugaji wanahangaika sana kama sivyo basi tuingie ndani hata kilomita kumi kutoka kwenye mpaka wa msitu ili liwe eneo la wafugaji na hatimaye tuone ni namna gani wafugaji hawa wanafaidika na

wataona umuhimu ya Sheria hii, lakini tutakapoagiza tu Serikali za Vijiji, ninaamini tunaweza tukawapa adhabu wafugaji wetu. Huo ni ushauri wangu wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupitishe Muswada huu wa Sheria lakini tuanze kutoa elimu kwa wafugaji, tuelimishe jamii na tuhakikishe kwamba tumetenga maeneo ndipo Sheria hii kama itapita ianze kutumika isianze kutumika kabla ya kutenga maneo haya na kabla ya kuwapa elimu wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 20, sehemu ambapo *Inspector* amepewa mamlaka ya kuondoa ile mifugo kama imezidi katika eneo husika ambapo wanaweza wakatoa hata kama ni kwa kuuza, bado tunalo tatizo la soko kwa ajili mifugo yetu. Wachangiaji wenzangu wamesema hii nguvu aliyopewa *Inspectors*, naona itakuwa ni tatizo sana kwa wafugaji. Nashauri kama tunakubaliana, huyu *Inspector* atumie mamlaka hayo ya kisheria, basi tuongeze kipengele cha kusema kwamba mifugo itakayotolewa iuzwe kwa kiasi cha shilingi kadhaa ili liwe kama soko kwa sababu hawana mahali pa kuuzia, itakapoenda Mahakamani, mifugo hii itauzwa kwa bei ndogo sana na wananchi hawa watanyanyasika na wakati huo hatujaandaa miundombinu mizuri ya soko kwa ajili ya mifugo ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri ama kipengele hiki cha kuuza Mahakamani kiondolewe au tuweke kiwango cha bei ya ng'ombe, mifugo ile ikikamatwa kama ni Mahakamani basi auzwe kwa shilingi milioni moja, hata ni ng'ombe wangu wakikamatwa wauzwe kwa shilingi milioni moja kwa sababu tunajua watakuwa wamepata soko. Lakini bila kuandaa mazingira yale, hali siyo nzuri na wafugaji wengi wataonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu *Inspector* tunampa nafasi nzuri sana ya ulaji na kuharibu utaratibu na mpango mzuri wa Serikali. Mmesikia hapa, nimeanza kwa kueleza jinsi wachimbaji wadogo wanavyopata shida, Serikali haijakusudia vile lakini wanaotekeleza sheria ile kule wanaisimamia vibaya. Naomba kuishauri Serikali iweze kurekebisha suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja lakini watoe elimu kwa wafugaji, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Mimi naomba nitoe pongezi nyingi kwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu, kwa kuleta Muswada huu Bungeni kwa sababu sisi watu wa Rufiji tumevamiwa na ng'ombe ambao hawana sheria yoyote wanayoifuata, wamevamia bonde lote, *the flood plains* ambalo ndilo msingi wa ulimaji wa chakula kwa Rufiji nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hivi, wafugaji wanasema Mtulia hapendi ng'ombe, si kweli. Tulipopokea wale ng'ombe, matatizo na vurugu tuliyopata, kama nilivyosema hapa kwamba takribani watu watano waliuawa, kidogo tumeanza kuwaelewa maana tulikuwa hatujui hawa jamaa wanaochunga ng'ombe, sasa tumeanza

kuwaelewa kidogo na tumeanza kuwa marafiki, hapa ndiyo Serikali inatakiwa ifanye mambo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani, sisi tunaona tumedanganywa kwa sababu tuliambiwa tunaletewa wafugaji na malambo mengi yatajengwa, majosho mengi yatajengwa na *land use* itapangwa vizuri, sivyo ilivyo! Ng'ombe wale wamefumuka, wameingia bonde zima mpaka *delta* wanakula chochote kilichopo pale na kuna kabilia lingine wao hawalimi, ukiwaambia ng'ombe amekula majani ya mpunga, anasema hayo ni majani tu, hawajui kama ule mpunga unatoka katika majani, hii imetuumiza sana. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba Muswada huu ni muhimu sana ili mradi tu tuutekeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika masuala haya, tumeona vile vile wale ndugu zetu wenyewe waliokuja kuchunga, hali yao, hata wakichanganyika vipi, utamjua tu yule na yule, sijui wanaweza wakajibadilisha kidogo wakaonekana kama Wandengereko kidogo hivi, maana wanaonekana kabisa. Watoto wao, hiyo ndiyo hatari, nimezungumza leo asubuhi, watoto hawa mvua yao, jua ni lao pia hakuna suala la mtu kachomwa mwiba aende *dispensary*, wapo porini, hakuna mtu anafanya chochote kule, sasa nasema hivi hamuoni kwamba tunalaumu tulikoangukia bila kulaumu pale tulipojikwaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumejikwaa, *overstocking* ndiyo tatizo letu kubwa na kuheshimiana bila kuwaeleza watu kwamba hawa ng'ombe wakizidi, ardhi haizidi, inabaki pale pale. Kwa hiyo, bila kushughulikia *overstocking* na bila kuwapa elimu watu hawa kwamba mali si ng'ombe, mali ni ng'ombe anatoa kiasi gani cha fedha za kutia mfukoni mwako au katika akaunti yako. Elimu ya namna hii ni muhimu na naona kama imechelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, watawala wa siku zile waliweka kabisa Maasai *Steppes*, *The Central Tanganyika and Sukuma Land for Grazing* siyo Rufiji! Sasa tumeachia wameharibu mazingira kule, mvua hazinyeshi, majani yamekauka, mnawaleta Rufiji, hivi nchi hii tutakwenda? Nasema tena, siwakatai wafugaji lakini nataka tufuge kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wenye kauli katika Serikali hii waanze kufikiria kufanya *Land Use Planning* ya nchi, nikilala, nikiamshwa, Mtulia watu wanafuga wapi, nasema tu wanafuga huko, wanalima wapi, nasema wanalima Sumbawanga na Rufiji sio kila mahali nchi nzima malisho ya ng'ombe, itakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ni yetu wote, tuna haki ya kulima na tuna haki ya kufuga lakini lazima kuangalia, pale mtu analima unampelekea ng'ombe, haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa uchungu mkubwa na ninaomba wananchi wangu wanisikie kwa sababu ndiyo tatizo tulilonalo. Mimi kila nikienda kule, naambiwa

Mzee, ng'ombe wanatupa taabu, lakini siyo ng'ombe ni Serikali ndiyo inawapa taabu watu. Kinachotakiwa ni lazima tupange, mje Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna eneo linaitwa *flood plains*, ng'ombe wote ni marufuku kukaa pale, waletwe juu huku, ardhi kubwa, jengeni malambo, somesheni wafugaji maana ya malambo na matumizi ya majosho, vile vile pajengwe shule za watoto, *dispensary* na kama mtu anaweza kufuga mifugo mingi wachunge wenyewe wasitumie watoto, tuone kama mtu mmoja anaweza kuchunga mifugo elfu mbili mpaka elfu kumi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ndugu zangu hii Sheria msiipingi, tuiboreshe tu, kama ng'ombe wako unasema wapo kila mahali basi kule ulikozaliwa kaa nao kule kule uone kama watatosha, kwa nini unaleta huku, ni kwa sababu ya *overstocking*, *we have to fight overstocking*, tupigane tupunguze hali hii kwa nguvu zote. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unisamehe nasema kwa sauti kubwa kwa sababu mambo yenyeve yamenifika, hakuna kikao kingine, nimeongea na wananchi wanalamika juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nirejee kwenye Muswada huu, ukitazama *Section* ya 8(1)(a)...

NAIBU SPIKA: Muswada gani, iko miwili?

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa *Grazing*, samahani, mimi ugomvi wangu ni *grazing* tu huku kwingine waache watengeneze vyakula wanavyotaka, lakini *grazing* inaharibu nchi.

NAIBU SPIKA: Hebu rudia tena.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtazame Muswada wa Malisho, Kifungu cha 8(1)(a), hapa nguvu alizopewa *Inspector* ni kubwa mno, hata akisikia uvumi tu, tutakwenda kweli na mnajua nchi hii mtu anaweza akakuchukia, akazua jambo tu. Nadhani apunguziwe nguvu hizi, asiingie katika *premises*, atoe *official search warrant* na *notice*. Wamefanya vizuri, wameandika pia *ten Cell Leader* nao watakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section* ya 16, ninarudia jambo ambalo msemajji aliyepita kalizungumzia, kwa kuliachia jambo hili kwamba *the village will do it, the village has no manpower capacity*. Maneno ya *D by D* mmeharibu, tumepeleka pesa nyingi kule, hawawezi hata kuzitumia, wanatumia wao badala ya kufanya miradi, leo unawapelekea ng'ombe, wao ndiyo wafanye *land planning* ya *grazing*! Hii inachekesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, ameniambia Rufiji ina vijiji 98 sasa hivi ni mia moja, vilivyopimwa ni ishirini, kesho unapeleka ng'ombe kule, hiyo *demarcation* utafanya lini? Mimi nadhani njia nzuri ni kwamba *National Land Use*

Plan itamke, tutaboresha mazingira ya *Central* Tanganyika au *Central* Tanzania ili wafuge hapo, tutaboresha mazingira ya Maasai *Steppes* ili wafuge pale, tutaboresha mazingira ya *The Sukuma Land* wafuge pale, siyo kuwahamisha, mara peleka huku, mara peleka huku, sisi mmetuonaje? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kwenda katika Muswada, Kifungu cha 19(1), kinachozungumzia *grazing land inventory*, tunayo *inventory*? Tukifungua ile ramani ya Tanzania, tunaweza kusema ardhi ya malisho ipo wapi? Mimi naona kwenye maji mengi na majani mazuri, basi ndiyo hiyo hiyo *grazing land, no, that is agricultural land not grazing land!* Kwa hiyo, hapa naomba kusisitiza *National Land Use Planning* kwa ajili ya wafugaji, kwa sababu ndiyo itafanya *rational use of land in this country* iwe bora ama sivyo Serikali iko tayari kugeuza jangwa nchi nzima hii kwa kuwfurahisha wafugaji wanaoondoka hatua hii na hatua hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana *inventory* ifanywe kwa dhati na tuambiwe lakini tusiambiwe kwamba Tanzania nzima ni malisho ya ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 20(1) hapo nadhani suala la kupunguza ng'ombe kuna neno, *the inspector may*, mimi hapa nasema *the inspector shall*, iwe na nguvu kidogo siyo anasema *he may do it, no, he shall*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo katika *Section 20(3)*, ninaomba badala ya kumwachia Waziri ye ye ndiye aseme *this is excess livestock*, hapana, Sheria iandikwe kwa sababu mambo haya ni ya kisayansi, siyo wewe unasema hapa leo *livestock size* ni kiasi kadhaa, hapana, dunia nzima imeweka kiwango ambacho ardhi inaweza kubeba ng'ombe kwamba ni kiasi kadhaa. Kwa hiyo, nashauri iwekwe katika Sheria badala ya kusema Waziri ndiye afikirie halafu aseme ni ng'ombe kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nasisitiza kwamba nchi ikatae *seriously* kugeuza Tanzania kuwa jangwa, iweke *Land Use Planning* kwa ajili kilimo na kwa ajili ya ufugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya wafugaji ni muhimu, elimu ya watoto wao pia ni muhimu zaidi kwa sababu hawa watoto tunaweza tukawabadi lisha kabisa badala ya kuhamahama wakawa wafugaji waliotulia mahali na wakafanya kazi zao za ufugaji kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hili suala la nyumba za kuishi, hawa wafugaji tunazungumza nao lakini? Jambo zuri watu waishi katika nyumba nzuri jamani, watu waishi kwenye nyumba, ndiyo wataona uchungu wa mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba sana Serikali iwe na program maalum, kwanza, kukataa kuigeuza Tanzania kuwa jangwa, pili, programu ya kupiga vita idadi ya ng'ombe waliozidi, Serikali isiogope iseme tu ng'ombe hawa basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja, ahsante.
(*Makofii*)

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nizungumze mawili, matatu kuhusu suala zima la Miswada hii kwa ujumla wake. Nazungumza kwa kutumia *microphone* ya Mheshimiwa Batenga kwa sababu ya kwangu ninapokaa haifanyi kazi na kadi yangu pia imepotea, naomba Ofisi waendelee kuchunguza mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kuuongelea Muswada huu humu ndani, nadhani tunajaribu kutafuta suluhisho la wafugaji hawa, kwa maana ya kuwatoa kwenye uchungaji ili wawe wafugaji. Nadhani ndiyo umuhimu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono Muswada huu kama ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuelewe kwamba Tanzania hii ni ya Wakulima na Wafugaji na pia wapo wafanyakazi, ndivyo tunavyozungumza ndani ya nchi hii kwamba Tanzania ni ya Wakulima, Wafugaji na Wafanyakazi. Wafugaji ni kundi kubwa kabisa na kama tutazungumza ‘kilelemama’ kuhusu kundi hili, linaweza likatufikisha pabaya kama hatutaelewa vizuri na kama hatutalifuatilia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu mimi ninatoka katika maeneo ya wafugaji na wafugaji kuwabadili ni kazi ngumu, wako *conservative* kweli hawa, si rahisi kuwabadilisha. Naiomba Serikali kama tunatunga Sheria inayowagusa wafugaji hawa, tukubali kabisa kuwa nao karibu na kuwaelimisha kikwelikweli kwa nini tunatake tuwatoe katika uchungaji wawe wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea kuwaweka sehemu moja, ni lazima tuwape elimu ya kutosha, hawabadiliki kwa haraka haraka, kuna wafugaji ambao mimi nawafahamu kazi yao ni kufuga tu halijui jembe kabisa, ye ye maisha yake yote ni ufugaji, akijiuliza akiachaka kufuga ataishije, lakini kwa vile tunalitambua kundi hili lipo basi ni lazima katika kulielimisha tulitambue. Tuwaambie hasara ya kuwa na mifugo mingi ambao hawaleti manufaa yoyote, wakipata elimu ya kutosha na tukakubaliana kuwaelimisha kwamba ufugaji wa huria bila kujua hata idadi maana kuna wafugaji wengine hawajui hata idadi ya ng’ombe walionao, ye ye ili mradi anaona kundi tu basi anaridhika na anafurahi na hata ukimwambia kuhusu elimu anakuambia naenda kusoma ili iweje, kwa sababu kila kitu anapata, atauza ng’ombe atapata chakula, hana hitaji lingine ye ye anachojuwa ni ng’ombe, kula na kushiba basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama kweli tumedhamiria kuwatungia Sheria, basi na wenyewe tuwaelimishe nadhani watakuwa tayari kuelimika, naamini kabisa, nani asiyetaka maendeleo? Sidhani kama kuna mtu ambaye hataki maendeleo na sidhani kama kweli kuna mtu anapenda kuacha Mji wake, wanahangaika hivi, inawezekana ni kwa sababu hawana elimu na inawezekana pia ni mapenzi yake Mungu, kama kunakuwa na

ukame sasa afanye nini, ni lazima ahame kutafuta maji. Serikali imejiandaa vipi kuwawekea malambo na mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo yao, kwa sababu ni lazima tujue kwamba tunahitaji mifugo pia, nchi hii hatuwezi kuishi bila mifugo, kama tunasifu Botswana na nchi nyingine, mifugo ndiyo inaleta maendeleo na sisi Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo na tunasikitika mifugo wanapokufa, kwa hiyo ni lazima tuwe na mipango thabiti ya kuweza kuwaelimisha wafugaji ili tuendelee kuwa na mifugo. Tuwapatie mabwawa ya kutosha, tuwapatie maeneo ya malisho, hatukatai wenyewe wakielimishwa kwamba ukikaa hapa mpaka hapa na bwawa lako la kunywesha mifugo lile pale, sidhani kama naye atapenda kwenda Tunduru, Rufiji, kwanza ni maeneo ya watu tu wala hawana lolote, watakula nini huko. Wanakwenda tu kule kwa sababu pale pana maji kwa sababu ya mtu wa Rufiji hana hata Mbuzi, kwa hiyo, maji yapo bure tu, kwa hiyo, kweli wanaenda kunywesha mifugo yao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, katika maandalizi ya kuupitisha Muswada huu kuwa Sheria, Serikali ikubali hata kama sasa mnasema kwamba lazima kuwe na idadi fulani ya mifugo na idadi fulani ni lazima ipunguzwe basi tuandae masoko, ukimwambia ng'ombe wako ni kadhaa, ukizidisha hapa ni lazima uuze, atauza wapi, masoko na viwanda viro? Haya yote yawekwe vizuri ili hata kama mnawaelimisha hawa wafugaji basi aweze kujua hayo maeneo ya kupeleka mifugo yake ili aweze kuuza na auze kwa kutumia mizani na mfugaji apate faida, mfugaji akiona atauza kwa faida sidhani kama kuna mtu atakataa kuuza kitu kwa faida, hakuna anayependa kuuza kitu kwa hasara. Serikali ijiandae tu kikamilifu, tuwaelimishe na kuwaonesha, vitu vingine si anaona kwa macho, siyo lazima aingie darasani, anaona kwa macho soko hilo hapo, peleka, atapeleka, mzani huo hapo, peleka kapime, pia atapeleka, anapata hela yake ya kutakata, ni nani ataendelea kubishana na Serikali? Serikali ni Serikali lakini nayo Serikali imthamini huyu mfugaji kwa sababu lazima tuwe na wafugaji hawa na waishi pia kwa amani, hii ni nchi yao jamani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kama kweli tuna nia ya kutunga Sheria hii kwa dhati kabisa na kweli tunakubali kwamba Sheria itawalinda wafugaji hawa na kuwapa elimu na wenyewe elimu ikawatosha, naomba muda uwepo wa kutosha, tusiende kwa haraka, tuna haraka gani, mbona tulikuwa nao siku zote, wanaofanya uadilifu tunawaona, lakini tuone sasa kwa vile tumeshadhamiria, utolewe muda mzuri kama kweli Sheria hii itapita Kanuni zake kweli tuweke muda wa kutosha ili tuwe nao, mimi naamini wako tayari. Naomba suala hili litiliwe maanani nisije nikawa narudiarudia ya wengine lakini cha muhimu ni kwamba uwepo muda wa kutosha na kwamba hawa wafugaji waweze kuelimishwa vizuri, naamini watalielewa zoezi na Sheria hii wakiambiwa kwa undani. Wenyewe mnawasemasema tu kwamba eti hawakusoma, hivi hakuna Wasukuma na Wamasai waliosoma? Mimi wala sijaona Mmasai na Msukuma anayelingana na Mrufiji. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wasukuma na Wamasai wamesoma. Wafugaji wengi wamesoma, naomba msitutangaze hivyo. Wafugaji tumesoma ila tunachohitaji ni ustaraku tu na kupata elimu bora ya ufugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, nazidi kusema naunga mkono Muswada huu lakini Serikali ituboreshee maeneo yetu sisi wafugaji na mtupe muda wa kutosha ili muweze kuendelea kuelimisha na kutoa huduma zote ambazo zitasababisha hawa watu waweze kutulia sehemu moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie nikiwa naongea nikiwakilisha wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini na wafugaji wote nchini kwa sababu mifugo ni utajiri, ni fedha, ni suala tu la kuweka mifumo itakayowezesha zao hili muhimu na rasilimali ya Taifa liweze kuleta thamani inayotakiwa katika kuboresha maisha yetu na kwa hiyo, mwisho wa siku hao wanaolaani mifugo kwa sababu eti inaharibu mazingira, kitu ambacho si kweli, ni pale tu ambapo mifugo inapokuwa imezidi uwezo wa malisho ndiyo mifugo inaweza ikaharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba wafugaji wana hali duni za maisha kwa sababu wanakula nyama, wanakunywa maziwa na wana uwezo wa kujenga nyumba bora kwa kutumia mifugo yao na kwa hiyo, wana maisha bora zaidi. Matatizo ya wafugaji ya msingi yanafahamika na nitataja kidogo katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina matatizo na Muswada wa Nyanda za Malisho, nauunga mkono lakini kwa sababu ya muda siwezi kujuadili. Naomba nijielekeze zaidi kwenye ule Muswada wa Utambuzi, Usajili na Ufutiliaji na michango hii ina uhusiano wa karibu sana na harakati zinazoendelea katika Jimbo langu la Shinyanga Mjini na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla katika ufufuaji wa Kiwanda cha Nyama kilichokuwa cha *Tanganyika Packers*. Mimi naelewa kwa kina hatua zilizofikiwa na tunahitaji kuipongeza Serikali kwa kuonyesha na kuendelea kuona kuwa hatimaye kiwanda hicho kinafanya kazi, mimi nafahamu kitafanya kazi. Nilipenda kianze kufanya kazi nikiwa Mbunge, *Inshallah*, bado muda mfupi kweli kweli lakini naamini kitaanza kufanya kazi kabla sijamaliza Ubunge wangu.

NAIBU SPIKA: Kwani unakusudia kumaliza. (*Kicheko*)

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Wananchi wa Shinyanga wataamua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu nyingi sana za kuunga mkono hata huu Muswada wa Utambuzi, Usajili na Ufutiliaji, mimi nimeziandika kama tisa ambazo zinajenga msingi wa kusema kuwa tunahitaji kuwa na Sheria kama hii. Tatizo tulilonalo kwa Miswada yote miwili, ni wazi kuwa tunayo mifumo kwa mfano hii ya utambuzi, kila mfugaji ana namna ya kutambua mifugo yake isipokuwa hapo suala linalokuja ni kuwa na mfumo mpya, ndiyo hofu. Lakini siamini kama kuna mfugaji anayekataa kuitambua mifugo yake isipokuwa ni kuhamza kutoka kwenye mifumo tulioizoea na kwenda

kwenye mifumo ambayo ni bora zaidi. Mabadiliko yoyote yale lazima yalete hofu mionganoni mwa binadamu, ndivyo hivyo binadamu walivyoumbwa. Kwa hiyo, mimi nawaomba Wabunge wenzangu tuunge mkono Miswada yote miwili. Suala hapa ni kuamua ni lini Miswada hii baada ya kuwa Sheria ianze kutumika. Kutokana na changamoto ambazo mimi naziona na natazitaja moja baada ya nyingine, mwishoni naweza nikasema pengine baada ya kuwa Sheria hatuna haja ya kuharakisha sana kuanza utekelezaji, tukizingatia changamoto hizo ambazo baadhi ni kama zifuatazo:-

Kwanza, kwa sasa hivi uhusiano wa Wizara na Halmashauri zetu hauko wazi sana kiasi kwamba Mkurugenzi anayetajwa kwenye Sheria hii haijaleza uhusiano wake na *DALDO* aliyeko kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, madaraka ya Mkurugenzi yatakasiwi namna gani ili kuboresha msimamizi wa Sheria hizi ambazo zitapitishwa lakini hata *DALDO* anasimamia kilimo na ufugaji. Mimi nadhani kabla ya utekelezaji wa Sheria, ni lazima tuangalie uhusiano wa Wizara pamoja na Halmashauri lakini na huyu *DALDO* labda nafasi igawanywe na kuwa *District Livestock Officer* peke yake na *District Agricultural Officer* peke yake. Kwa sababu majukumu yanakuwa ni mengi sana kiasi kwamba huwezi wewe ukawa unasimamia kilimo na ufugaji kwa wakati mmoja wakati changamoto ni nyingi sana. Tukiendelea na utaratibu huu, naamini hatuwezi kusema tutapata ufanisi unaotakiwa, changamoto ya kwanza hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, Sheria hizi ufanisi wa utekelezaji wake, utategemea sana uhusiano wetu na Sheria za nchi jirani katika suala la malisho kwa sababu mifugo haijui mipaka, inaweza ikaingia hata nchi jirani, udhibiti wa magonjwa na wizi wa mifugo. Kama sisi tuna Sheria hizi bora lakini nchi jirani zinazotuzunguka hazina Sheria zinazofanana na hizi, sisi hatuwezi kutegemea sana ufanisi ambao tunautamani kuwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tatu, nchi yetu ni kubwa sana na mifugo ni mingi. Mifugo hii ni mali na kwa hiyo, mimi sikubaliana na suala la kusema tunapunguza mifugo tu kwa sababu ya kupunguza mifugo mbona wenye hela benki hatujasema wapunguze fedha nyingi walionayo, maana ng'ombe ni fedha. Kwa nini wafugaji tuwaonee kwa kuwaambia punguza mifugo? Ni kuweka tu utaratibu wa kuhakikisha kuwa mfugaji huyu anafaidika na Taifa linafaidika vile vile. Kutokana na nchi kuwa kubwa na mifugo kuwa mingi, ndiyo maana ya hoja yangu ya kusema ni lazima tuwe makini katika kuamua ni wakati gani tunaanza kuitekeleza Sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine, ni lazima tutambue kuwa kuna mifumo mikuu ya ufugaji hapa nchini ambayo ni uchungaji, (*pastoralism*), uchungaji na kilimo (*Agro-pastrorlalism*), ufugaji kwenye mashamba makubwa (*ranching*), ufugaji katika mashamba madogo madogo (*livestock faming*) na ufungaji nyuma ya nyumba kwenye mabanda (*backyard farming*), wenzetu wa Kilimanjaro wanalifahamu hili. Kwa hiyo, Sheria hii ni lazima itambue mifumo hii na hatutarajii kuiondoa kwa siku moja na litakuwa ni kosa kubwa sana kusema tunataka kuelekea kwa mfano kwenye *ranching* au kwenye *livestock farming*, mifumo hii itakuwepo kwa muda mrefu hapa nchini. Kwa

hiyo, tunapoiangalia Sheria hii hususan katika kutunga zile Kanuni ni lazima kuwa na mawazo kuhusu uwepo wa mifumo hii ya ufugaji ambayo haiwezi ikaondoka kwa siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tano, ni elimu kwa wafugaji. Tusipowaandaan wananchi wetu katika kuelewa azma ya Serikali ikianzia kwenye Sera na kwenye Sheria katika maana ya utekelezaji, tutakuwa tunawapeleka wananchi wetu kwenye mifumo ambayo pamoja na azma nzuri lakini inaleta matatizo kwa sababu tu hawaielewi. Ni muhimu sana kuwaandaa wananchi wetu wakaelewa, hawawezi wakakataa na hofu itaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika changamoto nyingine ni uwezo wa Serikali katika kusimamia jambo hili ambalo lina mambo mengi sana. Ninaposema Serikali, hapa ni uwezo wa Halmashauri zetu kuweza kusimamia haya mambo, ndiyo maana nimesema tukiendelea kubakisha DALDO kuendelea kusimamia kilimo na mifugo, siamini kama tunaweza kufikia kwenye ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima vile vile tutambue kuwa kwa sababu mifugo ni utajiri wa Taifa, ni zao la kuendelezwa kuvunwa na kuuzwa ili lichangie katika mapato ya mfugaji na pato la Taifa. Ni muhimu tutambue kuwa katika maana ya thamani ya mifugo, ni lazima useme mfugaji anafuga zao, mfugaji anatunza, mfugaji ni lazima awe na sehemu ya kuuza na sehemu ya kuuza ni kuwa na viwanda na machinjio makubwa ya kisasa. Kwa hiyo, hili la kusema ubora wa mifugo au wingi wa mifugo, litajirekebisha lenyewe kwa sababu mfugaji akishajua nafuga kwa sababu nitaiza pale ili nipata fedha, mfugaji hawezi kuacha kukubali kubadilika. Lakini tusipozingatia suala la *ku-establishing a complete value chain*, hadithi zote hizi tutazipiga kwa miaka nenda rudi lakini hatuwezi kubadili hali ilivyo kwa sasa kwa sababu mifugo ni dhahabu juu ya ardhi lakini hatutaki kuzingatia kuwa lazima kuwe na *a complete value chain* ili kuweza kufaidika na mifugo hii ambayo ni utajiri wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya mwisho, mifugo ni mali ya mtu binafsi, kwa hiyo, Sheria yoyote ile ni lazima izingatie hilo. Nafahamu wafugaji ukilinganisha na wakulima ni kundi la watu wanaonyanyasika sana. Tunayo mifano mingi na ya kutosha mingine ya siku za karibuni ya jinsi wafugaji wanavyoonewa si kwa sababu Serikali inapenda hivyo isipokuwa baadhi ya watendaji wa Serikali wanatumia mianya kuwanyanya waufugaji kwa kuwanyang'anya mali zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nalielewa suala hili kwa kina sana. Ni lazima tuendelee kuwatetea wafugaji katika mfumo wa aina yoyote ukaokuja ili ulete hali bora ya mfugaji na Taifa kwa ujumla tukizingatia kuwa mali yao hii binafsi ni lazima ilindwe kwa sababu asilimia 98 ya mifugo tuliyonayo iko mikononi mwa watu binafsi. Hatuwezi kusema tuanze kuibadili sasa ili iwaje? Lazima itaendelea kuwa hivyo. Kwa hiyo, mifumo yote hiyo lazima tuiangalie katika maana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukizichukua changamoto hizi pamoja na zingine, mimi nadhani Muswada huu pengine urudi kwenye Kamati ili ufanyiwe kazi ili kikundi cha Wabunge wanaotoka kwenye maeneo ya wafugaji waweze kushiriki na kutoa mchango wa mawazo yao katika maana ya kuuboresha Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hii Miswada miwili ambayo imewasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimekuwa na maswali ambayo nimeshindwa kupata majibu kwamba kwa nini iwe sasa na siyo wakati mwingine wowote? Nilikuwa najaribu kulitafakari suala hili kwa kina sana, nikitazama kwanza historia ya uhuru wa nchi yetu na hatua kadhaa ambazo tulizozipitia na hususan katika suala linalohusu mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuwakumbusha wenzangu kwamba mpango huu wa kupunguza mifugo si mpango mpya katika nchi hii. Ni mpango ambao ulikuwepo hata kipindi kile ambacho nchi hii ilikuwa inatawaliwa na Wakoloni. Kulikuwa na mpango wa kupunguza mifugo katika utaratibu uliokuwepo kwa wakati ule lakini wakati huo huo sambamba na zoezi hilo la kupunguza mifugo kulikuwa na vuguvugu la harakati za kudai uhuru wa nchi hii. Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alipokuwa amekwenda *Sukuma Land* kwa ajili ya kukitangaza Chama cha TANU, alikutana na suala hili ambalo lilikuwepo wakati ule, kwamba Chama chako kinasema nini kuhusu mifugo, je, na ninyi mtapunguza mifugo? Mwalimu akasema Chama changu hakiwezi kupunguza mifugo, leo mnawageuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la kupunguza mifugo, ni wazo jema sana kwa mazingira ya wakati huu tuliokuwa nao na kwa sababu ambazo zimeainishwa lakini athari zake ni kubwa na wakati mwingine haziwezi kubebeka. Wazo wa kurudisha Muswada huu ili uweze kupitiwa tena na wadau nafikiri bado lina nguvu sana. Kwa unyenyevu kabisa, tuiombe Serikali na kama wanavyosema mara zote kwamba Serikali hii ni sikivu, nadhani itasikia kilio cha Wabunge hawa ambao wanataka Muswada huu urejeshwe kwenye Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilibahatika kuhudhuria *public hearing* ya Muswada huu pale Dar es Salaam katika ukumbi wa Bunge, namba 12. Nilichokisikia pale na nilicho jifunza, moja, ni kwamba wadau wengi waliofika katika kikao kile na kutoa maoni, walilalamika kwamba wengine wameupata Muswada siku hiyo ya tarehe 31, hawakupata muda wa kuusoma na kuweza kutoa maoni ipasavyo. Lakini ni watu gani ambao wameshirikishwa katika kikao kile cha maoni? Ni makundi machache sana na hususan makundi ya Dar es Salaam tu ndiyo yanawakilisha katika kutoa maoni ya wafugaji wa Mpanda na wafugaji wa Simanjiro na maeneo mengine ya ufugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna jitihada zozote ambazo zimefanywa za kuwashirikisha angalau wawakilishi wanaotoka katika Mikoa ya wafugaji na wao wakashiriki katika kutoa maoni yao kuhusu suala hili. Nadhani nia njema iliyopo ya kutaka Muswada huu urudishwe ili uweze kuangaliwa upya, nafikiri bado ina nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu sana kulitafakari suala hili lakini bado sina majibu ya kutosheleza pengine Mheshimiwa Waziri anaweza akanipa ufanuzi. Katika Sheria ya Malisho, kifungu cha 17, kinatoa haki kwa Serikali za Vijiji kutoa ardhi. Migogoro ambayo tumekuwa nayo katika kipindi kilichopita na ambayo bado ipo na haijapata ufumbuzi, imezigusa sana Serikali hizi hizi za Vijiji ambazo zilishindwa, leo Sheria inawarudishia mamlaka hao hao ili waweze tena kuleta migogoro mingine. Ni Serikali hizi hizi ambazo zimetoa ama kwa halali ama katika njia zisizo za halali kuwamilikisha wafugaji maeneo ambayo baadaye yameleta migogoro mikubwa lakini bado mamlaka ya Serikali hizi yanaingiliwa na Serikali Kuu. Kwa hiyo, hata kuwepo kwa mamlaka hizi ambazo zinazitaka mamlaka za Serikali za Vijiji kutoa ardhi, hofu yangu ni kwamba wanaweza wakaingiliwa kama walivyoingiliwa katika kipindi kilichopita katika Mikoa ya Morogoro na Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wafugaji wengi waliokuwepo katika maeneo ya vijiji, ni wale ambao tayari walikuwa wamekubaliwa katika taratibu za vijiji vile lakini leo wameonekana kwamba wameingia na wamekuwa na makundi makubwa ya ng'ombe. Sasa mipaka na mamlaka haiwezi kufahamika mpaka hatua madhubuti ziwe zimeshachukuliwa katika kurekebisha dosari zilizokuwa zimejitokeza hapo nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane kabisa na wale ambao wameshauri ni lazima Serikali itazame ni namna gani sasa inashughulikia suala la matumizi bora ya ardhi. Mheshimiwa Profesa Mtulia hapa amezungumzia Wilaya ya Rufiji ambayo ina vijiji 98 karibuni 100 vimepimwa 20 tu. Unapoleta suala la kuwapa mamlaka vijiji vigawe ardhi ambavyo havijui mipaka yake bado tatizo litaendelea kuwepo. Sasa ni kipi tunatanguliza na kipi tunaahirisha, ni Serikali kuangalia kwa makini sana suala hili. Hofu yangu ni kwamba jambo hili limesukumwa, halikufanyiwa utafiti wa kutosha na wa kina na athari zake ambazo zinaweza kujitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii hata kama itakuwa ni nzuri kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali isikwepe majukumu yake ya msingi. Kumekuwa na utamaduni sasa wa Serikali yetu kukwepa kila jukumu ambalo ni wajibu wa Serikali kwa raia wake libebwe na raia wenyewe. Suala la gharama zozote zitakazokuwa zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizi ambazo zimeletwa hapa basi zibebwe na Serikali yenye na wala zisiwahusishe wadau kwa namna yoyote ile. Suala la kuwasajili wanyama, suala la kupima ardhi na suala lolote lile ambalo linatokana na kuwepo kwa Sheria hizi, gharama zake kwa namna yoyote ile wasihsishwe wadau kwa namna yoyote ile kama ilivyo katika Kifungu cha 24 cha Muswada wa malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri, imepitishwa *amendment* hapa kuhusu Kifungu ambacho kimepigiwa kelele sana cha namna ya upunguzaji wa mifugo ambacho kilikuwa kinampa mamlaka *inspector*, angalau sasa kinasomeka vizuri na nimeridhika na hiyo *amendment* ambayo inatoa muda wa yule mfugaji aweze kuwapunguza wale mifugo kwa taratibu. Lakini tatizo kubwa ambalo lililopo ni soko la mifugo hiyo. Wakati ule wa Sera ile ya Kupunguza Mifugo, masoko yalikuwepo, *Tanganyika Packers* ilikuwepo, kwa hiyo, walikuwa na uhakika wapi watauza mifugo yao, leo hatuna masoko ya uhakika ya mifugo, itakuwaje? Kwa hiyo, ni vizuri suala la kuwepo kwa mfumo wa masoko yenye uhakika na lenyewe lizingatiwe. Lakini pamoja na kuwepo na masoko bila kuwepo na viwanda ambavyo vitakuwa vinachakata nyama hizo bado tatizo la soko la mifugo la ndani litakuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni umuhimu sasa wa kuwaelimisha wafugaji wetu watokane na ufugaji huu wa sasa waliokuwa nao waje katika ufugaji huu ambao utakuwa ni bora. Lakini hili linahitaji sana elimu na ushawishi mkubwa na utashi wa kisiasa katika kufanikisha azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Muswada huu lakini yapo matatizo mengi katika utekelezaji wake. Ninaamini kabisa kama dosari hizo zitasimamiwa basi Muswada unaweza kuwa mzuri lakini kwa hali ilivyo na jinsi ulivyowasilishwa, sishawishiki kabisa kuunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Muda uliobakia, ingawa nina mse maji mmoja tu aliye baki hautoshi. Kwa hiyo, tutakaporudi saa 11.00, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa atakuwa ndiyo mse maji peke kutoka kwenye upande wa Wabunge. Halafu tutamwita mtoha hoja, atajaribu kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa hapa ndani. Kwa hiyo, sasa hivi tukitoka hapa tunakwenda Ukumbi wa Msekwa kwenye semina ya MKUKUTA. Kama nilivyosema, ni vizuri tuhudhurie semina ile kwa sababu inaelezea mambo muhimu sana yanayohusu maendeleo ya nchi yetu. MKUKUTA ni dhana mpya ambayo ilibuniwa na sisi Watanzania baada ya PRSP za mwanzo zilizokuwa zimeletwa kutoka nje. Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mkashiriki kwa sababu vitu vingine kama sisi wenyewe ndiyo watunga Sheria hatushiriki, inakuwa vigumu sana kuingia katika mtindo wa kutunga sheria. Ni MKUKUTA I unaopita na MKUKUTA II unaoingia, ni vizuri mkashiriki. Kwa hiyo, tutakutana saa saba Ukumbi wa Msekwa, mtawezza kuelezwaa na watalaan mambo yote.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, napenda kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

Waheshimiwa Wabunge wakati naahirisha Bunge kipindi cha kwanza nilisema nina mchangiaji mmoja tu nae ni Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa.

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba na mimi niungane na wenzangu katika kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa siha na nguvu ili tuweze kushiriki katika mjadala huu muhimu hapa Bungeni. (*Makofii*)

Lakini pili, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza kwenye mjadala huu na pia naomba nikushukuru pia kwa uamuzi wako kwamba Wabunge waendelee kuujadili Miswada huu la sivyo haya maelezo na taarifa tulizopata hapa hatungeweza kuzipata kwa hiyo, hili ni jambo zuri. (*Makofii*)

Lakini la mwisho lakini sio la mwisho kwa umuhimu naomba pia niwashukuru wapigakura wangu wa Ulanga Magharibi kwa kuniunga mkono tangu tumeanza mwaka 2005 na kwa kuendelea kuniunga mkono mpaka sasa na nina matumaini kwamba wataendelea kuniunga mkono mpaka mwezi Oktoba, *Inshallah*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu Miswada hii mizuri, kwanza inafanya mapinduzi katika shughuli zetu za ufugaji, mapinduzi ambayo lengo lake ni kuboresha kipato cha wafugaji. Zamani tukiandika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 1995 kulikuwa na mahali tulizungumzia suala la kuwashimiza wafugaji kuweza kutumia mifugo yao kujiondoa katika umaskini, jambo hili tulilifanya na nadhani linaendelea mpaka leo. Ni kweli vilevile kwamba katika mjadala huu wa jana na leo na pamoja na Sheria yenye, mtu unaweza kusema kwamba kuna mambo mazuri na kuna mambo ambayo sio mazuri. Kwa hiyo, ungependa kutumia *balance sheet* katika kupima Miswada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, na dhana ya *balance sheet* sio mpya, wahasibu wanaijua na wachumi wanaijua. Shabaha yao kwa kweli ni kutaka kujua mazuri yanazidi mabaya au mabaya zanazidi mazuri. Mimi naweza kusema kama ninavyoona mimi ya kwamba upo ukweli katika Miswada hii. Kuna baadhi ya vifungu sio vizuri, vifungu ambavyo wenzangu wamevitaja hapa ambavyo vinaleta utata. Kwanza utata katika kutekeleza, lakini utata katika utata wa maudhui tu ya wananchi hasa wakati huu maana suala hili pia la *timing* ni muhimu hasa wakati huu. Sasa hili lazima tulifanyie uamuzi muafaka la sivyo tutakuwa tunafanya maamuzi ambayo baadaye yatatutia kwenye kitanzu, jambo hili nadhani lazima tuliepuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kusema kwa mfano katika Ibara ya Tano katika ile Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Ibara ya Tano, Ibara ndogo ya nne ambayo inataka Serikali kusababisha usajili wa mifugo. Sasa mtu unajiuliza hasa pale kwenye ngazi ya Wilaya pale na kijiji hasa Wilayani pale. Pale kweli tuna uwezo, mimi nafikiria Jimboni kwangu kwanza, wafugaji sisi wengi wameingia katika eneo la Mto Kilombero. Kule ndio walipojaa, sasa unakwenda kwendaje kule, sehemu nyingine kule ni visiwa, yaani mto ule Kilombero una sehemu mbalimbali zimekatika katika hivi ambayo ndani mle mtu akiwa mle yuko kisiwani, unamfuata fuataje ili uende ukasajili mifugo yake au huyu yeeye atoke kule aende mpaka Mahenge kilomita zaidi ya mia moja na hamsini, mia moja na sabini aende akasajili. Kwa hiyo, kuna ugumu katika kutekeleza baadhi ya masharti ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna mambo mazuri, moja zuri ambalo mimi nalipenda sana ni lile la alama, unajua zamani nilikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, tatizo letu la ngozi zetu kuuzika lilikuwa hilo kwamba ng'ombe wale wamepigwa wamewekwa alama, tena wanawekwa alama mpaka kwenye mbavu namna hii, kwenye miguu mle yote alama tupu tena alama ya kuchoma. Kwa hiyo, ubora wa ngozi katika nchi yetu ni hafifu kabisa.

Lakini hata mimi walinionesha Kusini kule kompyuta inaonesha alama ya jiwe alipopigwa ng'ombe na ngozi ilivyoharibika. Kwa hiyo, ubora wa ngozi katika nchi yetu ni mbaya pamoja na kwamba tuna viwanda vya ngozi tumevibinafsisha na havifanyi kazi na mimi nilikuwa mmojawapo, nilitaka kuwanyang'anya wale na kabisa nilitaka kuwanyang'anya wakubwa wale.

Lakini wakafanya ujanja wale, wale waliochukua vile viwanda nilitaka kuwanyang'anya wale lakini hiyo sio hoja ya kutosha ya kuzuia alama za kuwekwa kwenye ng'ombe. Halafu pili hizi alama za asili hizi zingine nzuri lakini zingine sio nzuri, sisi Watanzania tuna mila zingine za asili za hovyo kabisa, moja ya mila ambayo haifai ni hii ya kukeketa akinamama na wasichana, hii haifai hii lazima tuifute kabisa. Inadhalilisha akinamama, inatuzuia kutupa heshima katika dunia, lakini tunafanya, Sheria ipo lakini bado watu wanafanya mpaka leo. Lakini jambo hili ni baya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kuna mila ambazo lazima tuondokane nazo, mojawapo ni hii ya kuchoma ngozi ng'ombe na kukeketa, mnaharibu mambo mazuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mle kwenye Muswada Ibara Ndogo ya Tano, siwezi kuisoma kwa sababu ni ndefu inasema mambo mazuri sana juu ya teknolojia itakayoitumia katika kuwatambua ng'ombe hawa, halafu baadaye wanaweza kufuatilia hata katika suala la wizi la mifugo.

Kwa hiyo, hili jambo ni zuri ni zuri kabisa, mimi naliunga mkono. Lakini sasa nataka kuzungumzia Muswada ule wa pili ule wa *Grazing* hasa katika zile Ibara za 17, 18 na 19. (*Makofi*)

Mimi naona zile Ibara nazo zina matata kabisa licha ya asubuhi hapa mwenzangu Mheshimiwa Simbachawene aliisahihisha badala ya kuiita *village council* iwe *village assembly*, mimi naona hili ni ndogo. Kubwa zaidi mimi linanikera ni lile la *Land Use Planning Act*. *Land Use Planning Act* tumeipitisha mwaka 2006 hapa tena aliyoileta Bungeni hapa nadhani huyu huyu bwana Magufuli huyu, ndio.

Lakini ile haijatekelezwa. Hamna *Village Land Use Plans* nchi nzima hii, kama zipo ni chache tu. Wala hakuna *District Land Use Plans*. Kwa hiyo, ile *concept* wanayozungumza kwenye Ibara ya 19 ya *Grazing Land Inventory* haiko, kwa sababu lazima uwe na *Land Use Plan* pale kwenye kijiji ambayo ina-*define* maeneo ya *Grazing*, maeneo ya kilimo, maeneo ya shule, maeneo ya majengo na kadhalika. Sasa hizi *plans* hazipo sasa *how can you discuss about*, utawezaje kuzungumza juu ya kuhesabu vifaa au maeneo ya malisho, haiwezekani mpaka uwe na ile. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema jambo hili limekuja kama *premature* linatakiwa lifanyiwe kazi vizuri ili tuweze kubainisha kwamba hizi *inventories* zipo na hii Sheria yenewe ya *Land Use Plan Act* ina mambo mazuri sana kama unasoma.

Kwanza inazungumza juu ya *planning authorities* na *planning authorities* kuanzia na *National Land Use Planning Commission*, unakwenda kwenye Wilaya pale ambayo ni *District Council* na kwenye kijiji pale ni *Village Council*. Sasa *Village Council* ziko ambazo zimesha *draw* tayari mipango hii ya ardhi ? Mipango bora ya matumizi ya ardhi ? Hatunayo.

Kwa hiyo, mimi naogopa kweli kweli kuwapanga wananchi katika maeneo na kusema kwamba hapa watakuwa na *grazing land*, lakini *land* yenewe haiko kwa hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili naweza kutoa mfano hata kule kwangu pia, pale Itete. Pale pana mpaka uliwekwa zamani kati ya mwendeshaji na wakulima, sasa yule mwendeshaji alipoona mambo yake hayaendi vizuri akaongeza eneo na alipoongeza eneo akaanza kuchoma nyumba za wakulima na wafugaji. Amechoma nyumba zaidi ya 300 pale, mpaka leo tuna mgogoro nae jinsi ya kulipa fidia.

Kwa hiyo, hii *Land Use Plan* haiko, halafu pili pale Kilombero kuna tatizo lingine la *Ramsa Planning* sasa hili nalo halijakamilika bado, sasa kama bado haujakamilika hawa wananchi wafugaji utawapangia maeneo wapi ili waweze kufuga mifugo yao na kuandikisha mifugo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna utata mwangi. Pendekeso langu ni kwamba maandalizi hayajakamilika, maandalizi yenewe kwa maana ya wafugaji pale, maandalizi ya elimu, maandalizi ya maeneo hatujakamilisha, maandalizi hata ya miundombinu unahamisha watu kwa mfano kuna wakati tuliamisha watu hapa tukapeleka mahali hakuna hata josh, hakuna *veterinary centre*, ng'ombe wakafariki ama walikufa, *ok*, basi walikufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba hili jambo tulahirishe kama walivyosema wenzangu kwa sababu *timing* yake ni mbaya, *timing* yake kwa maana ya zile *process* za maandalizi, lakini *timing* yake, tuna mambo makubwa yanakuja hapa mbele mwezi Oktoba, sasa kama mnataka kuleta maneno haya ya nini ? Tutafarakana bure tu hapa.

Kwa hiyo, hatuna muda mrefu tunaweza kuileta tena mwezi Januari au Februari mwakani wakati tumelifikiria vizuri, tumefanya mabadiliko katika mambo ambayo vifungu mbalimbali ili kuviiimarisha kwa sababu kwa kweli mimi hii sheria naipenda, napenda kule Ulanga itumike sheria hii, lakini wakati wake sio *appropriate* na maandalizi hayatoshi bado. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kutokana na maoni yangu haya, mimi napata shida kusema naunga mkono hoja na napenda zaidi kwamba jambo hili tulahirishe ili tujipe muda zaidi ili tuweze kufikia lengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru kwanza kama nilivyosema pale kwa kunipa fursa hii, lakini vilevile kwa kunipa fursa ya mwisho katika mjadala huu kabla ya Mheshimiwa Waziri hajaanza kuchangia na najua ataanza kuchangia ya kwangu kwanza, lakini ndio mambo yenye we yalivyo halisi. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nashukuru sana maana yake wewe ndio umepata heshima ya kuwa mzungumzaji wa mwisho katika Bunge hili, katika Miswada hii.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujikita katika kuzungumzia Fungu la II la Muswada katika ukurasa 14 hadi 15. Nimevutiwa na vipengele Na. 17, 18, 19 na 20 vya Muswada vinavyohusu kwa ufupi suala la “*Grazing Land Management*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kuwa kuna wataalam wazuri sana wa mifugo waliobobea kwenye masuala ya “*Grazing Land Resource Management*” hapa nchini.

Umuhimu wa kuzingatia suala la uwezo wa ardhi au eneo husika kumudu kiasi cha mifugo kutokana na rasilimali zilizopo, yaani “*Carrying Capacity*” (CC) au “*Limits of Acceptable Use*” (LAU). Utaratibu wa kuzingatia “CC au LAU” sio mgeni kwa wataalamu wetu wa mifugo pamoja na Waziri mwenye dhamana ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, tumeshuhudia matatizo makubwa ya uharibifu wa *grazing lands* na kusababisha kuhamahama na mifugo kila mahali hapa nchini na kuleta madhara makubwa zaidi ya mazingira. Matatizo haya yanaendelea hadi leo na hakuna hatua zinazochukuliwa kudhibiti hali hii. Nasita kuamini kuwa sheria hii

itabadilisha hali hii inayoendelea ya kutojali taratibu za “CC” au “LAU” unaotokana na *Overstocking*.

Naomba Mheshimwa Waziri anionyeshe ni vipi sheria hii italeta maajabu ya kuhakikisha kuwa “CC” au “LAC” inazingatiwa katika kusimamia na kuendeleza *grazing lands* au *range lands* zetu.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja hii, naomba nianze kwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja kwa wakati wake, wakati muafaka kwa vile tumepita katika uzoefu wa kutosha hasa kwa kipindi hiki ambacho tumeshuhudia malumbano na hata vifo kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni vigumu sana kutatua migongano hiyo kwa vile sheria na kanuni zake zilikuwa hazipo. Nampongeza kipekee Waziri wa Mifugo na Uvumi, Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa ubunifu wao na hata kufikiria kuleta Muswada huu muhimu sana. Bila shaka sheria hizi na kanuni zake zitasaidia sana kukuza uchumi utokanao na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria peke yake haitoshi, kama hakutakuwa na umakini katika kusimamia. Kwa vile sheria hizi sana sana zitawahusu wakulima na wafugaji, basi ni vizuri kama zitatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Ni muhimu kabisa kutoa elimu na kuwepo na mikakati ya kutosha kuhakikisha kwamba elimu hii inawafikia wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nieleze kidogo kuhusu vyakula. Kumekuwako na udhibiti hafifu sana katika swala la utengenezaji wa vyakula vyaa mifugo. Bila shaka kazi hiyo itakwenda sambamba na kuongeza watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la udhibiti wa vyakula ni tatizo ambalo linazikumba nchi nyingi zinazoendelea. Hakuna mtu anajali kuwa unanunua nini na unakula nini. Vivyo hivyo kwa vyakula vyaa mifugo. Kwa mantiki hiyo, suala la kuwa na watumishi wa kutosha katika Wizara husika ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine naunga mkono hoja hii.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. John P. Magufuli pamoja na Naibu wake Mheshimiwa James Wanyanya, pamoja na Watendaji wao wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mimi napenda kutoa maoni yangu kuhusu sheria ambayo tunataraja baada ya muda, sio mrefu itakuwa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa Sheria hii itakuwa ni mkombozi wa wafugaji kwani imekuwa tatizo kubwa kwa wafugaji kupata soko la kuuza nyama na ndiyo mwanzo wa kupunguza mifugo lakini kwa faida, kwani Serikali itawenza kuwasaidia wafugaji kwa kuwapa mafunzo ya kutosha, kwani mbali na kupata ngozi nzuri ya kuuza, ni vizuri ng'ombe huyo kuwa mnene, kwani hata ngozi yake itakuwa kubwa pia na kumwongezesa mfugaji kipato. Hilo litakuwa ni suala la mafanikio kwani wafugaji wetu wale wa asili hawana utaalamu wa ufugaji wa kisasa. Tunaiomba Wizara iwe ni mwalimu wa wafugaji wa asili na wasiwe sindano ya moto kwa kutimiza sheria kwa kutowaelimisha sheria yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, alama pia ni nzuri kwa utambuzi wa mifugo kwani kwa njia hii mifugo kama itatibiwa ni rahisi kujua ni wapi ipo, kwani kila mmoja atakuwa na alama kwa ng'ombe wake. Pia katika ufuatiliaji wa mifugo, itakuwa bora sana ikiwa ufuatiliaji wa mifugo utakuwa sio wa kero. Watendaji wa mwisho mara nyingi wamekua ni kero katika sheria hutumia nguvu zaidi na hata kuongeza gharama zisizowenza kutekelezwa. Hivyo basi, tunaiomba Serikali kuwa makini sana na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wazi kama Serikali haina eneo la kutosha maana wafugaji hawana mabwawa, madawa na hata elimu ya kutosha na mifugo mingi hulala nje zizini, kwani hawana uwezo wa kuwajengea makazi bora. Hapo basi ubora wa ngozi utapatikana wapi? Hivyo, naomba iwe ni jukumu la Serikali kuwaelimisha zaidi na hata ikiwezekana wafugaji hawa waweze kukopeshwa hata pembejeo, kama ilivyo kwa wakulima. Ahsante.

MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza kwa kuleta Muswada huu muhimu sana kwa sekta ya mifugo.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu ya Tanzania inakisiwa kuwa na ng'ombe milioni 19.1 na ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika kwa wingi wa ng'ombe, hata hivyo ng'ombe (mifugo) au sekta ya mifugo inachangia asilimia ndogo sana kulinganisha na idadi ya mifugo. Kwa hiyo, kutokana na kutungwa kwa sheria hii, itasaidia kuongeza pato la Taifa kutokana na ubora wa mazao yanayotokana na mifugo.

Sheria hii itasaidia sana udhibiti wa magonjwa ya mifugo ambayo kwa asilimia kubwa magonjwa mengi yanaweza kuzuilia kwa mfano magonjwa ya kupe yanazuilia iwapo mifugo itaogeshwa. Kwa hiyo, suala la kufufua na ukarabati wa majosho yote nchini ni muhimu sana ili mifugo iweze kuogeshwa.

Madawa ya tiba na kinga ni muhimu sana yawepo ya kutosha ili mifugo iweze kupata chanjo wakati wa milipuko ya magonjwa. Kwa mfano, magonjwa ya Kimeta (*Anthrax*), miguu na midomo (*Foot and mouth diseases*) na kadhalika.

Hata hivyo, gharama ya madawa (bei) ni kubwa sana. Wafugaji wengi wanashindwa, uwezo wao wa kuyanunua haya madawa ni mdogo. Serikali ingeangalia uwezekano wa makampuni ya madawa yapunguze gharama/bei ya madawa hayo ili wafugaji waweze kununua na kuhudumia mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya utafiti wa mifugo ikiwemo Taasisi ya utafiti wa mifugo ya Kitaifa ya Mpwapwa kuimashwa na kutengewa fedha za kutosha katika bajeti ili kuboresha utendaji na mazingira ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Mifugo kikiwemo Chuo cha Mifugo cha Mpwapwa viimashwe na kutengewa bajeti ya kutosha ili kuboresha mazingira ya vyuo hivyo, pia kuongeza idadi ya Wanachuo ili kupata idadi kubwa ya wataalam na kuwapeleka vijiji kuboresha hali ya ufugaji wa kisasa na kutoa elimu zaidi kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara kwa kuleta Muswada, hongera sana. Ugawaji wa maeneo ya kulisha mifugo ni muhimu sana na uwekewe mkakati maalum ili kuepuka kufukuzwa kila wanapokwenda. Tanzania ina mkakati gani wa kuendeleza bidhaa za ngozi kama jirani zetu Ethiopia? Kama mkakati upo, basi utekelezwe.

MHE. CHARLES N. MWERA: Kwanza napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dr. John Magufuli, Naibu Waziri - Mheshimiwa Dr. James Wanyancha pamoja na timu nzima ya Watendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo una faida nyingi kwa nchi, pamoja na faida za kufuatilia kwa njia ya urahisi tangu mfugo anapozaliwa hadi anapochinjwa au anapoanza kukamuliwa.

Maeneo hasa Mara (Tarime) wananchi hao ndio wakulima na wafugaji, kwa hiyo, ni vigumu sana kutenganisha mkulima na mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu utasaidia sana wananchi (wafugaji). Wafugaji wanaishi maeneo ya mipakani ambapo wizi wa mifugo umeshamiri sana. Mara nyingi wezi wa mifugo hupeleka ng'ombe zilizoibwa kwa masoko ambapo ng'ombe huchinjwa. Kwa hiyo, kuwa na usajili wa mifugo utasaidia wananchi wa Tarime hasa wanaoishi katika mipaka ya Mwema, Sirari, Kata za Pemba, Nyakonga, Nyarero, Nyamwaga, Mariba, Nyanunu, Goringa na Nyarokoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wezi wa mifugo kutoka nchi ya jirani ya Kenya wameiba ng'ombe nyingi sana na kuua raia wengi wasiokuwa na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ya Tanzania na Kenya kushirikiana na kurudisha ng'ombe kwa nchi ambazo ng'ombe zimeibiwa. Kwa nchi ambazo ng'ombe

zimeibiwa kama kutakuwa na ushirikiano huo, basi usajili wa mifugo utakuwa na maana sana. Naishauri Serikali kutafasiri Muswada mara utakapokuwa sheria kwa lugha rahisi kwa Kiswahili pawepo na semina kwa wafugaji ili kuifahamu sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila wananchi kuifahamu hii sheria wananchi wengi wataishia Magerezani. Nina mashaka makubwa, hii sheria inaweza kuwa kero kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijafahamu ni namna gani usajili unaweza ukazuia wezi wa mifugo. Namwomba Waziri wakati wa majumuisho anijulishe ni kwa namna gani usajili utazuia wezi wa mifugo hasa maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi washauriwe kupunguza idadi kubwa ya mifugo ili kupunguza ugomvi uliopo kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa Muswada unaposema kuwa kutengewa sehemu ya kuchungia/kufuga ng'ombe, hayo maeneo yatatoka wapi? Maeneo kama Tarime, haya maeneo yatatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, huo Muswada wa Sheria, naishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wakulima na ufugaji ili kuepusha migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

MHE. SALUM KHAMIS SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wafugaji wetu wauze mifugo yao kwa mizani ili waweze kupata bei stahili ya soko. Pia naomba sana minada yote ya mifugo lazima iwe na mizani za kupimia mifugo ili wasipunjwe tena na wanunuzi. Naunga mkono hoja.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kuileta sheria hii ambayo ndiyo mkombozi kwa mfugaji ambaye amesota kwa miaka mingi bila kupewa hadhi na heshima inayostahili kama Mtanzania mwingine ye yote yule. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sheria ilivyo, yapo mambo ambayo itabidi yawekewe kanuni na taratibu za kuhakikisha kuwa watu wasitumie mianya ya kutumia malisho duni kwa mifugo. Mfano, wananchi mijini ni wajanja sana katika kutayarisha chakula cha mifugo bila kuzingatia viwango.

Kwa sasa kuna wimbi kubwa la wawekezaji ambao wangependa kuanzisha mashamba ya mifungo, lakini miundombinu iliyopo inawakatisha tamaa: Je, isingekuwa jambo zuri kwa Serikali kwa maeneo yote yatakayotengwa kwa ufugaji, ikahakikisha

kuwa mambo yafuatayo yanazingatiwa? Kwanza, ni barabara/reli viwepo karibu; maji/mito/maziwa na malisho mazuri kutegemea uhakika wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri aone uwezekano wa kutumia eneo la Uhuru *Corridor* kwa kufungua mashamba makubwa na hayo yawe rasmi kwa wawekezaji. Maeneo kama hayo yatambulike rasmi na Serikali ili visiingiliane na maeneo ya Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Tanzania isitumie utaratibu wa kukata masikio ya ng'ombe na kuweka alama za utambulisho kama wafanyavyo Ulaya? Nasema hili kwa kuwa wafugaji kama watapewa maeneo yao yaliyopimwa, utaratibu wa kuchoma ngozi “branding” (*primitive way*) tuache kabisa huko tunakoelekea. Uchomaji wa ngozi na kuwapiga ng'ombe kwa kutumia mijeledi ipigwe marufuku, maana unatuharibia ubora wa ngozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala la kuwaweka karibu Askari Polisi wanaoishi mipakani, hawa ni budi tukawa tunawapa ushirikiano wakati wa *operation* zote za chanjo ya mifugo, wizi wa mifugo, matumizi wa alama za mifugo na wakati wa semina za mifugo tuwe tunawashirikisha sana.

Naunga mkono hoja hizi zote mbili.

MHE. GAUDENTIA M. KABAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja hii kwa asilimia mia moja. Nashauri usajili wa kutambua mifugo usifanywe kiwilaya au Mkoa ila kila Kijiji kiwe na alama yake ndani ya Wilaya. Hii itasaidia uthibiti wa karibu wa mifugo na kuzuia wizi kutoka Kijiji kimoja kwenda kingine hasa Wilayani Tarime ambako koo na koo ndani ya Wilaya moja huibiana mifugo hasa ng'ombe.

Wengi ni wafugaji, ni wakulima pia na baadhi ya wafugaji huishi pamoja na wakulima. Kabla ya zoezi la kusajili mifugo hasa ng'ombe, nashauri elimu itolewe kwa makundi yote mawili ili kuzuia mgongano wa maslahi ya kundi moja kufikiria kuwa ni muhimu zaidi kuliko lingine. Hii itapunguza ugomvi wa mara kwa mara kati ya wafugaji na wakulima. Lakini pia elimu hii ilenge kuwashawishi wafugaji kupunguza mifugo yao na kuiboresha kwa malisho bora zaidi ili kupata mazao bora yatokanayo na ufugaji wa maziwa na ngozi.

Nashauri kila mfugaji amilikishwe eneo lake ili kulitunza na kuliboresha kadri ya mahitaji yake kama anavyomilikishwa mkulima. Hii ni kutohana na hali halisi kwa wafugaji kufikiria wana haki ya kuchunga popote penye nafasi ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba nichangie kwa kifupi Muswada huu kwa kutoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Muswaada huu uahirishwe kwani kuna utata ambaao utaumiza wafugaji wetu na kujiona kama hawatakiwi Tanzania, kwani migogoro yao huwa haiishi, hiyo tuahirishe ili sisi Wabunge wao tupatiwe semina ya

kutosha ili tuweze kutoa maoni tuonavyo kulingana na hali halisi tunayoipata toka maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Muswada huu umeletwa kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi: Je, inalenga kuwatenga wafugaji wasipige kura? Nashauri tuwe na subira na kufanya utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema siungi mkono Miswada hii.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma na kurudia tena na tena kuhusu Muswada wa *The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010*, nimeshindwa kuuelewa na kwa hiyo, labda kama kuna maelezo ya ziada kutoka kwa mtani wangu Mheshimiwa Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja hii kwa sababu *timing* yake mbaya uchaguzi kesho kutwa.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Serikali kwa kuileta Miswaada hii miwili Bungeni ili iweze kujadiliwa kisha kutungiwa sheria.

Nampongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Dr. Magufuli na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Wanyancha, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara na Wadau wote walioshiriki kuandaa Muswaada huu wenye malengo maalum ya kuboresha ufugaji wa mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi, sasa nitumie muda wangu kutoa mawazo yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha kuwa mifugo ni chanzo kikubwa sana katika kuinua uchumi wa nchi hii maskini. Hivyo, sheria iwe na meno kuhakikisha wanafuga kwa lengo la kuwaboresa ili wawe na soko la kimataifa kuliko walivyo sasa wanyama wengi, afya zao ni duni kwa sababu ya kufuga kwa mazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ya wanyama ni mzuri sana, ila wasiwasni wangu ni kwamba maeneo hayo yapo? Ninaomba Serikali ilitazame suala hili kwa kina kwani linaweza kuleta migogoro kati ya wakulima na wafugaji kugombea maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika ninashauri maeneo haya yatengwe mbali na makazi, yawe maeneo mapya sio kupokonywa wananchi. Tutaanzisha mgogoro mkubwa sana. Ninashauri tuige mfano wa nchi ya Botswana, maeneo ya ufugaji yako mbali na makazi na mifugo haichungwi, imejengewa uzio. Utaratibu huu unampa mfugaji nafasi hata ya kufanya shughuli nyingine za ufugaji, pia wizi wa ng'ombe nao utapungua ama kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kusajili mifugo mimi linanipa wasiwas sana, kwani mfugaji kuondoka kwenda kusajili mifugo mbali, ni kazi sana. Ningeshauri Serikali iendelee na utaratibu wa kufanya sawa kwa kuwatumi Maafisa Mifugo kama ilivyo sasa. Endapo mifugo itakuwa na maeneo maalumu, basi Maafisa Mifugo itakuwa rahisi kufanya sensa ya mifugo na kumbukumbu hizi ziwepo kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina furaha kukiri kuwa Soko la Mifugo lipo kupitia Minada hadi Vijijini na wananchi wanauza mifugo yao kwenye Minada hii. Hoja yangu ni ile bei ya kununulia mifugo yetu, bado ni ndogo sana kwa kulinganisha na gharama ya kuitunza mifugo. Hivyo, ninaishauri Serikali kupanga bei upya tena kwa kufuata uzito wa mifugo, tena hiyo itasaidia kuweka kumbukumbu za uchumi wa mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa ushauri kuwa utaratibu wanaotumiwa wafugaji kuweka alama kwa kuchana au kuchoma moto ngozi wa wanyama sio nzuri kwani wanaharibu ngozi na kutoa thamani kabisa ya soko la ngozi za wanyama. Hivyo, ninaishauri Serikali kupitia sheria hizi, wabuni njia mbadala ya kuweka alama mifugo kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wafugaji wetu wanapenda kuwa na mifugo mingi hata kama haina ubora. Hivyo, sheria ya kupunguza mifugo ni nzuri, lakini swalii, hiyo mifugo mingi itapelekwa wapi endapo sheria hii itaanza kutumia mapema kiasi hiki? Ninaomba Serikali iangalie namna ya kupunguza mifugo bila kuwadhulumu wafugaji wala kuwapa hasara. Ni vyema Muswada huu usubirishwe ili mazingira bora yaandaliwe la sivyo tutaanzisha migogoro na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mifugo bado inapata magonjwa na ambayo yanaambukiza mifugo mingine na pia kuwadhuru wananchi wanaokula nyama. Jambo kubwa hapa ni kuhakikisha kuna majosho yenyewe dawa pamoja na madawa mengine. Vilevile, taratibu zilizopo bado sio mbaya, mfano kuweka njia za mifugo na kuweka maeneo ya malisho na Maafisa Mifugo kusimamia utekelezaji na Serikali ndiye msimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapata wasiwas sana kuunga mkono Miswaada hii kwani naona bado Serikali haina maandalizi ya kutosha. Hivyo, ni vyema Miswada hii iahirishwe hadi mazingira yatakopokuwa vyema yatakayoleta tija kwa wafugaji, hasa wale wafugaji wadogo wadogo walioko vijijini kazi ianze kwa kutoa elimu kwa wafugaji na sensa ya mifugo yote iliyopo kwa kila Mkoa. Hata hivyo, ninawapongeza kwa kufikia wazo hili, bali tu mazingira hayajakaa vizuri.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara na hususan Mheshimiwa John Pombe Magufuli – Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri - Mheshimiwa James Wanyancha, Katibu Mkoo na Maafisa wa Wizara kwa kuleta Miswaada hiyo Bungeni wakati huu muafaka.

Nimefurahishwa zaidi na Muswada wa *Livestock Identification, Registration* na *Traceability* pamoja na njia zitakazotumika. Hata hivyo, ninashauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa zoezi hili kwa mifugo (*Livestock*) yote, ingefaa kuanza zoezi hili na ngo'mbe amba ni wengi hapa nchini.

Kwa ajili ya *Traceability* wa mifugo ingefaa njia ya *Genetic Markers* pia itumike ili kuweza kufahamu hata koo za mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni sehemu muhimu ya malisho, vipi maji hayakutajwa kabisa katika Muswada wa *Grazing Land and Animal Feed Resources?* Kujenga mabwawa ya maji itafanya wafugaji waweze kutulia katika sehemu moja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wafugaji wengi vijijini kuwa mbumbumbu wa sheria na haki zao za kikatiba, uonevu wa mara kwa mara umewakumba na kupelekwa kudhulumiwa mifugo yao kila siku. Watendaji wasio waaminifu wameshirikiana kuwadhulumu wafugaji.

Hivyo, kifungu 12(3) kingewekwa wazi kujuu huyu katika *Livestock Identification, Registration and Traceability Officer*, madaraka yake ya kuingia mazizini na kukagua mifugo yana *control* gani? Anaambatana na nani? Ana hati zipi? Serikali ya Kijiji inahusishwa vipi katika zoezi hili la “*inspect livestock in the premises to ensure that the provision of this Act are complied with*”?

Nashauri kuwa katika utekelezaji wa madaraka yake ya kuingia na kufanya ukaguzi kuwe na uwazi na mipaka ya madaraka, mamlaka hayo yawekwe bayana. Leo hii ng'ombe wengi wanaokamatwa kwa visingizio mbalimbali zinapotea vituo vya Polisi. Tuna kesi nyingi jimboni ambapo ng'ombe wamepotea vituo vya Polisi au kwa Mkuu wa Polisi wanapohifadhiwa kama sehemu ya *exhibit*.

Sababu kubwa ni ujinga wa wafugaji kwa kutojua haki zao. Nashauri pia kwamba Muswada huu ushirikishe zaidi maoni ya wadau wenyewe. Wataalam wafanye kazi ya ziada ya utafiti kujuu idadi kamili ya mifugo iliyopo nchini na maisha ya wafugaji kwa ujumla. Aidha, kwa kifupi elimu kwa wafugaji bado ni muhimu kabla ya Muswada huu.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kukupongeza kwa kazi kubwa na nzuri katika Wizara yako, ukishirikiana na Naibu Waziri – Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu na watumishi wote walio chini ya Wizara yako. Uwezo wako wa uongozi ni wa kiwango cha juu. Nakutakia kila la kheri katika uchaguzi ujao pamoja na Naibu Waziri tuweze kuonana awamu ya tano kwa msaada wa Mungu. Amen.

Ninachukua fursa hii kuwapongeza kwa Miswada hii miwili ambayo kimsingi ni muhimu na ambayo inagusa sekta kubwa ya uchumi wa nchi. Hata hivyo, maoni yangu kwa Miswada hii miwili ni kama ifuatavyo:-

Ni vyema hii Miswada ingefanyiwa kazi zaidi kwa umakini na kuhusisha wadau wote mpaka yule mchungaji wa kawaida kabisa. Kwani wote wangehusishwa, Miswada hii ingekuwa na sura tofaouti kabisa. Pili, ingekuwa *down to earth* kwa maana ingezingatia hali halisi nchini kwetu na mwisho ingeungwa mkono wa wadau wengi.

Ningependa kufahamu endapo teknolojia ambayo inakusudiwa kutumika kama kumekuwa na *pilot study* au kumefanyika majoribio kuona *whether it is practical*. Hofu yangu, tusitunge sheria ambazo ni *non-starter* ili kuweka heshima ya Bunge letu linalojali wananchi na maslahi ya wafugaji wetu. Je, teknolojia hiyo inafahamika na Waziri husika? Kwani pengine mpaka ianze inawezekana ukawa katika ngazi ya tofauti.

Je, atakayekuwa ana ufahamu? Wataalam hao mpaka kwenye Halmashauri wapo? Au ndiyo tutaanza tena kutumia fedha chungu nzima kwa *seminar za capacity building* ambazo zingetumika kwa huduma nyingine muhimu za jamii kama miundombinu na kadhalika? Kama *una-numbered seminars and workshops on Kilimo Kwanza*, dhana ambayo inafahamika, ila imepewa jina lingine na masuala machache kubadilishwa, nimetoa mfano huu ili tuweze kujifunza, tuepuke makosa hayo hayo. Kumbuka hata wataalam wa mifugo ni wachache Wilayani na hata hao hawana vitendea kazi.

Wilaya ya kilingi ina wafugaji wa jamii zifuatazo Wamasai, Wazigua/Wanguu, Wakaguru, Wabarbaig, Wakamba na kila kundi lina utaratibu na desturi zake za ufugaji. Hivyo, ni muhimu hawa wadau wahusishwe kuitia umoja wao katika maeneo husika, *then we will all be fair*. Kama kada wa juu wa CCM, nataka nikuhakikishie kuwa hawa wafugaji wote ni wana-CCM na wana imani na Chama chao na Serikali yao, naomba tusiwabdalilishe kwa sheria ambazo hawajahusishwa.

Aidha, lugha pia inahitaji *more definitive meanings*, kama *definition* ya *flock* na *heard*. *Why wouldn't sheep fall under herd?* Au *item 5(7) kind of contradicts itself?* Kuna mengi ambayo nitaandika na kuwaletea.

Kwa hekima ya Mungu, kubali Miswada hii irudi ifanyiwe kazi. Wananchi wana imani kubwa sana na wewe. *Please natoa ushauri, kubali irudi tuifanyie kazi.*

MHE. DR. MZERU O. NIBUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri husika, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara hiyo kwa kuleta Muswaada huu muhimu ambao umekuja katika wakati muafaka kwa vile katika kipindi kirefu kumekuwa na mgongano mkubwa kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoamini, huu sasa ndiyo ufumbuzi wa jambo hili, kwa vile tatizo kubwa ni kuwa na mifugo mingi katika baadhi ya maeneo, mifugo ni mingi mno kuliko maeneo ya malisho, hivyo basi, mifugo hiyo huanza kuharibu mazao ya wakulima na hivyo basi, kuleta ugomvi mkubwa mno.

Lakini baya zaidi, inapotokea kesi za namna hiyo, mara nyingi wafugaji ndiyo huwa washindi kwa vile hutumia utajiri wao unaotokana na mifugo na wakulima hunyanyasika na kujiona kama hawana haki ndani ya nchi yao.

Lakini pia baya zaidi ni kwamba, inapotokea mgongano, wafugaji wamekuwa wepesi mno kuanza kulalamika na sauti zao husikika mno kuliko sauti za wakulima. Yote hiyo ni kwamba, kundi hili la wakulima lina watu wazito wenye uwezo mkubwa na hivyo husikika kwa haraka na uzito unaostahili. Ndiyo maana nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni kwa wakati huu.

Naamini Mheshimiwa Waziri tatizo la mifugo analifahamu vizuri zaidi, pengine kuliko mtu mwingine yejote hapa nchini kwa vile katika Tume iliyoundwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume hiyo. Kwa maana hiyo, alijiona mwenyewe kwa kina sana na ndio maana ameonelea Muswada huu uletwe hapa Bungeni.

Naomba kutoa ushauri kwamba usikubali kabisa kuahirisha Muswaada huu muhimu au sivyo utapata laana ya wakulima. Tambua kwamba hivi sasa tunazungumzia Kilimo Kwanza, hivyo hatuwezi kukubali wafugaji wawakatishe tamaa wakulima wetu.

Songa mbele Mheshimiwa Waziri na sisi watoto wa wakulima tupo nyuma yako. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. OMARI S. KWAANGW: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *Part II*, 4(1) (2), 5, 8 na kadhalika, sehemu yote ya *Part II* kuhusu utaratibu wa kuandikishaji na uwekiwa wa alama ni muhimu jamii ihusishwe kwa ukamilifu kwa kuzingatia utamaduni uliozoleka tangu enzi za mababu zetu. Kwa sasa inaonekana bado jamii haina uelewa wa kutosha, elimu kwanza ni muhimu tena kwa miaka kama mitano ili sheria iweze kutekelezeka vizuri. Hivyo nashauri eneo hili litungiwe sheria baada ya jamii kukubali utaratibu utakaoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *The Grazing Land And Animal Feed Resources And Traceability Act*, napendekeza kuondoa section zinazotaja “inspector”, kwa namna ilivyokuwa italeta matatizo makubwa kwa jamii hasa 20(1) na (2). Hakuna haja ya kuwa na ofisa atakayeivuruga jamii kwa madaraka anayopewa ya kuuza mali ya mtu au kumwekea kiwango cha mali yake.

Pia napendekeza Serikali itenye kwanza maeneo ya wafugaji kabla ya kuwazuia kutafuta malisho kwa njia ya kutafuta vibali. Hii italeta mgogoro mkubwa kwa sababu malisho yakikosekana eneo moja, ni lazima wanyama watakwenda eneo lenye malisho na ndipo mgogoro utakapotokea. Miswada hii miwili bado inaonekana ina kasoro katika utekelezaji. Hiyo ni muhimu, kuwe na muafaka ili sheria iwe ya manufaa kwa jamii. Kila la kheri.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wa Wizara kwa kuleta sheria hizi mbili na muhimu na vizuri zimeletwa. Pamoja na yote yanayoonekana na kusemwa kuwa ni mapungufu katika sheria hizi lakini kweli hatuwezi kuendelea kuchunga kwa jinsi tunavyochunga sasa hivi,

lazima tubadilike, na kianzio ni sheria hizi. Ni kweli zinahitaji kuboreshwa, lakini lazima tubadilike na tunabadilike haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yenyeye nia ya kubadili “*mindset*” ya wafugaji ni lazima kama tunataka sheria hizi zipokelewe vizuri na kutekelezwa bila mtifaruku. Serikali isifanye peke yake, vitumiwe vikundi hasa vinavyopokelewa vizuri na wafugaji. Hili litachukua muda, lakini ni muhimu. Serikali itumie watu na vikundi vinavyotokana na jamii za wafugaji wenye, baada ya kuwaelimisha na kuwapa *tours*, watapokelewa vizuri zaidi na wafugaji wenzao kuliko Maofisa wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiboreshe Miswada, lakini iendelee. Naunga mkono hoja.

MHE. YONO STANLEY KEVELA: Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa sheria ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo wa mwaka 2010 (*The Livestock Identificaton Registration and Traceability Bill, 2010*) na Sheria ya Malisho na Vyakula vya Mifugo wa mwaka, 2010 (*The Grazing land and Animal Feed Resources Bill, 2010*)

Kwanza napongeza sana kwa kuleta Muswada huu katika kipindi kizuri cha kilimo kwanza. Nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Magufuli kwa jinsi alivyo mchapakazi mzuri, kwani kila Wizara anayokwenda huwa kunakuwa na mabadiliko makubwa yenyeye faida kubwa kwa Taifa na Kimataifa.

Nampa hongera sana Dr. Magufuli, uzi ni uleule. Pia ameletewa msaidizi wake Mheshimiwa Dr. Wanyancha - Naibu Waziri, naye ni mchapakazi kama yeye. Nawapongeza sana watendaji wake wa Wizara akiwemo katibu Mkuu wake kwa kuuleta Msawaada huu muhimu. Wanachi wa Jimbo langu ni wafugaji na wakulima, hivyo Muswada huu naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Ningependa kushauri kwamba wafugaji watengewe maeneo maalum na mifugo yao idhibitiwe vizuri kutokana na idadi, kwani tukiacha mifugo iwe inarandaranda ovyo kutakuwa na uharibifu wa mazingira, lakini zoezi hili lifanywe kwa umakini mkubwa sana. Hivyo, ni vizuri wakulima na wafugaji washirikiane vizuri kwani wafugaji pekee wakishiriki wenzao wakulima wanaweza kuwanyang’nya maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati husika ilipitia na kujadili na Wizara ikapitisha, ni vizuri tukubali mabadiliko ya kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusajili na kutambua mifugo inakotoka ni muhimu sana ingawa wengi wa wafugaji ni vigumu kukubali mabadiliko haya hata kama ni muhimu. Hivyo, elimu ya kutosha kwa wafugaji ni muhimu sana.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na mpaka sasa wameiweka mahali pazuri sana na inatambulika na inafanya majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zote hizi ni nzuri sana na zenyenye malengo ya kuboresha ufugaji hapa nchini kupunguza kuhamahama kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba tu, kwa kuwa hili jambo ni jipya na zito, naomba elimu ipelekwe kwa wafugaji wa vijijini, waelewe kwamba lengo la Serikali ni jema na pia ni mpango ambao utawasaidia wao kufupa kisasa na kuongeza kipato chao. Pia mahusiano kati ya wakulima na wafugaji yatakuwa mazuri zaidi, maana hawatakuwa wanaingiliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa mia. mia.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, Miswada yote imeletwa kwa wakati muafaka na naunga mkono kwa sababu uharibufu wa mazingira utapungua kwa kiwango kikubwa; kutakuwa na amani na utulivu kati ya wakulima na wafugaji vijijini; mifugo itaboresha na kutakuwa na tija upande wa mifugon a ubora wa ngozi utaboreka zaidi badala ya kuharibiwa kupigwa chapa kila sehemu ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii itasaidia sana kusambazwa huduma za mifugo kwa urahisi kwa sababu uchungaji holela utapungua na kuwa ufugaji mzuri.

Hata hivyo, nashauri kuwepo mpango wa makusudi kutoa elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora. Huduma maalum kama vile chanjo, majosho pamoja na malambo ziwepo na kukamilishwa. Pia kuwe na jitihada za kusambaza elimu ya msingi kwa watoto wa wafugaji hasa mkazo uwekwe kwa wasichana.

MHE. DAMAS PASCAL NAKEI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ili uwe sheria. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dr. John Magufuli - Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kusimamia zoezi hili.

Sehemu ya Tatu ya Muswada huu Part III - vifungu 16 hadi 19 vinazungumzia uwekaji wa mipaka ya maeneo ya malisho. Ni kazi inayotakiwa kufanyika kwa makini. Kwa miaka mingi wafugaji wamekuwa hawana utaratibu wa kutambuliwa maeneo yao ya malisho ya ufugaji, sheria hii ikitekelezwa vizuri itasaidia sana.

Kifungu cha 20 cha sheria hii katika utekelezaji wake inaleta ugumu pale ambapo mwenye mifugo anapolazimishwa kupunguza au kuuza mifugo yake kwa amri ya Mahakama. Hii ni aina ya vitisho. Kipengele hiki ni kama *intimidation and deterrence*. Ni vyema kutafutwe namna bora zaidi ya kutekeleza uwiano wa maeneo ya malisho na idadi ya mifugo, kuelimisha zaidi na kuhamasisha.

Kwa upande wa Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010, umuhimu wake pia ni mkubwa. Muhimu ni kuwezesha utekelezaji kwa makini, mfano *Logistics* za utekelezaji ziwekwe sawa kama vile kifungu cha sita kusajili mifugo ndani ya siku saba: Je, ni *realistic*?

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hizi zina mambo mengi sana ya kufanya katika kuzitekeleza. *Administration* yake ni lazima iundwe vizuri na *administration* hii iende sehemu mbalimbali duniani ili kupata usoefu (*best practice*) mahali pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zote mbili ni nzuri kwa ajili ya *wellbeing and development* ya mifugo yetu kwa kuwatengea mifugo maeneo yao; kuwatayarishia malisho/chakula; kuwakinga dhidi ya maradhi; na kuwapa ulinzi na usalama wao. Lakini mifugo hawa hufanyishwa kazi kubwa kama kilimo, huteswa ama kwa kupigwa sana au kutembezwa masafa marefu, kupelekwa machinjioni. Sehemu hii ya utesaji wa mifugo iko wapi katika sheria hizi mbili?

Baada ya hayo machache, naunga mkono Miswada yote miwili ili kutoa fursa ya kuboresha na kuendeleza sekta ya mifugo nchini.

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wa Wizara kwa kusimamia vizuri ukamilishaji wa Miswada hii muhimu kwa kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa na kutokomeza umasikini.

Napenda kutoa ushauri na msisitizo kuhusu baadhi ya vipengele vilivyomo katika Miswada hii, Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji, ukurasa wa 10 ibara ya 10 kuhusu kazi na madaraka ya Mkurugenzi, inamhusu Mkurugenzi kama Afisa Mwandamizi.

Ushauri wangu ni kwamba kanuni itungwe kuhusu ofisi ya Mkurugenzi na Wasaidizi wake ili madaraka na kazi yake iweze kutekelezwa katika Ofisi za Mikoa na Wilaya.

Madaraka ya Mkurugenzi kukagua minada na sehemu wanazotunza mifugo, kwa kuwa kazi hii ni kubwa hufanywa na Mkurugenzi peke yake, kanuni iandaliwe kuhusu watalaamu wa mifugo ambao watatekeleza madaraka hayo kwa niaba ya Mkurugenzi.

Sheria ya kusimamia na kudhibiti malisho na vyakula vya mifugo na biashara. Sehemu ya tatu kuhusu uendelezaji na usimamizi wa malisho ibara 18, kuhusu Halmashauri kuandaa matumizi ya ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo, Sheria ya Ardhi inazingatia ardhi ya mila inayomilikiwa na familia na wanavijiji.

Wafugaji wengi ni wafugaji na wakulima. Mfugaji anategemea ardhi na mifugo. Kwa hiyo, kuachia mamlaka ya Halmashauri kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi vijijini kwa ajili ya malisho ya mifugo ifanyiwe marekebisho ili iwashirikishe wamiliki wa ardhi ya mila inayomilikiwa na wanafamilia.

Miswada hii ni ukombozi na kiboko ya wezi wa mifugo, inahitaji kuboreshwa kwa kuzingatia michango ya wabunge kuhusu vipengele vyenye utatanishi. Naunga mkono hoja.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuandaa Muswada huu na hatimaye kuufikisha Bungeni hapa.

Napenda pia kuwapa pole kwa kazi mbalimbali zinazotolewa na baadhi ya Wabunge katika kuchangia Muswada huu. Binafsi, naunga mkono hoja hii.

Muswada huu ni mzuri sana na ninafahamu malengo mazuri ya Muswada kwa wakulima, wafugaji na wachungaji. Kwa bahati mbaya, muda huu sio muafaka kwa vile tunaelekea katika kipindi cha uchaguzi kwa bahati mbaya sana baadhi ya matamshi yanachanganya, na hasira zao zinaweza kuelekezwa katika uchaguzi, hivyo elimu inatakiwa kutolewa mapema sana kwa wahusika wote na wadau wa Muswaada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, binadamu kwa asili yake hupaamini na kujihisi yuko salama zaidi mahali alipo na alipopaacha kwa kuwa hapo ndipo anapopahamu. Binadamu ni mwoga kuingia katika eneo asilolifahamu vya kutosha. Kwa ujumla binadamu ni mwoga wa mabadiliko yoyote hata kama kwa siku za usoni yanaweza kuwa ya manufaa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kuwa waandaji wa Muswada huu wa *vision* ya hatima ya Muswada huu ukiwa sheria, natambua jinsi wanavyoumia wanaposikia wanaupinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kitu kinachomuumiza mtu kama mtu kumtendea mema mtu mwingine na anayetendewa wema asitambue kuwa anatendewa wema. Binafsi naiunga mkono hoja kwa vile nimeshafika Botswana na kuona jinsi utaratibu huo wa kugawana maeneo ulivyofanikiwa, ninatamani sheria hii itungwe utaratibu uandaliwe wa kuiwezesha ianze kutumika, hatimaye tuone changamoto zitakazojitokeza na kuzirekebisha mapema. Hatuna budi kuupitisha Muswada huu ili tupate mahali pa kuanzia. Tusiogope mabadiliko, tuyakaribishe ili hatimaye tusonge mbele kimaendeleo katika sekta ya mifugo. Naunga mkono hoja.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza naipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwasilisha Bungeni Muswada huu ambao utekelezaji wake utachangia kupunguza kama sio kuondoa kabisa migogoro kati ya wakulima na wafugaji kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia mifugo kulishwa kemikali zisizofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mapendekezo kama ifuatavyo:-

Sehemu ya pili kifungu 7(3), napendekeza iongozwe (d): “*To inspect livestock units in grazing land*”, kama moja ya kazi ya ‘*Inspector*’. Sehemu ya tatu kifungu 17(2), napendekeza katika kanuni uwekwe utaratibu mzuri wa ‘*Communal ownership*’ kwa sababu bila hivyo inaweza kutokea migogoro au uharibifu wa mazingira na

sehemu ya tatu kifungu cha 20(1): Je, kutakuwepo na idadi ya mifugo itakayoruhusiwa kwa kaya au kwa Kijiji?

Sehemu ya tatu kifungu cha 20(2), ninao wasiwasi kwamba kutakuwepo na mianya ya rushwa na kupunjwa wafugaji endapo Mahakama ndiyo itakayosimamia uuzaji wa mifugo na sehemu ya nne, elimu itolewe ya kutosha kwa wananchi ili waelimishwe, tatizo ni nini endapo watatengeneza chakula cha mifugo kiholela?

Sehemu ya nne 23(2), napendekeza watoaji wa cheti cha usajili kwa watengenezaji wa chakula cha mifugo wawepo kila kanda ili kuokoa muda utakaotumika pia kupunguza usumbufu, kwani kwa siku zijazo wazalishaji wanaweza kuwa wengi, hivyo kumtegemea Mkurugenzi mmoja tu Tanzania kunaweza kusababisha kero.

Mwisho, naipongeza Wizara kwa kazi yake nzuri. Naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya mifugo na uvuvi kwa juhudhi zake kubwa za kuleta mabadiliko katika sekta hii ya mifugo ili iweze kuleta tija na kuchangia uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Utafiti, Usajili na Ufutiliaji wa Mifugo kwa mazingira ya wafugaji wetu na hali ya ufugaji wetu hapa nchini unahitaji maandalizi makubwa sana kabla ya kutekelezeka, japo masuala ya msingi ambayo yanabidi kuwepo kwanza kabla ya kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza utaalam wa hali ya juu unahitajika ili usajili utaratibu na ufuutiliaji uweze kufanyika kwa ufanisi. Wataalamu tulionao ni wachache sana. Pia tunahitaji ofisi zenye vifaa vyote muhimu zikiwemo *Computer* na watendaji wa kutosha ili kuweka kumbukumbu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala haya muhimu sana yanafanyika vijijini, tunafahamu uwezo wa viongozi wetu wa vijijini waliokuwepo wenyeviti wa vijiji na watendaji wao. Elimu waliyonayo ni ndogo sana na mambo haya yanahitaji ufanuzi mkubwa. Kwanza elimu inatakiwa kutolewa ya kutosha kwa wafugaji wote amba ni wadau namba moja na pia kwa wale wote watakoshughulikia utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria/Mswaada umeweuka siku saba kwa wafugaji kusajili mifugo tangu alipowapata. Kwanza kila siku mifugo inazaliwa, inakwenda machungani, inakwenda kufuata maji kilometra kadhaa kutokana na kukosa huduma hizo karibu kwa siku hizo saba. Ina maana mifugo isiende malishoni, iwepo kwenye foleni ikisubiri kusajiliwa, hili siyo rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwepo kikomo cha mifugo nalo siyo halali. Tanzania tuna maeneo kibao ambayo hayatumiki kwa uzalishaji wowote. Serikali iweke utaratibu wa maeneo haya kutumika kwa mifugo na wafugaji wapewe elimu waweze kutulia kwenye maeneo yao. Kuhusu vibali vya kuhamisha mifugo wakati wa kuhamisha

mifugo ni wakati wa ukame hakuna malisho na pia maji. Hivyo ikiwa wafugaji watasubiri kibali na pengine wacheleweshwe au wanyimwe ina maana mifugo itakufa kwa kukosa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaweza kuboresha huduma za mifugo kwa kiasi cha wafugaji kutulia eneo moja. Ili kuondoa matatizo ya kuhama mara kwa mara kwanza kuwepo mikakati madhubuti ya kuhakikisha maeneo ya wafugaji hudumia zote muhimu kwa mifugo ziwepo. Muswada wa kutenga maeneo ya malisho na vyakula vya mifugo, hii itasaidia sana wafugaji kufuga kwa tija na pia kuepusha migogoro kati ya wafugaji na wakulima. Kwa kuwa jukumu la kupanga mpango bora wa matumizi ya ardhi wanaweza kutenga maeneo ya malisho kuendana na idadi ya mifugo waliyonayo ndani ya eneo lao. Serikali kwa kupitia kwa wataalam wa kilimo, watoe elimu ya kutengeneza vyakula vya akiba vya mifugo, mfano Silage, hays na kadhalika ambao kunaweza kutumika wakati wa ukame ili kuepusha kutegemea malisho mabichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wafugaji wanaotamani madawa na *hormons* kukuza mifugo mapema, wapo wanaotumia ARVS na *hormones* kukuza kuku, ndani ya wiki tatu, nne *from day one chick old* analiwa ni nyama. Hii ni hatari sana, kwa afya ya wananchi, watoto wanapata maumbo ya ajabu yasiyoendana na umri wao, watoto wa kiume wanaota maziwa. Hivyo ni muhimu sana Serikali ikafuutilia kujua haya yanayofanywa na watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi izingatiwe kikamilifu na wataalamu wa ardhi na sekta zote zishirikishwe kutenga maeneo ya kutosha ya malisho ya mifugo na kutambulika kisheria (kupatiwa hati miliki) ili kuondoa tatizo la malisho ya mifugo na hivyo kupunguza au kuondoa kuhamahama kwa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Siungi mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa hatua inayofuata naanza kuwaita wenye hoja, nadhani tunaanza na Naibu Waziri, sikupata maelezo basi ni dakika kumi na tano. Sikupata maelezo, kama ningepata ningeambiwa, kama sikupata basi dakika kumi na tano.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi zilizopo mbele yetu. Nianze mchango wangu kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja.

Kabla sijaingia kwenye majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge naomba kwanza kuwashukuru wananchi wa Serengeti tunavyoshirikiana nao na naomba kuwashukuru kwamba lile bwawa letu la Manchira sasa karibu maji yataanza kuingia Mbamu, wavute subira tu kazi ya miaka thelathini imekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kwanza niwashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Maji kwa ushauri wao ambao wametuwezesha kuboresha Muswada huu. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo naomba sasa nitoe maelezo ya hoja ya baadhi ya Wabunge zilizojitokeza katika kuchangia Miswada hii miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema baadhi ya hoja kwani Mheshimiwa Waziri atawatambua wote muda mfupi ujao atakapokuwa anahitimisha hoja hii. Naomba niwashukuru wote waliochangia kwa maneno na wale waliota michango yao kwa kuandika nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lililojiteza katika Miswada hii, ilionekana kwamba ili iweze kuwa na maana kwa wananchi, lazima kwanza elimu itolewe, tunajua hali za wafugaji wetu na hilo Serikali halina tatizo nalo, Serikali imepokea ushauri huu na utatekelezwa katika mpango wakati wa Wizara. Kwa hiyo, naomba kukuhakikishia kwamba elimu itatolewa ili wananchi waweze kuelewa hii Miswada na wasione kwamba inatoa bughudha yoyote. Lingine lilikuwa *traceability officer* katika *section nine* aliteuliwa na kusajiliwa na *director* au kuwepo na *special committee* katika *local government authority level*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa *D by D (Decentralization by Devolution)* inamatka wazi kwamba *local government* wanatakiwa kuteua watendaji wao, lakini nafikiri tutatoa ushauri kwamba pale wanapoteua wateue watu ambao wanafahamu mambo ya mifugo.

Mheshimiwa Dr. Mzindikaya alitoa ushauri kwamba kumbukumbu za *traceabilities* zitunzwe hadi ngazi ya Wilaya, hatuna matatizo na hilo kwa hiyo, mfumo wa kutunza kumbukumbu utawekwa katika kanuni na utakuwa katika ngazi ya mfugaji, kijiji, wilaya,mkoa hadi Taifa.

Lingine lililojiteza ambalo Mheshimiwa Janet Mbene alitoa hoja kwamba nchi jirani zishirikishwe katika kuonisha au *to harmonize* na kutekeleza mifumo ya Kitaifa ya utambuzi na usajili. Ushauri huu unatekelezwa kwa nchi za SADC kuititia mradi wa *print* katika nchi za pembe ya Afrika mradi wa EPICO IEC, *Mifugo Project* ambapo Tanzania ni Mwenyekiti wa *Regional Task Force on LITIC (Livestock Identification and traceability)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Dr. Mzindikaya na Mheshimiwa Rosemary Kirigini ni kwamba *traceability officers* aoneshwe katika kifungu namba kumi na mbili. Hoja hii itazingatiwa katika maandalizi ya kanuni za Sheria na uteuzi wa *Livestock Identification and Traceability Officer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Wabunge wengine walitoa hoja kwamba sensa ya mifugo ifanyike kwanza kabla ya kuanza kutekeleza Sheria hii. Kama tutafanya utambuzi na usajili wa mifugo kwa kweli huu utakuwa ufasaha wa njia mojawapo ya kupata takwimu za sensa ya mifugo, lakini tunatumaini kwamba mwaka 2012 tunatarajia kufanya sensa ya mifugo kwa hiyo, tutaimarisha zaidi. (*Makofii*)

Hoja nyingine iliyojitokeza sana ambayo ilichangiwa na Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Wabunge wengine ni kwamba alama za jadi za kutambua mifugo kama kutumia alama chapa za ukoo, rangi ya mnyama na nyinginezo hazitambuliwi na Sheria hii. Je, kuna uhusiano gani wa utangulizi wa jadi na wa Kitaifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba utambuzi wa njia za jadi, alama za chapa na nyinginezo za kawaida au kisayansi ambazo zipo nyingi kama *genetic maker of gain, A prints, North Prints, Ratina prints etc.* zimeruhusiwa kutumika sambamba na mfumo wa Kitaifa kama *complimentary system*. Hapa ni kwamba zile alama za asili zitaendelea kuwepo lakini tutakapokuwa tunauza hizi za Kitaifa zinatakiwa zitumike sana itahusika hasa tunapokuwa tunauza mazao yetu. Huwezi kwenda kuuza hii nyama EU na nchi zingine bila kuwa na alama hizi ambazo ni *international traceability. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine imetolewa kwamba kutofautisha mifumo ya utambuzi itakayotumika kwa *traditional* na *commercial livestock*. Ni kweli kabisa kwamba mtu wa *commercial livestock* anatakiwa azingatie zaidi hizi mifumo. Kwa hiyo, ushauri utazingatiwa katika Kanuni zitakazoandaliwa kutekeleza Sheria hii ambapo mifumo ya utambuzi itazingatia mifumo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililojitekeza ni kwamba viwango vya adhabu zilizotajwa katika *section 25* ziko juu. Ni kweli lakini ni kwamba viwango vilivyotolewa vimetoa wigo tu mpana kwa Hakimu kuamua kulingana na uzito wa kosa na kuepusha viwango kupitwa na wakati mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limekuja ambalo lilichangiwa na Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na wengine ni kwamba zile siku saba zilizooanishwa katika kifungu cha 6 (4) hazitoshi kwa mfugaji kufanya usajili wa mifugo inayozaliwa na inayopatikana kwa njia mbalimbali. Hoja hii imekubalika na katika kifungu cha 6(iv) kimefanyiwa mabadiliko katika *Schedule of Amendments* na kwa sasa hivi kwa mifugo ambayo itakuwa inaingia kwa mfugaji wakati huo huo amba sheria inatumika itakuwa ni siku 30. Lakini kwa wakati hii Sheria inaanza tutatoa kama miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine iliyojitokeza kwamba njia za mifugo, masoko na miundombinu mingine iandalive sanjari na kuwepo na Sheria hii. Hii hoja ilitolewa na Wabunge wengi. Ushauri huo umepokelewa na utazingatiwa wakati wa utekelezaji pamoja na inavyosimamiwa na Sheria nyingine za sekta ya mifugo na Sheria ya nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililojitekeza ilikuwa kwamba mfumo wa utambulizi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo utaboresha mauzo ya bidhaa za mazao ya

mifugo na hivyo kuchangia katika kuondoa umaskini. Hii hoja ilitolewa na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na tunaiunga mkono na tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba maeneo ya ufugaji (*grazing land*) yawe na miundombinu ya maji, majosho na vitu vingine na kadhalika. Hii hoja ilitolewa na Mheshimiwa Janet Mbene, Mbunge wa Kuteuliwa. Ni kweli kabisa kama tutatenga maeneo ambayo tutatenga ni lazima yawekewe miundombinu ya mifugo kama maji, minada, njia za mifugo na majosho. Aidha, malisho yataboreshwa ili kukidhi mahitaji ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo limejitokeza sana kutoka kwa Wabunge wengi ni kwamba *Inspector* amepewa madaraka makubwa sana na Sheria anaweza akaitumia vibaya.

Naomba kusema kwamba ushauri huo umezingatiwa na kufanyiwa marekebisho ya ziada (*Further Schedule of Amendments*) ambapo sasa madaraka yale ya kwamba anaweza kuingia kwenye mifugo akachukua ng'ombe, akaiza na yule mfugaji akalipa gharama zile sasa yametolewa na kwamba atampa mfugaji miaka mitatu, mara ya kwanza miaka mitatu mingine na kama huyo mfugaji atashindwa kukubaliana na hilo basi itabidi mambo haya yatatuliwe kwa kutumia Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililojitokeza ni kwamba ufugaji huainishwa na rasilimali za malisho ili kupunguza madhara kwa mazingira na watumiaji wengine. Marekebisho ya kifungu cha 20 yatazingatia matumizi endelevu ya asilimia za malisho na kuvuna mifugo ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililojitokeza ambalo lilitolewa na Mbunge Luckson Mwanjale wa Mbeya Vijijini ni kwamba udhibiti hafifu wa vyakula vya mifugo na upatikanaji wa wataalam wa vyakula vya mifugo. Alisema kwamba kuna udhibiti hafifu wa vyakula vya mifugo na upatikanaji wa wataalam wa vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii imeweka utaratibu wa kusimamia utengenezaji na uuzaji wa vyakula vya mifugo. Aidha, Wizara inaendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani walio katika Halmashauri ili kupata ujuzi wa kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia ningependa tu kutoa *summary* kwamba Miswada hii kwa sasa hivi inaweza ikawa na kasoro ama haina lakini kwa kweli jamani mambo kama ya *traceability* na *registration* bila kuitisha huu Muswada *at a long run*, ni kwamba hatuwezi kuuza nyama nje, EU wala hatuwezi hata kama ni Uchina, hata Uarabuni ambapo sasa hivi wanapeleka. Haya ni mambo ambayo kabisa ni lazima yazingatiwe. Kitu kinachotakiwa hapa ni namna ya kuhakikisha kwamba Muswada unaenda vizuri, na hauumizi wananchi. Lakini ni kitu cha muhimu kabisa, bila hivyo tunajenga pale kiwanda Ruvu, ile itakuwa *White Elephant* kama hiyo haipo. Hakuna mtu ananunua nyama aende kula hajui imetoka wapi.

Kuhusu Sheria ya malisho, Waheshimiwa Wabunge wafugaji, mimi ni mfugaji, natoka na nimezaliwa katika sehemu ya wafugaji. Tumeumia sana, leo ukienda hapa unafukuzwa. Unasema lazima utoke upishe, unaenda *Game Reserve* lazima utoke upishe mwekezaji, utoke upishe wakulima. Hii ndiyo itawapa wafugaji uwezo wa kuwa na maeneo yao. Mtu yejote akiingia pale wanasema hapana hili ni eneo la wafugaji. Kwa hiyo, watatulia na hawatabughudhiwa tena, wataishi tu na kulala. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa ufupi ni kwamba Miswada hii tunachoweza kufanya sana ni kuboresha vifungu na ambavyo tumejitahidi lakini ni muhimu sana kwa Watanzania ili tuweze kwenda na karne ya 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijaanza kuchangia na kujibu baadhi ya hoja katika Muswada huu umechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 54. Waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni ni 28 na waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 26. (*Makofi*)

Ningeomba nianze kuwataja, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, ambaye wote ni kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati ya Maji, Kilimo na Mifugo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Wengine ni Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa Kaika Telele. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Tatou Ntimizi, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa pamoja na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. (*Makofi*)

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Salum Mohamed Salum, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Omari Nibuka, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi na Mhesihmiwa Magdalena Sakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Miswada yote hii miwili na nawapongeza sana. Nchi yetu wakati tukipata Uhuru eneo lake bado ni hilo hata baada ya kupata Uhuru. Wakati tukipata Uhuru nchi yetu ilikuwa na ukubwa wa kilometra za mraba 949,000, wakati huo tulikuwa na ng'ombe milioni 8, watu walikuwa milioni 9, leo watu wako zaidi karibu milioni 40 na ng'ombe kutokana na sensa ya mwaka 1984 ndiyo hao tulionao amba ni ng'ombe zaidi ya milioni 19.1, mbuzi milioni 13.6, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.4, kuku zaidi ya milioni 57, mbwa milioni 4 na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba tumekuwa na ardhi, matumizi ya ardhi yamekuwa yakiongezeka lakini ardhi imekuwa hiyo hiyo. Na hapa ndipo chanzo cha matatizo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba kutokana na hiyo hali na kutokana na hizo changamoto zote ndiyo maana palipitishwa Sheria Namba 4 ya Ardhi ya mwaka 1999 na baadaye pakapitishwa Sheria ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 na baadaye tena ikaletwa Sheria Na. 7 na Na. 8, Sheria Na. 7 ya mwaka 2007 ni ile ya matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, hizo zote zilikuwa ni changamoto katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na matumizi bora ya ardhi katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika changamoto kubwa ambazo tumekuwa nazo pamoja na kwamba tumekuwa na ng'ombe wengi kiasi hicho katika nchi yetu na kwamba sisi ni wa tatu katika Afrika. Lakini ni ukweli usiopingika kwamba bidhaa hii, mifugo hii imekuwa iki-*contribute* kiasi kidogo sana katika *GDP* ya nchi yetu.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita *contribution* katika *GDP* inayokuwa *contributed* na mifugo ni asilimia 4.7 tu. Lakini hii haiachi ukweli kwamba mifugo imekuwa ikisaidia sana wananchi wote wa Tanzania. Kwa sababu kama mazao yote ya nyama, maziwa, mayai kama tungkuwa tunayaagiza kutoka nje karibu kila mwaka zingekuwa zinahitajika karibu zaidi ya trilioni 35 kwa ajili ya kuagiza bidhaa hizo. Kwa hiyo, hivi ndivyo vitu muhimu ambavyo tunatakiwa kuvizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na ukweli kwamba sisi kama *contribution* ya mifugo imekuwa ni ndogo sana katika kusafirisha na kuuza mifugo yetu nje ya nchi na ndiyo maana pamekuwepo na masuala mbalimbali katika kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya mifugo. Ili sekta hii iweze kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi yetu na hasa kwa kuzingatia kwamba kwa sababu tuna mifugo mingi na ndiyo maana katika mwaka 2006 palipitishwa sera ya mifugo. Lengo kubwa ilikuwa ni kuhakikisha kwamba mifugo hii inatumika kikamilifu kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri wakati ikipitishwa hii sera ya mifugo ilijadiliwa na wadau katika mikoa yote wanaohusika na masuala ya mifugo. Ndiyo maana baada ya hapo pamekuwepo na sheria mbalimbali ambazo zimeweza kupitishwa katika kuhakikisha kwamba sasa wafugaji wanapata faida kubwa kulingana na mifugo yao.

Ieleweke kwamba pamoja na kuwa sera ya mifugo ya mwaka 2006 lakini ni ukweli usiopingika kwamba tangu wakati huo mpaka sasa hivi eneo ambalo limeshatayarishwa kwa ajili kulishia mifugo ni hekta milioni 1.3 tu, wakati maeneo yanayofaa kwa ajili ya kulisha mifugo ni karibu hekta milioni 50 katika nchi.

Lakini tukiangalia katika maeneo ambayo yametayarishwa kwa ajili ya kilimo na maeneo kwa ajili ya wanyamapor, yana eneo kuliko maeneo ambayo yangeweza kufaa kwa ajili ya mifugo na ndiyo maana Sheria hizi zote zililetwa hapa ili kuhakikisha sasa wadau hawa wa mifugo amba ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu wanawekwa sawasawa lakini pia kumaliza kabisa migogoro.

Hii inaendana na baadhi ya sheria ambazo tayari zimeshapitishwa, zinazoendana na mifugo ambayo ni pamoja na Sheria ya *Veterinary Namba* 16 ya mwaka 2003, Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Namba 17 ya mwaka 2003. Sheria ya Nyama Namba 10 ya mwaka 2006, Sheria ya Maziwa Namba 8 ya mwaka 2004, Sheria ya Ngozi ambayo tumeipitisha hivi karibuni Namba 18 ya mwaka 2008 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama Namba 19 ya mwaka 2008. Hivi vyote ili kusudi viweze kukamilika vizuri basi ilitakiwa ziende na hizi Sheria mbili ambazo tumeziwasilisha hapa. (*Makofi*)

Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri wenzangu waliotangulia katika kuweka michakato mizuri ya kuhakikisha kwamba Sheria hizi ambazo nimezitaja zimepita pamoja na Sera ya Mifugo ambayo wakiwepo Mheshimiwa Edward Lowassa ambaye alikuwa Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Dr. Dr. Charles Mlingwa amba kwa kweli sheria hizi zote ndiyo zimeleta mchakato mzuri wa kuleta sheria hii ambayo tunaamini kabisa ni sheria hii pekee ambayo ingeweza kuwasaidia wananchi. Ni kweli kabisa utungaji wa Sheria ni kitu kigumu sana.

Hili mimi nime-*prove* leo kwamba utungaji wa sheria ni vigumu na ndiyo maana hata Mwenyezi Mungu alipokuwa akiweka masharti yale 10, zile amri 10 hakuauliza watu, alimwita tu Mussa kule mlimani akamwambia chukua hizi amri 10 usizini, usiibe, usifanye nini pamoja na kwamba Mussa mwenyewe katika maisha yake ya nyuma alikuwa ameshawahii kuua, angeweza kuulizwa kwamba achague hizi sheria kwamba ni ipi ambayo asiichukue, inawezekana Sheria ya kuua asingeweza kuichukua. Lakini kwa sababu sheria ina masuala yake na ndiyo maana pamoja na kuwa na hizo sheria 10 bado watu tunazini, bado tunaiba, bado tunatamani wake wa watu. Bado tunatamani na kadhalika na kadhalika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi niliamini kabisa kwamba kupidishwa kwa sheria hizi haikuwa ndiyo mwisho wa mambo mengine yote, kwa sababu bado palikuwa na masuala mengi ambayo tungeweza tukayaweka kwenye *regulations* katika kuhakikisha kwamba sekta ya mifugo inaweza sasa kuleta changamoto kubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwa sasa hivi hatuwezi tukauza nyama katika soko la *European Union*, ni kwa vile hatuna sheria hizi za *traceability, traceability* maana yake lazima wa-*trace back* hata mfugo kule ulikozaliwa na ulikotoka, sasa kwa

sababu hii inatuwia vigumu kufanya biashara na hivyo sekta ya mifugo inakuwa vigumu sana kuweza kuchangia katika Pato letu la Taifa. Kutokana na kutopitishwa kwa Sheria hizi sisi nchi yetu hatuwezi tukauza maziwa katika nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Egypt kwa sasa hivi inahitaji nyama nyingi tu kutoka Tanzania, lakini wanaagiza nyama kutoka India na kutoka India kwenda Egypt ni mbali zaidi kuliko kutoka Tanzania kwenda Egypt na sisi ni watatu katika Afrika kwa kuwa na wanyama wengi. Lakini ni kwa sababu tumeshindwa kuendana na masharti ya dunia inavyotaka sasa hivi ambapo nchi zingine kama Botswana, Namibia zimeshaanza kuzingatia masharti haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwamba *concern* ya Waheshimiwa Wabunge na michango yao mizuri sana katika Muswada huu na mimi nawapongeza sana wote na ndiyo maana katika michango mingi ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge tumejitahidi sana sisi kama Serikali kufanya mabadiliko mengi sana. Hata lilie suala ambalo lilikuwa linazungumzia katika Fungu la 20 ambalo lilikuwa linazungumzia juu ya *Inspector* tumejaribu kulirekebisha ili kusudi huyu *Inspector* kwa sababu jukumu la Bunge hili ni pamoja na kutunga Sheria na ndio maana nasema nimefurahia michango yote ya Waheshimiwa Wabunge.

katika fungu la 20 ambalo lilikuwa linazungumzia juu ya *Inspector*. Tumejaribu kulirekebisha ili kusudi huyu *Inspector*, kwa sababu jukumu la Bunge ni pamoja na kutunga sheria na ndio maana nasema nimefurahia sana michango yote ya Waheshimiwa Wabunge. Tukasema angalau sasa *Inspector* anaweza akatoa *notice* ya miaka mitatu, lakini bado tena anaweza akaongeza *notice* nyingine ya miaka mitatu. Ukijumlisha miaka mitatu na miaka mitatu ni miaka sita, maana yake ni kwamba tutachaguliwa, tatarudi tena, tutakuja kuchaguliwa, bado hiyo *notice* imesimama tu. Sasa vitu kama hivi ambavyo Serikali ilikuwa imevikubali ili kusudi angalau wenzetu ambao ni wadau wakubwa katika sekta ya mifugo, tuanze kuuza mifugo yetu na mifugo yetu sasa ianze kuleta mafanikio katika nchi yetu. Tumeyafanya haya kwa kuzingatia ushauri mzuri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika lile suala la kutambua zile alama za jadi kama za watani zangu wamasai, zimeandikwa kwenye Muswada wetu, katika ukurasa wa nne na ninafikiri mkifunua pale mtapaona. Kwa kuzingatia muda, nisingependa niusome wote. Umeeleza kwa kuzingatia kwamba weka alama zako za kijadi, lakini pia zile hazizuii kuweka alama nyingine za kitaifa. *Experiment* hii tumeifanya katika Wilaya ya Rarya na Tarime, na ambayo mafanikio yake wameyaona. Sasa sisi tulitegemea hii itazuia wizi, itazuia mifugo yetu, sasa inakuwa *traceable* vizuri, tutafanya biashara, ng'ombe wetu tutaanza kuwauza nje, wafugaji wote, Wasukuma, Wamasai, Wakurya na wengine, nao wataanza kupata fedha. Lakini sasa kutopitishwa kwa sheria hii, kutopitishwa kwa Miswada hii, tumejifunga wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linajionyesha wazi, hata katika biashara ya samaki. Samaki wetu sangara, walikuwa hawanunuliwi katika soko la *European Union*. Tulipokubali masharti yao na kuleta sheria hapa ikiwa ni pamoja na sheria Na. 22 ya mwaka 2005, samaki wamenunuliwa sana. Na ndio maana tumekuwa tunaona ndege zinakuja kuchukua samaki aina ya sangara, wanakwenda kuliwa *Europe*. Na ndio maana katika mwaka mzima wa jana, nimeingiza shilingi bilioni 224 kwa samaki tu. Sasa sisi kama Serikali tulifikiri kama Miswada hii ingepita, kama palikuwepo na matatizo mbalimbali ambayo yangeweza kujitokeza, mimi nilikuwa niko wazi kukaa pia na Waheshimiwa Wabunge, wakati tunapopitisha *regulations*, kusudi tuzipitishe kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ni-*declare interest*, mimi ni mtoto wa mfugaji, lakini pia ni mtoto wa mkulima, kwa hiyo, nimechunga tangu darasa la pili. Ninafahamu ng'ombe, ninafahamu hata majina tulivyokuwa tunawaita, bugondo, mukara, mapembe, nawafahamu. *Of course* siiti kimasai, lakini ninaita kwa lugha yetu. Ninafahamu namna ya kumkamua ng'ombe, ninafahamu hata ng'ombe anapomkataa mtoto nifanye nini ili yule mtoto aweze kukubalika kunyonya kwa mama. Hizi zote ninazifahamu. Sisi katika Muswada huu tuliamini kabisa kwamba kwa kushirikiana na hizi teknolojia za asili ambazo tungeweza kuziweka kwenye *regulations*, zingeweza kuboresha mifugo yetu kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema suala la kupitisha sheria ni gumu. Na ni gumu kama ambavyo nimetoa katika amri kumi za Mungu kwamba, nazo ni ngumu hata kuzitekeleza tu. Lakini inawezekana pia hata katika sheria ambazo tumewahi kuzipitisha hapa, bado zinaweza pia kuonekana ni ngumu kama mtu anaweza akazipitia na zikaonekana zina dosari.

Lakini ninachotaka kusema kwa dhati ni kwamba tumeheshimu sana michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu michango yao ni mizuri. Sisi kwa upande wa Serikali tunaamini kabisa kwamba Sheria au Muswada unapoletwa Bungeni, lengo lake kubwa ni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Hatutungi Muswada au sheria kwa ajili ya kumkomoa mtu. Lakini pia niliamini katika suala kubwa ambalo lilikuwa linawasumbua wafugaji kwenye masuala ya malisho, huu Muswada kama ungepitishwa, ukweli ndio ungekuwa kitanzu kwa upande wa Serikali kwa sababu, huwezi ukatoa amri ya kusema ng'ombe hawa wahamishwe wapelekwe mahali fulani wakati kuna hii sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninataka nieleze sheria ile ya ustawi wa wanyama, ilisaidia sana na ndio ambayo imekuwa inatusaidia sasa hivi katika kutokufanyika *operations* za ajabu ajabu. Kwa sababu huwezi ukamchukua ng'ombe akakaa masaa mawili bila kunywa maji. Kwa hiyo, hata Serikali haitakiwi kuvunja sheria, hata watendaji hawatakiwi kuvunja sheria.

Sasa kwa sheria hii ambayo kwa vyovyyote Serikali ingebidi kuweka fedha kwa ajili ya kutayarisha maeneo ya malisho ili kusudi yaende sambamba na maeneo ya malisho ambayo ni ya wakulima. Ingewezekana pia katika kupitisha sheria hii, hata maeneo mengine ambayo yalikuwa ni ya misitu, yangeweza kutengwa kwa sababu

Serikali ni moja. Mimi niliamini kabisa suala la wafugaji lingekuwa limepata *solution* yake, lakini pia suala la migogoro ya wakulima nayo ingekuwa imepata utambuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi, ninazungumza kwa jumla, wamezungumza kwamba wafugaji watakuwa wanalazimishwa kuwa na mifugo kadhaa. Hii sio kweli. Sheria hii inasema wazi mtu anaweza akawa na mifugo hata kama ni 1,000,000 hazuiwi kuwa na mifugo yoyote, ilimradi awe na eneo. Na eneo maana yake lingeweza kupimwa. Lakini katika sheria hii ndio maana imeweza kuoanishwa na sheria ya ardhi ambayo ipo, sheria Na. 4 na sheria ya vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, pamoja na sheria ya matumizi bora ya ardhi Na. 7 ya mwaka 2007. Hizi sheria ni muhimu kwa sababu ni sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, tumezipitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu *concern* nyingi za Waheshimiwa Wabunge, lakini sisi kwa upande wa Serikali tumejitahidi sana katika kufanya *amendment*. Hata katika zile siku saba za kuzipunguza, tumesema sasa zitakuwa zinafanyika; na zile ni kwa wale wenye ng'ombe ambao wamewanunua, kwamba zitakuwa siku 30. Lakini tulikuwa tunajua kwamba katika *regulations* kwa wale wenye mifugo yao tungeweza ku-*extend* hata miezi sita hata mwaka, kwa sababu *regulations* ni zile ambazo tunazitunga sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu Serikali ya *CCM* ni Serikali sikivu, inaheshimu michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge wa Vyama vyote, inapenda kuona kwamba Sheria yake inayotungwa inaleta manufaa kwa wananchi wake, na kwa sababu jukumu la kutunga sheria ni jukumu la Bunge hili na sio mtu mwingine, na Bunge hili ndio lenye mamlaka ya kufanya *amendments*, *ku-add*, kufanya nini, kwa sheria yoyote inayotungwa, sisi kwa upande wa Serikali, tumetafakari na hasa niseme mimi mwenyewe pia nimetafakari sana na hasa kwa kuzingatia kwamba na mimi mwenyewe ni mfugaji, na kwa kuzingatia ibara ya 87 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 207, napenda nitamke wazi kwamba naomba Miswada hii yote miwili niirudishe kwenye Kamati ili ijadiliwe, iwekewe nguvu zote kwa manufaa ya wafugaji na wakulima.

Ni matumaini yangu kwamba Miswada hii itawekewa hizo nguvu zote kwa manufaa ya Watanzania wote, ili twende kutekeleza vizuri Ilani ya *Chama Cha Mapinduzi* ambayo katika Ilani yake ya mwaka 2005, inazungumzia juu ya suala la mifugo. Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja Iilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Miswada iliyotajwa, ilirudishwa kwenye Kamati, kwa ajili ya kujadiliwa tena*)

NAIBU SPIKA: Hoja ya mwenye hoja sio lazima iungwe mkono. Nimewauliza *just* kujiridhisha kwamba kweli alichokisema Waziri? Haihitajiki kwa sababu mwenye hoja ndiye anayeiondoa katika *stage* hii, ama *stage* nyingine yoyote, angeweza kusimama na kusema naiomba Kamati iweze kurudia hiyo kazi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nadhani Ofisi yangu itashirikiana na Serikali kuona ni nini kitakachotakiwa kufanyika. Lakini nadhani kikubwa hapa ni ushirikishaji. Nadhani kile kifungu chetu cha *Public Hearing* ni muhimu sana na wakati mwingine tusifanye *Public Hearing* kwa watu wa Dar es Salaam tu, ni vizuri tukaenda zaidi kunakostahili.

Baada ya kusema hivyo, ninaomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kusema kwa ufupi sana. Kwanza nataka niungane na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kuwashukuru kwa michango mizuri. Haikuwa Miswada myepesi sana, kidogo ilikuwa ni migumu kwa sababu inagusa maslahi ya wafugaji kwa upana wake. Lakini tumeona ni vyema baada ya kuwasikiliza na kusikiliza maoni ya baadhi ya Wabunge, ambayo tumeyaona ni mazito, tukafikiri njia nyepesi ya kuweza kufika mahali na mkaelewana vizuri na Bunge, ni kurudi kwenye Kamati na tujaribu kuyafanya kazi tena haya mawazo yote kwa ujumla, halafu tuombe tena kuweza kurejea hapa tukiwa na *spirit* moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili vilevile nataka niseme kwamba wakati tunafikiria kutunga sheria hii, nadhani vilevile ni jukumu kwa upande wa Serikali, nasema baadhi ya maeneo ambayo tumeyafanya marekebisho ni kwa kutambua kwamba changamoto zilizoko mbele yetu kwenye sekta ya mifugo ni kubwa. Nimewahi kusema, mimi naona ni rahisi zaidi ninapozungumza na wakulima kwa sababu mambo yao ni yale ambayo yanaweza kubadilika kwa urahisi. Lakini kwa upande wa sekta ya mifugo, mapendekezo ambayo yameingizwa kwa maana ya marekebisho. Nadhani vilevile yataisaidia Serikali kuweza kujipanga vizuri, tuweze kwenda hatua kwa hatua katika masuala yote ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi mmezungumza juu ya elimu ambayo ni kweli tutahitaji kutoa elimu kubwa. Lakini vile vile ni lazima tukubali, kama nilivyosema leo jioni, katika kipindi hiki vilevile Wizara itabidi ijaribu kuja na mpango wa kuendeleza sekta ya mifugo peke yake. Mpango ambaao utajaribu kuainisha mambo yote na tuweze kuzingatia hata namna tunavyoweza kutekeleza sheria hizi nyingi ambazo tumezipitisha. Maana unaweza ukawa na sheria hata 40, lakini kama hamna mpango mzuri wa kuendeleza sekta hiyo, unaowiana na hiyo sheria, mnaweza mkakuta hazifanyi kazi. Kwa hiyo, ninadhani ni nafasi nzuri vilevile kwa upande wa Serikali kuweza kupata nafasi ya kuifanya kazi hiyo kwa umakini zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ninataka niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane katika jambo hili. Waziri amelieleza vizuri, ni kwa manufaa ya Taifa letu, tungependa kuona sasa mifugo iliyo bora zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Kuna

wakati Mheshimiwa Rais aliwahi kusema unamwona ng'ombe mwenyewe kakonda na mfugaji mwenyewe na yeze kakonda; sasa hatuwezi kuendelea na jambo la namna hii. Kwa hiyo, ni lazima sasa tufike mahali tupige hatua ya kuboresha mifugo yetu kwa manufaa ya Taifa, na hii ndio itawasaidia zaidi wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini fursa zipo, tukijipanga vizuri tutaweza. Mifugo kama ilivyo sekta ya kilimo kwa upana wake, kilimo cha mazao lakini vile vile uvuvi, ndio eneo kubwa sana ambalo Watanzania wengi tunashughulika nalo. Ndio maana tunatwanga maji kwenye kinu tunapopambana kupunguza umasikini bila kujikita hasa kutoa majibu kwenye maeneo haya makubwa matatu, manne; kilimo cha mazao, ufugaji, uvuvi, urinaji asali na shughuli nyingine ambazo zinamgusa Mtanzania moja kwa moja. Bila kuelekeza nguvu zetu huko, bila kujipanga vizuri kwenye maeneo haya, kusema kweli umasikini mtaendelea kuusema hivi hivi, lakini hatutaona umetoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, karibu nchi hizi zote ndogondogo nilizotembea, ambazo sasa zimepiga hatua kubwa, zimekuwa ni nchi za wakulima kama sisi, tena masikini kama tulivyo sisi. Miaka ya sitini tu hapa, lakini leo wako mbali kabisa na sisi. Lakini nguvu kubwa waliweka katika kilimo. Kwa hiyo, ninawaombeni sana tutakapopata nafasi ya kuirejesha sheria hii, ni tumaini langu kuwa hata Bungeni tunaweza tukairejesha wiki ijayo kama tutakubaliana mapema, kubwa tuone kwamba ni kwa manufaa ya kusaidia sio wananchi tu kama wafugaji, lakini kubwa kama Taifa. Kwa sababu ni aibu sana, sisi Tanzania hatuwezi kuwa tunalinganishwa na vinchi kama Namibia, Botswana, kwa nini? Sioni sababu hata kidogo! Kwa kweli, tungepaswa kuwa kwa kweli ni Taifa kubwa kwa utajiri tulionao. Kwa hiyo, tukijipanga vizuri, nina hakika tutaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarejea kuwashukuru na niwaombe tu Waheshimiwa Viongozi wenzangu wa upande wa Serikali, basi tujipange vizuri tuone namna tutakavyoweza kushirikisha Wabunge wengi, hasa wale wanaotoka kwenye maeneo ya ufugaji, tujaribu kuzingatia vizuri kwa mitiririko mzuri yale maeneo yote ambayo watu wanaona yakiwekwa yatakavyokuwa yamewekwa, tuna hakika mchakato wa kuleta maendeleo kwa wafugaji utakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, narejea kusema ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa maelezo ya ziada kuhusu hatua tuliyofikia kwenye Miswada yetu muhimu ya wafugaji. Sasa nina matangazo machache.

Asubuhi, tulikuwa tumetangaza kwamba kikao cha Kamati ya Uongozi ya Chama Cha Mapinduzi, wangekutana saa 2.00 baada ya kuahirisha shughuli. Sasa tumeahirisha, kwa hiyo, mkitoka hapa wale Wajumbe wa Kamati ya Uongozi watakuwa na kikao kwenye Ukumbi wa *Speaker's Lounge* baada ya kutoka hapa tu. Kwa hiyo, tufanye mapema zaidi kuliko ile saa mbili tuliyosema.

Lakini pia saa 5.00 Kamati ya Uongozi ya Bunge ilikuwa imekaa kujaribu kuangalia ratiba yetu. Bahati mbaya mimi nilikuwa hapa, lakini maelezo tuliyopewa ni kuwaambia kwamba kesho tutakuwa na kipindi cha maswali kama kawaida, lakini tutajadili Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Mitaji na Dhamana wa mwaka 2010, yaani *The Capital Markets and Securities Amendment Bill 2010*. Halafu pia tutakuwa na Azimio la kuongeza Mtaji wa Mfuko wa Dhamana. Sasa mnakuta kwamba haya hayakuwepo jana, yaani mkiangalia ratiba mliyopewa ilikuwa ni Muswada mwingine. Kwa hiyo, mjiandae kwa Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Mitaji na Dhamana wa mwaka 2010 na Azimio la Kuongeza Mtaji wa Mfuko wa Dhamana. Hii ninaisema hivyo kwa ajili ya Wenyeviti wanaohusika na maoni ya Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, mtakuwa na kazi ya ziada, kwa sababu muda mliopewa ni mfupi. Kwa hiyo, mjiandae kwa hilo.

Lakini pia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, inapenda niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, kwamba siku ya Jumamosi kutakuwa na tamasha la watoto kwa ajili ya kulipongeza Bunge na Serikali kwa kuitisha Sheria ya Kumlinda Mtoto ya mwaka 2009. Tamasha hilo litafanyika hiyo tarehe 17 Aprili, 2010 katika Uwanja wa Jamhuri, kuanzia saa 2.45 na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndio atakuwa Mgeni Rasmi. Kwa hiyo, Wabunge wote mnakaribishwa kwa hilo Tamasha. Mnafahamu tarehe 17 itakuwa ni Jumamosi, kwa hiyo, saa 2.45 asubuhi, wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba pia niwashukuru kwa kazi mliyofanya leo na hasa kwa michango mizito mliyoitoa katika Miswada ile miwili kutoka jana na leo. Mtakubaliana na mimi kwamba wote tumejifunza mengi sana kutokana na majadiliano haya tuliyokuwanayo. Na isingekuwa hivyo, tusingejifunza kitu. Kwa hiyo, ninawashukuru sana kwa elimu tulioipata. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba niwatakie jioni njema. Ninaahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.04 Jioni, Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,
Tarehe 16 Aprili, 2010, Saa Tatu Asubuhi)*